KUNG'ANG'ANIA

Asante, Ndugu Neville. Bwana akubariki. Asante.

Habari za asubuhi, marafiki. Ni majaliwa kuwa hapa asubuhi ya leo katika Uwepo wa Bwana, maskanini pamoja na watu. Na ni siku ya mvua nje, nami ndio kwanza niingie kwa gari sasa hivi, na jinsi mlivyokuwa mkiimba na kupiga makofi, hapana budi wana manyunyu ya baraka ndani. Kwa hiyo hilo ni zuri sana. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa ajili ya siku hii. Ni. . .Hatuna budi kuwa na mvua. Tusipokuwa na mvua, basi Bwana hawezi kuyakusanya matunda Yake. Kwa hiyo tuna m— mvua ndani, kiroho, la sivyo hakutakuwako na matunda yoyote kwa ajili ya mavuno. Inatupasa kuwa na mvua huku nje la sivyo hatutapata mavuno ya kawaida. Hiyo ni kweli.

2 Basi, mwajua, zote mbili, inahitaji kitu kilichokufa tupate kuishi. Mavuno huleta uhai, nao uhai hauna budi kusababisha mauti. Kupitia mauti sisi huishi. Mwajua, kila siku, kwa maisha yako ya kawaida, kitu fulani hakina budi kufa upate kuishi. Inakubidi. . .kitu fulani hufa. Kwa hiyo wewe—wewe hula na kuishi kwa vitu vilivyokufa. Ukila vipande vya nyama ya nguruwe, nguruwe alikufa. Ukila steki, ng'ombe alikufa. Ukila mahindi, yalikufa. Ukila mkate wa ngano, vema, ilikufa. Ukila sukumawiki, ilikufa. Unaishi kwa kitu kilichokufa, kwa kawaida. Basi, hilo si ni thibitisho kwamba ilipasa Kitu fulani kife tupate kuishi Milele? Kristo alikufa, Mwana wa Mungu, tupate kuishi Milele. Kwa hiyo nina furaha sana kwa ajili ya hayo yote asubuhi ya leo, kujua kwamba nyakati hizi za maafa makubwa tunazoishi sasa, na kujua kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya wenye dhambi, na huyo alikuwa ni mimi, kwamba Yeye alikufa kwa ajili yangu.

3 Sasa, nadhani Jumapili iliyopita mnakumbuka ya kwamba Bwana siku chache zilizopita alinena nami na kusema tutaninii. . .Mnaona kwenye kanda ya Jumapili iliyopita maafa yalikuwa yanakuja. Nikishuka tu huku nilikuwa nikisikiliza matangazo, na Ujerumani imepata mafuriko mabaya sana waliyowahi kupata katika taifa hilo. Yameua maelfu, na watu hata wanajiua wenyewe. Niliandika hili, nikishuka huku. Nayo maboma ya kuzuia maji yakapasuka, na kila kitu, huko Ujerumani. Nayo Uingereza ina dhoruba kali sana za pepo, zimepeperusha, ninaamini, nyumba sabini elfu, tayari. Mnaona? Vema, tuko kwenye wakati wa mwisho. Yesu ataonekana moja ya siku hizi, nasi tuko kwenye wakati wa mwisho. Kumbukeni tu, huu ni mwanzo tu, yataendelea kutokea zaidi na zaidi. Mnaona? Tuko mwisho.

4 Sasa, kesho, mara baada ya ujumbe leo, tunajiandaa

kuondoka kwenda Arizona tena, kwa hiyo tunaomba kanisa lituombee, tunapoenda. Halafu basi nina maamuzi makubwa ninayopaswa kufanya, enyi marafiki, nami siwezi kuyafanya peke yangu, maana sijui la kufanya. Basi nitaliomba kanisa hili, kama kundi la waaminio wanaokaa hapa pamoja nami, kwamba mtaniombea, kwamba maamuzi yangu yatakuwa ndio mahali pazuri pa kwenda. Yapata miji mia tatu ya nchi za ng'ambo, nafikiri, inaita, na—na—na Uswisi, Ujerumani, na—na Afrika, na kila mahali. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba Mungu atatusaidia tu kufanya jambo lililo sahihi ambapo Yeye anaweza kututumia. Nanyi niombeeni. Nitakuwa nikiwaombea daima, mnajua hilo. Kwa hiyo ninyi niombeeni ya kwamba Bwana Mungu ataniongoza.

5 Sasa, nikirudi kutoka Arizona, Bwana akipenda, na—nataka kuitisha usikivu wenu nasi tutalitangaza kanisani, watatangaza hapa, nami ningetaka kuwa na muda mrefu zaidi kidogo kuzungumza na hili kusanyiko hapa. Ninao Ujumbe, nami ningetaka kuhubiri yapata saa nane ama kitu fulani, mnaona, kwa hiyo namna hiyo. Wakati sisi . . .

6 Mama mmoja alikuwa akizungumza nami, Bibi Wood hapa wa hili kanisa, nilikuwa nikizungumza naye, nami nilikuwa huko Milltown kwenye lile kanisa la Kibaptisti pale ambako tulikuwa tukifanya ibada, halafu basi ninaamini moja ya ibada yao ya kwanza, alisema, "Niliingia saa nne, Ndugu Branham, ulikuwa ukihubiri." Kisha kasema, "Uliendelea kuhubiri hadi saa sita, halafu alasiri yote, ndipo wakawa na wakati mdogo wa dakika kumi na tano, ishirini wa kula chakula cha mchana." Kisha kasema, "Tuliondoka usiku huo saa nne, ulikuwa ungali unahubiri."

Ni—nikasema—kasema, "Vema, unajua sijui mengi sana, ila, wajua, ninapoondoa njiani yale machache nijuayo, na kumwacha Yeye aendelee kuzungumza, mimi . . . Yeye anajua mengi sana." Kwa hiyo, nami ninapenda tu kulisikia, pia, kwa hiyo mimi . . . Lakini nilikuwa tu nikisema hilo kwa njia ya mzunguko.

7 Lakini, tukirudi, Bwana akipenda, ningetaka kuanza mapema na kuendelea tu moja kwa moja kwa ajili ya Ujumbe ambao Bwana anauweka moyoni mwangu. Nami naomba ya kwamba Yeye atanijalia utimilifu wake huko nje jangwani, kwa ajili ya kanisa katika siku za mwisho sasa. Mnaona, mmoja tu wa mienendo ya mwisho ya Roho, ninaamini, umekaribia. Nasi tunaamini ya kwamba Bwana Yesu anajiandaa kuziachilia mbingu pamoja na nguvu za Mungu, hata zitazipasua mbingu, ambalo tunaamini Yeye atalifanya. Nasi tunatumaini ya kwamba Yeye atatupa ujumbe mkamilifu zaidi juu yake wakati tukirudi. Na tuwe na yapata . . . tuanzie kwenye saa tatu asubuhi, na, ama saa tatu na nusu, na kuendelea mpaka yapata saa nane ama tisa, ama wakati wowote nitakapopata wakati wa

kuumalizia, mnaona. Wakati . . .

8 Ndipo nafikiri basi labda niende Afrika kutoka huko, kwa hiyo, Bwana akiendelea kutuongoza hivyo, ama, Uswisi kwanza, kisha Palestina na Afrika, kwenye ile mikutano mikubwa. Kwa hiyo, iweni katika maombi. Lolote mfanyalo, angalieni tu juu leo na muombe, ombeni. Hivyo tu, hilo ndilo tumaini pekee tulilo nalo, ni maombi.

9 Tumepita ninii . . . Natumaini sisikiki wa kukufuru, ama kama mtu—mtu asiyejua yale waliyokuwa wakizungumzia, bali ninaamini taifa letu, kama taifa, tayari halikomboleki. Kuna ninii sana . . . Laiti kungalikuwako na Wakristo wa kutosha ama umoja wa kutosha kulivuta pamoja, bali mivuto mingi imefanywa, wainjilisti wakuu na ibada kuu kila mahali, na hata hivyo lingali linatumbukia katika machafuko. Kwa hiyo na—naamini ya kwamba kama vile tu mataifa yote makuu, mnaona, yote hayana budi kuanguka. Hiyo, mifumo yote hii na kadhalika haina budi kuanguka.

10 Nikiwazia juu ya watu wakiyatoa maisha yao kwa ajili ya demokrasia. Hilo ni—hilo ni jambo zuri sana kwa taifa. Hilo ni jema. Sina neno dhidi ya hilo. Lakini vipi kuhusu maisha yetu kwa ajili ya Kristo? Mnaona? Mtu anaweza kuwa ni shujaa; ainuke, jamaa mdogo katika upeo tu wa maisha, na kichwa chake kipigwe risasi kitoke mabegani mwake, na kuwa shujaa, na labda hata msisikie habari zake isipokuwa iwe ni familia yake mwenyewe nyumbani, ama mtu fulani kwenye ujirani wake ambaye alimfahamu. Lakini hata hivyo tunaogopa kujitokeza na kupiga hiyo hatua itoshelezayo kwa yote kwa ajili ya Kristo, mnaona, ambapo, "Yeye atakayeyaokoa maisha yake atayapoteza; yeye atakayeyaangamiza maisha yake kwa ajili Yangu atayapata, atayaokoa maisha yake." Kwa hiyo hebu—hebu tuweke tu kila kitu tulicho nacho moja kwa moja katika Bwana Yesu na tujitie tu muhuri mbali na mambo ya ulimwengu, na tumtazame Yeye na kuliamini Neno Lake na kuendelea moja kwa moja pamoja na Yeye.

11 Sasa, kabla tu . . . Sasa, leo hii, samahani, mimi . . . Jumapili iliyopita niliwaweka kwa muda mrefu sana kwenye somo hilo la umoja kati ya Mungu na watu Wake. Na sasa leo niliwazia ningewaachilia mwondoke mapema leo, kwa sababu Jumapili iliyopita kulikuwako na wengi wa kuombewa wala sikupata wakati wa kufanyiza mstari wa maombi baada—baada ya sisi kumaliza kuhubiri. Na—nami nafikiri walisambaza baadhi ya kadi Jumapili iliyopita ama kitu fulani kwa ajili ya watu, ama chochote kile, tutawaita ikiwa wako humu jengoni, na, wasipokuwako, tutaomba haidhuru.

12 Sasa, leo ninataka tu kuzungumza juu ya somo fulani ili kwa namna fulani kuijenga imani. Huna budi kufanya hivyo. Kama unajenga yoyote . . . Kama kunao wahudumu

hapa ambao hapana shaka wapo, wanajua kwamba wakati unapowazungumzia watu una mazingira ya kuhubiri kwa ajili ya wokovu, kisha unataka kufanya wito kwa huo. Halafu basi ukitaka mazingira ya uponyaji, u—unapata upako huo wewe mwenyewe, kwa Neno la Mungu, na kuwapelekea watu, na hilo linaliweka kundi lote katika upako kwa ajili ya jambo fulani. Vinginevyo, chini ya matarajio ya vitu fulani. Mnaona, tunatarajia jambo fulani.

13 Nanyi mwajua, ninaamini basi, kulileta hilo juu kidogo zaidi, kwamba Mungu ameliweka Kanisa Lake lote sasa, walioitwa watoke, masalio ya Kanisa Lake, chini ya matarajio ya Kuja Kwake, mnaona. Ninakumbuka pale langoni katika kuja Kwake, hapana budi palikuwa na Ijumaa Kuu ya ajabu sana wakati walipojua Yeye alikuwa akija kwenye karamu, na matarajio. Wengi wao walikuwa wakimtarajia Yeye kuwa kule, wapate kuona namna fulani ya mwujiza ambao Yeye angeufanya. Ama, na wengine walikuwa wakitaka kumwona Yeye. Wengine walitaka kumdhihaki. Na ilikuwa kidogo ni pa—pasaka tofauti na iliyokuwako kwa muda mrefu, wakati Yeye alipoingia mjini. Hebu tuwe tu tukimtarajia Yeye aje kutupeleka Nyumbani, na halafu tutaninii. . .wakati atakapokuja wakati huu.

14 Sasa na tuinamishe vichwa vyetu tunapozungumza na Yeye. Sasa juu ya kusanyiko hili la watu, iwapo kuna haja yoyote hapa ambayo ungetaka ijulikane kwa Mungu, naomba umwinulie tu Yeye mkono wako, na, kama, "Mungu, unirehemu. Na—nahitaji wokovu, nahitaji uponyaji, ninataka kutembea karibu zaidi na Wewe." Mungu awabariki. Ni kote jengoni.

15 Baba yetu wa Mbinguni, tunapokikaribia kiti Chako cha neema, katika Jina la Bwana Yesu, Yule aliyetuletea neema hii ya ajabu, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa mioyo yetu yote kwa ajili Yake Yeye asiyekuwa na dhambi naye akashuka na kutununulia wokovu, sisi tusiostahili, kwamba tukiwa wasiostahili hata hivyo tunaweza kuletwa karibu na Yeye kwa kumwagika kwa Damu Yake, ili Yeye aweze kutuosha kwa maji ya Neno na kutukabidhi kwa Baba Yake kama bikira safi, aliyesafishwa, akatakaswa kwa Damu Yake, na kufanywa akubalike mbele za Mungu, amesafishwa na yuko tayari. Tunapowazia juu ya kuoshwa kwa ile Dhabihu, tukiwazia ya kwamba wakati Yohana alipomwona akiingia majini, yeye alinena na kusema, "Mimi nahitaji kubatizwa na Wewe, basi mbona Wewe waja kwangu?"

16 Kasema, "Kubali, Yohana, iwe hivyo." Loo, ninapenda hilo. Kwa neno lingine, "Yohana, wewe ni nabii, Mimi ni Mungu wako. Sisi ndio viongozi wa siku hii. Ninajua unaelewa, nami pia naelewa. Ila, kumbuka, Yohana, inatupasa sisi, inatupasa kuitimiza haki yote." Yohana, akijua ya kwamba Dhabihu haina

budi kuoshwa kabla haijatolewa, na Yeye alikuwa ndiye hiyo Dhabihu, basi akambatiza, Yeye asiye na dhambi, akiiosha hiyo Dhabihu kabla haijatolewa.

17 Mungu, ioshe mioyo yetu asubuhi ya leo. Tuoshe kwa maji ya Neno, tupate kujitoa wenyewe Kwako. Tusafishe, Bwana, kutokana na kutokuamini kote, tupate kuvutwa karibu na Wewe kama dhabihu iliyo hai, takatifu na inayokubalika kwa Mungu, kwa kuwa hii ndiyo ibada yetu iliyo na maana. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya mambo haya. Tunakushukuru Wewe kwa kila mtu aliyepo. Tukiomba ya kwamba Wewe utalibariki hili Kanisa kuu la ulimwenguni kote la Mungu aliye hai, kote katika mataifa na kote ulimwenguni. Asubuhi ya leo, ambapo wahudumu wamesimama mimbarani, ninaomba ya kwamba utaimwaga Roho Yako, Bwana, katika njia ya kimiujiza juu ya kila mchungaji mwaminifu kwenye jukumu lake, juu ya wainjilisti, juu ya wamishenari. Ee Mungu, ninapowazia habari zao huko nje, baadhi yao bila jozi ya viatu, wamejizungushia suruali ndefu zilizochakaa, wakipitia misituni, kuleta amani na ukombozi kwa wale walio mbali na Kristo.

18 Mungu, tunasema, "Mtume Yesu upesi. Njoo, Bwana Yesu." Na sasa tunayaona maumbile, ishara yenyewe kama ile nyota iliyowaongoza mamajusi hadi Bethlehemu, ikisonga tena. Yesu alisema kungekuwako na mshangao wa wakati, dhiki baina ya mataifa, ishara mbinguni na duniani, bahari ikivuma, dhoruba kuu na kabobo na mitetemeko ya ardhi mahali mahali. Mambo haya ni ninii tu . . . hayo ni mivumo inayopiga king'ora cha mioyo yetu, Bwana, tujue kujitayarisha. Hatujui ni dakika ipi ama saa Yeye atakapotokea.

19 Nasi tunapokuja leo, tunaomba ya kwamba utaibariki siri iliyo nyuma ya kila mkono ulioinuliwa. Mungu, Wewe unajua yote kulihusu. Ninaomba ya kwamba utawaosha, Bwana, na kujitolea kwao na shauku zao, na kuwapa wanayohitaji. Na wakati tukija leo hii, Bwana, ninaomba kama kukiwapo wale hapa wasiokujua Wewe kama Mwokozi, ya kwamba hii itakuwa ndiyo ile siku, siku iliyo kuu sana ya maisha yao, wakati watakaposema "ndiyo" kwa Bwana Yesu. Tujalie, Bwana.

20 Wabariki hao sasa, Baba, tunapojaribu kujiandaa kuwafanya watu wawe na imani, kwa kulisoma Neno Lako. Mungu, litume Neno Lako pamoja na nguvu, kote kwenye hili jengo hapa, na katika nchi ambako hizi kanda zitaenda, na mataifa ya kigeni, popote pale, na jalia wengi waokolewe na waponywe leo kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Tunaomba hayo katika Jina la Mwana Wake mpendwa Mtakatifu, Bwana Yesu Kristo. Amina.

21 Tunaomba ya kwamba Mungu aongeze baraza Zake kuu mno sasa tunapolisoma Neno Lake. Kumbukeni, maneno yangu yatashindwa, ni maneno ya mwanadamu, bali Neno Lake

haliwezi kushindwa. “Mbingu na nchi zitapita bali Neno Langu halitapita.” Hilo ni tumaini la jinsi gani leo hii! Ninajisikia kama kuimba pamoja na Eddie Perronet, “Wote na wazisifu nguvu za Jina la Yesu, malaika na wasujudie; ileteni ile taji ya kifalme, mkamvike taji awe Bwana wa wote. Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama; sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao, sakafu zingine zote.”

22 Sasa, kwa wengi wenu mnaosoma nasi na mngetaka kuliandika hilo fungu, na wakati mwingine mnaorejea kwenye Maandiko ambayo nimeyaandika hapa kwenye muhtasari, tutaanza, tutasoma asubuhi ya leo kutoka Mathayo Mtakatifu 15:21.

> *Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro na Sidoni.*
>
> *Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Bwana, mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo.*
>
> *Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu.*
>
> *Akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.*
>
> *Naye akaja akamsujudia, akisema, Bwana, unisaidie.*
>
> Na *yeye akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.*
>
> *Akasema, Ndiyo, Bwana: lakini hata mbwa hula*. . . *makombo* ambayo yameanguka *kutoka mezani pa bwana zao.*
>
> *Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa: na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.*

23 Sasa, asubuhi ya leo tunataka kuzungumza juu ya imani. Sasa, somo langu asubuhi ya leo ni: *Kung’ang’ania*. *Kung’ang’ania* linamaanisha “ku—kushikilia kwa dhati, kutekeleza lengo.” Sasa, “Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.”

24 Tunao mwili wetu, na kuwako kwetu hapa ni kama mbegu. Nayo mbegu upande wa nje ina ganda; ndani ya hilo ganda mna ganda, ama nyama ya tunda, samahani; na ndani ya hiyo nyama kuna chembe hai. Hivyo ndivyo tulivyo: mwili, nafsi, roho. Sasa, kwa mwili kuna hisi tano: kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Kwa nafsi kuna dhamira, na kadhalika, milango mitano ya kuingia kwake.

25 Mle ndani kuna mmoja, mlango mmoja. Na huo mlango ndipo mahali pale pale ambapo Mungu alipomweka kila mtu tangu Adamu na Hawa, hiari ya mtu. Unachagua kuishi ama unachagua kufa, lolote utakalo. Ni, umewekwa msingi juu ya uhuru wa kujichagulia, na roho yoyote unayoiacha ikutawale itazaa matunda yake, maisha yako yatatawaliwa kutoka ndani. Nayo imani. . .Watu wengi sana wanategemea hisi hizi tano zilizo nje. Ni nzuri, sina neno dhidi yazo, kama zitakubaliana na hisi hii ya sita. Nafsi hii. . .roho hii inaweza tu kuwa ya namna mbili, moja ni Roho ya Mungu, hiyo nyingine ni roho ya ibilisi. Huwezi kuwatumikia mabwana wawili wakati ule ule. Unajitolea kwa mmoja kabisa ama unajitolea kabisa kwa huyo mwingine. Na ikiwa unaye Roho wa Mungu ndani yako, unayo imani, nawe utaamini kila Neno ambalo Mungu aliandika. Na kama hunaye, huenda ukawa. . .

26 Sasa, ibilisi si kama vile watu wengine wanavyodhania, "ni mchoyo na kila kitu," bali ni mdanganyifu. Ibilisi hukufanya ufikirie kwamba uko sawa. Bali unapotofautiana na Neno, hiyo inaonyesha ya kwamba si Roho wa Mungu, maana Roho Mtakatifu aliiandika Biblia. Halafu haina budi kukubaliana na Neno. Basi kumbukeni Jumapili iliyopita, kutokuamini kumoja tu kudogo katika Neno la Mungu. Hawa, Shetani alimwambia kweli, wala hakukana kwamba Neno ni kweli, bali sehemu hiyo moja ndogo ya Neno ilisababisha shida yote hii. Huyo mwanamke alikosa kuliamini Hilo kwa kuwa alikuwa akitafuta sana hekima badala ya kudumu pamoja na Neno. Wakati Mungu anaposema chochote, mbingu na nchi zitapita bali Neno Lake halitapita kamwe. Neno la Mungu halina budi kutimizwa kikamilifu kabisa. Kufikia tu kwenye ile yodi ndogo sana na nukta, Hilo halina budi kutimizwa.

27 Sasa, kung'ang'ania, kushikilia kwa dhati, kujaribu kutimiza lengo, kujitahidi, umeweka nia yako juu ya kitu fulani, na wewe—wewe umeshikilia kwa dhati kwa sababu unaamini ndilo jambo unalotaka, nawe unaamini unaweza kulipata. Sasa, [Ndugu Branham anasafisha koo lake—Mh.] (Samahani.) kushikilia kwa dhati, umeamua niani mwako sasa hilo ndilo utakalofanya. Sasa, huwezi kumwamini Mungu pasipo kujua Neno la Mungu ama kujua jambo fulani kumhusu Mungu.

28 Sasa, mtu fulani alikwambia, "Kama ukienda na kuigusa nguzo ile, utapata afya. Wewe ni mgonjwa." Nisingeamini hilo. Huenda ukaliamini. Lakini hilo kidogo lina nguvu kupita kiasi kwa imani yangu. Si—siamini kuna nguvu zozote katika nguzo hiyo, si zaidi ya ninavyoamini kuna nguvu zozote katika sanamu ama mnara ama msalaba wenye sanamu, ama kitu kama hicho.

29 Ninaamini nguvu zimo katika Kristo, naye Kristo ni Neno. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili

akakaa miongoni mwetu." Sasa, Neno lenyewe linarudi katika mfano wa Roho Mtakatifu, ndani yetu, Nalo ni Neno ndani yako. Mungu ndani yako. Watu wengi sana wanataka kumwelekeza Mungu kwenye kitu fulani cha kisiri huko mbali sana, ama mbali sana wanampita. Mungu yuko ndani yako. Tumaini la Utukufu, Kristo, nia iliyokuwa ndani ya Kristo, ndani yako. Unakipita kwa mbali kabisa, ukijaribu kupata kile umepewa. Mungu, katika mwanadamu! Sote . . .

30 Kristo, hapo alipokuwa duniani, alikuwa ni mwili wa Mungu. Mungu aliumba mwili huu. Ulikuwa ni mwili tofauti, hata hivyo ulikuwa ni mwili wa mwanadamu. Mwajua, Sulemani alimjengea nyumba. Lakini Stefano alisema, "Ila Yeye Aliye Juu hakai katika nyumba zilizojengwa kwa mikono, lakini Wewe umeniwekea mwili tayari." Sasa, Mungu alijiwekea Mwenyewe mwili tayari katika mfano wa Bwana Yesu, ambaye alikuwa ni Kristo, likimaanisha Yule aliyetiwa mafuta. Na, sasa, yote aliyokuwa Mungu, yalikuwa katika Kristo, Yeye alikuwa ni utimilifu wa Mungu katika mwili. Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo. Sasa, na yote aliyokuwa Mungu, Yeye aliyamwaga ndani ya Kristo. Yeye alikuwa Imanueli, Mungu pamoja nasi!

31 Na yote aliyokuwa Kristo, aliyamwaga ndani ya Kanisa. Ni kitu gani? Yeye aliyetiwa mafuta, kuendeleza kazi Yake ili Neno Lake lipate kudumu. Yeye aliishi kwa Neno la Baba. "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Wala Kanisa haliishi kwa mkate tu, bali kwa Neno la Kristo. Ndipo Roho Mtakatifu huingia na kulichukua Neno la Kristo na kulifanya tendo lililo hai siku hizi. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

32 Mnaona, Mungu hawezi kubadilika. Kama Mungu akifanya uamuzi, hauna budi kudumu hivyo. Kama akibadilika, basi Yeye ni mwanadamu kama nilivyo mimi, Yeye—Yeye ni mwanadamu tu anayeweza kufanya kosa. Lakini Yeye hana kikomo! Kwa hiyo, Naye hana kikomo na Yeye—Yeye ni mwenye nguvu zote, wala hawezi kufanya kosa na awe Mungu. Kwa hiyo uamuzi Wake wa kwanza . . . Mwanadamu alipofanya dhambi Yeye—Yeye alimsamehe juu ya msingi wa kuliamini Neno Lake. Mtu wa pili akija, Yeye hana budi kutenda vivyo hivyo la sivyo alitenda vibaya hapo alipotenda mara ya kwanza. Kama mtu aliponywa kwa uponyaji wa Kiungu, kwa imani katika Mungu, Yeye akalipa hilo mtu wa kwanza, kama mtu wa pili akija, Mungu hana budi kutenda vivyo hivyo kama ikiendewa katika hali ile ile. Kama hakufanya hivyo, Yeye ana upendeleo na anaonyesha upendeleo, ambalo hakika lisingemfanya Yeye Mungu. Mnaona?

33 Inakubidi uwe na imani katika yale unayofanya. "Na kama moyo wako hautuhukumu." Kama tunajua Biblia inatufundisha jambo fulani nasi tukose kulifanya, basi kuna jambo fulani tusiloweza kuwa na imani nalo. Unaona, hu—huwezi kujileta

pamoja, kwa sababu unajua kuna mambo fulani huko ambayo Mungu hufundisha, ambayo hutayatii. Na wakati unapofanya hivyo, basi uko wapi? Unaona, hu—huwezi kuwa na imani juu ya kile unachokiendea. Huwezi kupanda hapa juu na kusema, "Mimi—mimi—mimi, jana usiku nilikuwa huko nje nimelewa, na, Bwana, ninataka uniponye asubuhi ya leo. Mimi—mimi, sita—sitakunywa kupita kiasi tena." Inakubidi kujisalimisha, inakubidi kujisalimisha kabisa kwa Mungu. Inakubidi kutii kila sehemu ya Neno. Jitolee kabisa kisha ulichukue Neno. Hilo Neno liko kanisani. Ni Neno lililo hai.

34 Biblia ilisema, "Neno ni mbegu ambayo mpanzi alienda kupanda." Sasa, huwezi kutarajia kupanda vichomanguo na kupata ngano. Ukipanda ngano, utavuna ngano. Ukipanda vichomanguo, utavuna vichomanguo. Kwa hiyo, huna budi kuwa na Neno la Mungu.

35 Na hakuna mwaminio atakayeliweka Neno la Mungu mahali fulani katika siku zilizopita, kamwe hatamfanya Yeye mnyonge fulani ama mwanahistoria—Mungu wa kihistoria. Yeye ni Mungu wa kihistoria, hakika, bali "Yeye ni yule yule," Biblia ilisema, Waebrania 13:8, "yeye yule jana, leo, na hata milele." Kwa hiyo, kadiri tu Yeye alivyokuwa katika historia, ndivyo alivyo siku hizi. Hawezi kupoteza nguvu Zake. Na palipo na udhaifu ni kwamba ulianguka makanisani mwetu, hapo mwanzo, katika kanisa la mwanzoni la kimitume. Basi tulifanya nini? Tulianza kulichukua kanisa hilo na kuvunja ushirika na kuwafanya watu makundi mbalimbali na madhehebu, mpaka tumefikia kwenye machafuko makubwa yasiyo na faida. Rudini kwenye Neno! Mrudieni Mungu! Rudini kwenye Neno lililo hai!

36 Biblia hiyo isipotoa kila kitu inachosema ndivyo ilivyo, katika kila ahadi, mimi sina imani yoyote Kwake. Lakini Neno la kwanza lenyewe lililosema, "Njoni Kwangu nyote msumbukao na wenye kulemewa na mzigo," nilipolijaribu, lilikuwa ni kweli. Basi Hili ni Neno ama si Neno? Kama ni Neno, Hilo halina budi kutoa kila kitu lilichoahidi. Kama silo, basi ni . . . Ni lipi lililo la kweli na ni lipi la uongo? Lote ni Neno la Mungu ama, kwangu mimi, hakuna lolote lililo. Hakuna hata moja ama lote, mojawapo. Kwa hiyo ninaliamini Hilo, kila kanuni, kila mstari, kila kituo, kila koma, kila kistariungio, ninaamini kitu hicho chote kuwa ni Neno la Mungu. Nitaitegemeza nafsi yangu Kwake!

37 Sio kugusa nguzo, kugusa kitu kingine, ama nguzo ya kizimu, ama mwanamume fulani ama mwanamke fulani; ninaamini katika kumgusa Mungu kwa kuliamini Neno Lake, kwa imani. Ndipo unapofanya hivyo, Neno hilo linafanyika ndani yako maisha, Neno lililorutubishwa. Na kila moja ya Neno la Mungu limerutubishwa. Jambo pekee, kwamba ukichukua konzi la ngano na kulishikilia hapa jukwaani, halitafanya kitu

chochote likikaa hapa. Linapaswa kuingia kwenye udongo. Sio tu udongo, bali udongo unaofaa kuisaidia. Kama Neno zuri likianguka kwenye udongo mbaya, litazaa zao baya. Ukichukua punje nzuri na kuziweka katika udongo mzuri, kwenye hali nzuri zitazaa mara mia moja. Vivyo hivyo na Neno la Mungu wakati Hilo linapoletwa ndani ya moyo wa mwanadamu, pamoja na imani, imani isiyokufa katika Bwana Yesu Kristo, pamoja na Roho Mtakatifu na nguvu za Mungu mle kulitia Hilo maji, Hilo litarutubika na kuzaa kila kitu lilichosema lingezaa. Ni Neno. Hilo ni—Hilo ni Neno la Mungu.

38 Yesu alisema, Yohana 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Mbona, hakika! Ninaamini hilo. "Kazi hizi nizifanyazo," tafsiri sahihi ya hilo, "nyingi kuliko hizi mtazifanya." Linasema, "Kubwa kuliko hizi mtazifanya." Usingeweza kufanya kubwa zaidi; Yeye aliyakomesha maumbile, akawafufua wafu, akafanya kila kitu. Lakini, kwa maneno mengine, Mungu alidhihirishwa katika Mtu mmoja, Kristo, sasa amedhihirishwa kote ulimwenguni katika Kanisa Lake. "Nyingi kuliko hizi," kazi zile zile.

39 Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, akiwa kidogo ni mkosoaji, kasema, "'Kazi kubwa zaidi,' Yeye alisema, 'mtazifanya.' Sisi tunafanya kazi kubwa zaidi."

40 Nikasema, "Fanyeni zile ndogo zaidi kabla hamjafanya zile kubwa zaidi. Hebu unionyeshe tu hizo kazi ndogo." Unaweza kulifanya Hilo, kuligeuza Hilo na kujaribu kulifanya Hilo liseme jambo fulani, bali hata hivyo Hilo lingali linabaki vile vile. Basi hebu mwangalie mtu yeyote aliye na imani ya kutosha kuamini hilo, litajidhihirisha Lenyewe vile vile Mungu alivyolifanya. Sasa tunayo mengi sana siku hizi chini ya mihemko na kadhalika, hayo na kadhalika. Sina kitu cha kusema dhidi ya hilo, hilo ni juu ya mtu binafsi na Mungu.

41 Lakini, kwangu mimi, kila neno, kila tendo halina budi kutoka kwenye Biblia hii. Halina budi kuwa ni Neno la Mungu, ndipo ninajua ni kweli. Kama Mungu, Biblia, inaliunga mkono na kusema ni kweli, pamoja na ahadi, basi ni Kweli. Ni mtu ambaye amepata imani, anayesimama pale kwenye Neno hilo na kulifanya Hilo liishi tena. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Tunapoona hilo katika ahadi ya Mungu, basi tunaweza kung'ang'ania. Tunaweza kweli kuamini, tukae hapo kwa sababu ni ahadi ya Mungu. Dumu moja kwa moja nayo haidhuru itachukua muda gani, italileta.

42 Mwajua, Yeye alinena wakati mmoja juu ya mbegu ya haradali, ama imani kama mbegu ya haradali, iliyo ndogo kuliko zote. Mbegu ya haradali ni miongoni mwa mbegu zilizo ndogo sana zilizoko duniani siku hizi. Lakini ni kitu gani? Haitachanganyikana na chochote. Mbegu ya haradali haitachanganyikana na nyingine yoyote. Unaweza kuchukua

sukumawiki na mchicha, na kufanya rapa na kadhalika, na unaweza kuleta vitu mbalimbali kwa kuchanganya mbegu. Lakini haradali haitachanganyika, wananiambia ya kwamba huwezi kuichanganyisha na chochote. Hiyo ni haradali, nayo inabaki haradali.

43 Basi mtu anapolichukua Neno la Mungu, haidhuru hiyo imani ni ndogo vipi, lakini endapo haitachanganyika na kutokuamini kokote, itamleta nje kwenye Nuru. Baadhi yetu tuna imani kubwa ambayo itafanya tu miujiza. Wengine wana imani ya kushikilia tu mpaka litukie. Lakini kama ni imani halisi, mara ukiishika, hakuna kitu kitakachokutikisa kikutoe kwake. Haitachanganyikana. Ndipo mtu huyo ni mng’ang’anizi. Anang’ang’ania. Haijalishi ni watu wangapi wanasema, “Siku za miujiza zimepita,” yeye haamini hilo. Yeye anashikilia kwa sababu ametimiza masharti na kulizamisha Neno hilo katika moyo wa imani unaoliamini Hilo. Hapo anakaa.

44 Ninajua hilo. Nimeona kansa ya sarkoma ikiwatoka watu, na viziwi, bubu, na vipofu, watu wote, kote ulimwenguni, wafu wakifufuliwa, nami ninajua kwamba ni kweli. Kweli! Kutenda kazi katika ono, hakika, ndipo unajua. Ndipo unajua mapenzi ya Mungu ni nini. Huwezi kufanya kazi mpaka uyajue mapenzi ya Mungu. Ahadi katika Biblia inayokwambia jambo fulani, ambalo ni Neno la Mungu. Ndipo Yeye anamtuma Roho Wake kurudi kanisani katika karama, kujidhihirisha Mwenyewe kuondolea mbali tu zile tofauti ndogondogo na kadhalika, kujifanya Mwenyewe halisi miongoni mwetu. Loo, yale, tungewezaje kuomba lolote tofauti, mnaona? wakati Yeye anapokuja kwetu na kujitambulisha Mwenyewe sana, kujibinafsisha Mwenyewe sana, Mungu miongoni mwa watu Wake.

45 “Bado kitambo kidogo na ulimwengu,” ulimwengu, hilo hapo neno la Kiyunani, *kosmos*, ambalo linamaanisha “utaratibu wa ulimwengu.” Utazama. Kila utaratibu wa ulimwengu sharti uzame, kila taifa linalotawaliwa na Shetani. Daima umekuwa na sikuzote utakuwa, nje ya Israeli, wakati wanapofanyika taifa. Shetani alimpeleka Yesu juu ya mlima, kasema, akamwonyesha falme za ulimwengu, zote zilizokuwapo na zitakazokuja, kasema, “Nita—nitakupa Wewe kama utashuka na kunisujudia.”

46 Yeye akasema, “Nenda zako, Shetani.” Alijua atazirithi katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Lakini kila mmoja. . . Nilisimama pale Mafarao wakati mmoja waliutawala ulimwengu, uliojulikana, na ingekubidi kuchimba futi ishirini chini ya ardhi kuzipata falme zao, viti vyao ambapo wakati mmoja walikalia, Makaisari wa Rumi na—na Mafarao wa Misri, mambo haya yote. Nao ulimwengu ukisimama, vivyo hivyo na demokrasia hizi zitasimama. Lakini kuna ninii. . .wote

wanazungumza juu ya nini? Kitu fulani ndani ya moyo wa mwanadamu kinachojaribu kupata umoja huo.

47 Na kama ungeangalia juu tu, umoja hutoka kwa Mungu, nguvu za Mungu. Wakati mwaminio, kiumbe hapa duniani ambacho Mungu amekiumba, kimeunganishwa na Mungu, basi unakuja umoja na kutoa imani. Ndipo mwanadamu anapoliona hilo, yeye anang'ang'ania, hakuna mtu atakayemtikisa.

48 Yesu alisema hapo, "Kazi nizifanyazo Mimi nyinyi nanyi mtazifanya. Bado kitambo kidogo na ulimwengu, *kosmos*, hautaniona Mimi tena." Huo ni utaratibu wa ulimwengu, "Hawataniona Mimi tena."

49 Wafuasi wengi wa kanisa, watu wazuri wakienda kanisani, wakiishi chini ya wazo hilo kwamba wako sawa. Mbona, huko sawa kama mfuasi wa kanisa. Wewe ni mwenyeji. Huenda ukajaribu kufanya mema, lakini, ewe rafiki, hebu nikwambie, huna budi kuzaliwa mara ya pili. Huingii Kanisani, huingii Kanisani kwa kupeana mikono, huingii Kanisani kwa ufuasi wa kanisa. Unaingia Kanisani kwa kuzaliwa.

50 Nimekuwa katika familia ya Branham miaka hamsini na miwili, hawakuniomba nijiunge na familia nipate kufanya jina langu Branham. Nilizaliwa katika familia ya Branham. Mimi ni Branham kwa kuzaliwa.

51 Na hivyo ndivyo ulivyo Mkristo, kwa kuzaliwa, unapozaliwa kwa Roho wa Mungu. Mng'ang'anizi! Naam, hapo ndipo unapoweza kufanikisha jambo fulani. Watu wote kote katika nyakati daima wameweza kufanikisha yale. . .Wao wanang'ang'ania endapo wana—endapo wana imani katika yale wanayojaribu kufanikisha. Inategemea ufanisi wako ni nini. Inategemea yale unayojaribu kufanya, kama unang'ang'ania au la, kwamba una kiasi gani cha imani katika yale unayofanya. Hatuna budi kuwa na imani katika Mungu. Hatuna budi kumwamini Mungu.

52 Ninayo Maandiko mengi yaliyoandikwa hapa ninayotaka kuyarejea. Sasa, kama mtu anajaribu kung'ang'ania, basi yeye—yeye hana budi kuwa na kitu fulani kwanza kitakachompa imani katika yale anayofanya. Sasa tunakumbuka, kwanza kabisa, Biblia inatwambia ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa, kumbukeni jambo hilo. Mungu, wakati Kristo alipokuwa duniani, Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Marko 16, ilisema, "Enendeni ulimwenguni kote." Hotuba ya mwisho ambayo Yesu alilipa kanisa. Sikilizeni.

53 Agizo la kwanza Yeye alilolipa Kanisa Lake, lilikuwa, kwenda mijini kabla Yeye hajaja, Mathayo 10, na "pozeni wagonjwa, watakaseni wenye ukoma, fufueni wafu, toeni pepo, na kama mlivyopata bure, toeni bure." Hilo lilikuwa agizo Lake la kwanza kwa Kanisa.

54 Agizo la mwisho, ama maneno ya mwisho yaliyoanguka kutoka midomoni Mwake wakati alipopaa juu, hata atakapokuja tena pamoja na mwaliko, Sauti ya Malaika Mkuu, Yeye alisema, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka. Asiyeamini atahukumiwa, na...” *Na* ni kiunganishi, kuifunga sentensi yako pamoja. “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya. Wakishika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Biblia ilisema, “Walirudi wakishangilia, Bwana akitenda kazi pamoja nao, akithibitisha Neno kwa ishara zilizofuata.” Mnaona? Walikuwa...Waling’ang’ania katika hilo kwa sababu walikuwa na jambo fulani la kufanikisha. Walikuwa na agizo la moja kwa moja. Agizo hilo lilikuwa liende umbali gani? Ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe. Vizazi vingapi? Kila kizazi, kila kiumbe.

55 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, “Tubuni, kila mmoja wenu. Mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa ajili ya watoto wenu na kwa hao walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Unawezaje kumweka Roho Mtakatifu na nguvu za Kristo huko nyuma kwenye (karibu kitu cha zamani za kale) huko nyuma kabisa kwenye kizazi fulani huko nyuma? Mungu alijua ya kwamba wangesema hilo. Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, “Sitawaacha yatima. Nitamwomba Baba awatumie Mfariji mwingine, Roho Mtakatifu. Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, bali ninyi mtaniona kwa kuwa Mimi...” Na *Mimi* ni kiwakilishi nafsi. “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Amina. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Mungu akiishi ndani ya Kanisa Lake, ndani ya watu Wake.

56 “Dhehebu lipi, Ndugu Branham?” Yeye hatumii mbinu juu ya madhehebu. Mungu hushughulika na watu binafsi. Kila mwanamume, kila mwanamke, mvulana au msichana atakayemwamini Yeye. Haijalishi wao ni wa dhehebu gani, Yeye anatafuta mioyo iliyo na njaa.

57 Sasa, kung’ang’ania, kujaribu kufanikisha jambo fulani. Watu wote kote katika nyakati zote wamekuwa hivyo. Sasa tunachukua, kwa mfano, Nuhu. Nuhu aling’ang’ania sana baada ya kupata mapenzi ya Mungu.

58 Inakubidi kwanza kuyapata mapenzi ya Mungu. Sasa, inakubidi kuyatafuta mapenzi ya Mungu asubuhi ya leo, unapokuja kuombewa, huna budi kuyatafuta mapenzi ya Mungu, kama ni mapenzi ya Mungu kukuponya ama la. Na jambo lingine unalopaswa kufanya, kama unakuja kupata wakovu, unapaswa kutafuta kujua kama ni mapenzi ya Mungu

kukuokoa au la. Jambo la kwanza unalopaswa kutafuta kujua, kwamba mapenzi ya Mungu ni nini. Halafu basi, kama kweli umeipokea ile mbegu moyoni mwako, basi unaweza kung'ang'ania. Hakuna kitu kitakachokusogeza. Haijalishi yale mtu wa hekima anayojaribu kusema, "Sivyo ilivyo, wala si *hivi*, na *vile* na *vinginevyo*," halikusogezi hata yodi moja, kwa kuwa unajua yaliyo mapenzi ya Mungu. Yeye aliyanena moyoni mwako, imani yako imekaa pale na itashikilia moja kwa moja haidhuru kama hakuna zaidi ya kama chembe moja ya mbegu ya haradali. Itakuleta moja kwa moja ma—mahali hapo. Mapenzi ya Mungu. Naam.

59 Nuhu, baada ya kuisikia Sauti ya Mungu ikimwambia ya kwamba mafuriko yalikuja, yatakuja, samahani, ambayo yatauangamiza ulimwengu, maumbile yatakatiliwa mbali. Hivi Yesu hakusema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu"? Maumbile yangevurugika, nasi tunaliona siku hizi.

60 Ninataka kusimama hapa kwa dakika moja. Nilipokuwa nikiingia Bombay, ambako tulikuwa . . . Bwana alitupatia umati ulio mkubwa kuliko wote tuliopata kuwa nao, laki tano kwenye wakati mmoja, kuhubiria. Kulikuwako na kipande kwenye gazeti nililokuwa nikisoma, kasema, "Ninii, vema, tetemeko la nchi hapana shaka limekwisha." Kasema, "Siku chache kabla ya hilo tetemeko kuja, wote . . . " Huko India wao ni maskini, fukara sana. Wanajenga nyua zao kwa mawe, na kadhalika. Nao maskini ndege waliruka kutoka kwenye hayo mawe kutoka kwenye viota vyao wakaenda makondeni wakakaa mitini. Ng'ombe waliosimama karibu na kuta na minara, walienda makondeni kwenye jua kali, wasingesimama kwenye vivuli. Walisimama kwenye jua huko nje. Hawakujua kitu hiki cha ajabu kilikuwa ni nini. Kisha, mara, tetemeko la nchi likazitikisa hizo kuta zikaanguka, minara ikaanguka. Kama maskini hao ndege wadogo wangalikuwa huko, wangaliuawa. Kama ng'ombe walikuwa wamesimama chini ya hizo, wangaliuawa.

61 Hivi hamwoni Mungu yeye yule aliyewaonya wale ndege na wale wanyama katika siku za Nuhu? Basi kwa nini mnataka kuliita jakamoyo, ama chochote mnachotaka kusema, jinsi Mungu alivyowashughulikia ndege hawa? Yeye aliwapa silika kuruka kutoka kwenye ukuta huo na kukiondokea kitu hicho kabla hakijapiga. Mnafikiri Mungu huwazia vya kutosha juu ya shorewanda kumwondosha kutoka ukutani, ni zaidi sana jinsi gani ninyi mlivyo zaidi ya shorewanda? Yeye anajua jinsi ya kuwashughulikia walio Wake.

62 Dada anayelala hapa kwenye kitanda hiki cha wagonjwa, machela, kama Yeye alimlisha shorewanda na kulivalisha konde nyasi, ni zaidi sana vipi Yeye anavyokuwazia! Wewe u zaidi sana vipi kuliko shorewanda? Mwamini Mungu bila kujali hisia

ama chochote kingine. Ni Neno la Mungu. Lichukue Hilo na kulishikilia. Kweli! Pia ung’ang’anie, liamini Hilo, lishikilie Neno Lake.

63 Ndipo baada ya tetemeko la nchi kwisha, wale ndege wadogo wakarudi, wakarudi mahali pao na kufanya mawe yao wapate kushikilia, ama mahali humo kwenye mawe tena, na kujenga kiota chao; ng’ombe.

64 Mungu yeye yule aliyekuwa katika siku za Nuhu. Nuhu! Vema, mnafikiri sayansi ingalimwambia...Walikuwa na sayansi kubwa kuliko waliyo nayo sasa. Wangeweza kufanikisha mambo makubwa kuliko wanayoweza sasa. Wa—walikuwa na rangi inayovifanya vitu kuonekana vikamilifu hata wa leo. Walikuwa na dawa ya kufanya miili isioze ambapo wangefanya mumiani. Tusingeweza kufanya hivyo siku hizi, ninaambiwa. Halafu kwa kitu kingine, walijenga piramidi. Ni nani angaliweza kujenga piramidi siku hizi? Hayo majabali makubwa kule yaliyosimama hapo na kuangalia kule juu na kuona ile sfiniksi, na, mbona, ingehitaji mabehewa mengi kuuweka mguu wake mmoja mle. Waliyanyanyua majabali hayo huko juu namna gani? Walifanyia wapi? Nguvu za petroli hazitaweza. Hakuna kitu tulicho nacho, isipokuwa ingekuwa ni nguvu za atomiki, na hicho huenda kikawa ndicho kitu kile kile kilichosababisha yale maangamizi yaliyotangulia gharika yaliyopotosha ulimwengu huo na kuurusha mbali na jua, kuurudisha nyuma na kusababisha mvua.

65 Kama Mungu alisema kutakuwako na mvua, kulikuwa kunaenda kuwako na mvua bila kujali kama kuliwahi kuwa nayo ama la. Haijalishi ni mathibitisho mangapi ya kisayansi yaliyokuwako kwa Nuhu, Nuhu aliisikia Sauti ya Mungu, kasema, “Itanyesha.” Wala hapakuwa kumewahi kuwapo na mvua juu ya nchi. Mnaona?

66 Kama vile alivyompeleka Ibrahimu juu ya mlima, na hapo akamwambia amtoe dhabihu mwanawe. Basi wakati Ibrahimu alipomwandaa Isaka, naye mtoto Isaka akauliza swali. Vema mfano wa Mungu na Mwana Wake. Akaifunga mikono yake nyuma yake. Akasema, “Huu hapa moto, na hizi hapa kuni, na kadhalika, haya hapa mawe, haya hapa madhabahu, bali iko wapi sadaka?”

67 Basi baba huyo mzee, sasa yapata umri wa miaka mia moja na kumi ni minne, akiwa na mwana aliyekuwa amemngojea kwa muda wa miaka ishirini na mitano, kupitia kwa shida na kadhalika, na jinsi ambavyo alikuwa amelishikilia hilo Neno la Mungu lisiloweza kufa, lililokuwa limepandwa moyoni mwake, yeye alikuwa atampata huyo mtoto kwa vyovyote vile. Alikuwa ni kitu gani? Mng’ang’anizi. Akasema, “Nimemshikilia umbali huu. Ninajua ya kwamba kama Mungu alinipa huyo kwa

kumwamini Yeye, Yeye atamfufua kutoka kwa wafu." Haya basi. Kung'ang'ania, kulishikilia Neno hilo la Mungu kwanza.

68 Na, hilo, wakati alipokuwa tayari kuutoa uhai wake, kulikuwa na Malaika aliyeshika mkono wake na kukizuia kile kisu. Pia palikuwapo na kondoo dume aliyeshikwa kwa pembe zake, huko nyikani nyuma yake. Huyo kondoo dume alitoka wapi? Alikuwa umbali wa safari ya siku tatu, na mtu yeyote siku hizo angeliweza kutembea kwa urahisi maili ishirini na tano. Mimi hutembea maili ishirini na tano na thelathini kila wakati ninapoenda kuwinda ama kufanya doria, ama chochote kile, ninazitembea kwa urahisi. Nasi tuna ile inayoitwa miguu ya petroli. Mtu huyo alitembea kutoka kwenye safari ya siku tatu, kisha akaangalia huko mbali na kuuona ule mlima. Mbona, wanyama pori wangalimwua huyo kondoo dume. Na jambo lingine, alikuwa juu ya mlima ambako hakukuwako na maji wala chochote kile. Si ajabu alipaita mahali hapo *Yehova-yire*, "Bwana atajipatia Mwenyewe dhabihu."

69 "Anawezaje kuyafanya mambo haya, Ndugu Branham, katika siku za sayansi, katika siku za ulimwengu mkuu wa sayansi? Anawezaje kuyatenda mambo haya? Unafikiri atawezaje kuyaepuka?" Yeye angali ni Yehova-yire, Bwana. Tunalidumisha Neno Lake na Yeye anaweza kutenda yale aliyosema. Amina. Yeye anaweza kuchukua kanisa baridi lililokufa, la kawaida, anaweza kumchukua mfuasi kutoka kwa kanisa hilo na kuuweka Uzima wa Mungu ndani ya jamaa huyo, na kumwasha moto kwa Injili. Anaweza kumchukua kahaba kutoka mtaani, Yeye anaweza kumchukua mlevi kutoka kichochoroni huko nje, na kufanya mwanamume na mama wa heshima kutoka kwao, kwa sababu Yeye ni Yehova-yire, "Bwana atajipatia Mwenyewe dhabihu." Amina.

70 Jinsi tunavyomweka Mungu katika misingi yetu! Tunawazia katika misingi yetu. Tunaamini katika misingi yetu. Achilieni kitu hicho. Hilo ndilo lililomwingiza Hawa katika tatizo, yeye alikuwa akiwazia katika misingi yake mwenyewe. Wazia katika misingi ya Mungu, yale Neno Lake lisemayo. Jiinue mwenyewe juu ya hayo, kwa imani, ukiliamini Neno Lake.

71 Nuhu alisema, "Sijali ni kiasi gani sayansi inaweza kuthibitisha hakuna maji huko juu, Mungu anaweza kuweka maji huko juu. Yeye atafanya hivyo kwa sababu Yeye aliliahidi. Kama aliliahidi, Yeye atalifanya."

72 Na yeye—yeye, yeye alifanya nini? Hakuwa ati azunguke tu na kusema, "Vema, Yeye aliniambia hilo. Naam, na—naamini itakuwa." Alifanya jambo fulani kulihusu. Loo, ndugu, dada, unaona ninalomaanisha? Yeye hakuketi tu pale na kusema, "Mungu alisema hivyo," alifanya jambo fulani kulihusu. Kama unataka kuokolewa asubuhi ya leo, Mungu aliahidi wokovu. Basi fanya jambo fulani kulihusu, usiketi tu hapo. Usijiunge

na kanisa moja na kuhamisha barua yako kutoka kanisa hadi kanisa. Yeye aliahidi wokovu, ukombozi.

73 Kama wewe ni mgonjwa, “Kwa nini uketi hapa?” Kama vile yule mwenye ukoma alivyosema siku ile wakati ule mji ulipozingirwa, “Mbona tuketi hapa mpaka tufe?” Wakati Samaria ilipozingirwa na Waashuri, wao walisema, “Tukiketi hapa hata tufe, tuta—tutakuwa hapa sikuzote. Tutafia papa hapa. Tukienda mjini, wanakufa huko kutokana na njaa. Hima twendeni kwenye kambi ya adui.” Loo, jamani, ni ninii duni jinsi gani. . .Ni imani ndogo jinsi gani wangaliweza kuwa nayo. Ni kitu kidogo jinsi gani. . .Wanaenda kwenye kambi ya adui aliyekuwa akijaribu kuwaua. Lakini kasema, “Kama tukifa, tutakufa haidhuru. Kwa hiyo tukijiokoa. . .maisha yetu yakiokolewa, mbona, tutafanya vema.” Nao wakashuka kwenda kule chini, naye Mungu akaiheshimu chembe hiyo ndogo ya imani ovyoovyo. Na hakuwakomboa tu, bali aliwakomboa Israeli.

74 Kile tunachohitaji siku hizi ni wanaume na wanawake ambao watamchukua Mungu kwa Neno Lake na kung’ang’ania Nalo. Mungu atafanya matetemeko ya ardhi na matetemeko yashuke kambini kwanza. Mungu atashughulikia kama kutakuwa na mvua huko juu ama la.

75 Wasema, “Vema, Ndugu Branham, daktari aliniambia ya kwamba nilikuwa ninakufa. Nina kansa.” Huenda hilo likawa ni kweli. Huyo mtu anakwambia yote ajuayo. Lakini, jambo pekee analoweza kufanya, yeye yuna hisi tano za kufanyia kazi, mbili za hizo anaweza kuzitumia. Ni kitu gani? Hisi moja ni ya kugusa, mahali hapo pengine ni—ni kuona. Kuona na kugusa, anaweza kugusa kitu fulani, ama kuona kitu fulani kwa eksi-rei. Hizo tu ndizo mtu huyo alizo nazo za kutumia. Hayo tu ndiyo ajuayo, bali anafanya vizuri awezavyo. Bali usiangalie hayo, yeye amefikia mwisho wake. Angalia hapa juu yale Hili liliyoahidi! Useme, “Inaweza kutendwaje?” Mungu alisema hivyo. Hilo linatosha hapo Mungu alipolisema. Hilo linatosha, liko imara Milele daima Mbinguni, Neno Lake liko imara. Nayo Maneno Yake yalifanyika mwili, Nayo ni mwili leo hii ndani yako, kama utaliacha Hilo lifanyike mwili. “Mkikaa ndani Yangu nayo Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi ombeni mtakayo nayo yatafanywa,” Yohana Mtakatifu 15. Mnaona, tunataka tu kuyaacha Maneno hayo yakae humu ndani. Liaminini, ni la kweli. Ni mbegu, nayo ita—itatimiza kila kitu Yeye alichoahidi.

76 Sasa, angalieni, wa sayansi wangalikuja pale, kundi la wanasayansi, na kusema, “Bw. Nuhu, wewe ni mhudumu mzuri. Tu—tunakuthamini. Unalo kusanyiko zuri hapa, familia yako, lakini, na hata hivyo, kama ukininii. . .hatukubaliani nawe, nasi tunajua ya kwamba wewe ni—wewe ni tofauti. Una—unasababisha tu ushupavu kupandwa miongoni mwa watu, na

hata unawaogopesha baadhi ya watu, ukiwaambia ya kwamba ulimwengu unafikia mwisho wake. Tunataka kukuonyesha na kukuthibitishia kisayansi."

77 Loo, ibilisi huyo kamwe hakufa. Yeye—yeye angali anajaribu kufanya hivyo. Yule yule aliyesema, "Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, hebu nione mwujiza. Fanya mwujiza na uugeuze mkate huu, huu. Una njaa, yafanye mawe haya kuwa mkate, nitakuamini Wewe." Ibilisi yule yule ndani ya hao makuhani wenye elimu, alisema, "Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka msalabani na ututhibitishie." Mnaona? Ibilisi huyo haninii, kamwe yeye hafi. Mnaona, ibilisi daima humchukua mtu wake bali roho yake hubaki hapa kwa ajili ya mwingine. Lakini hebu niwaambie jambo la kutia moyo: Mungu humchukua mtu Wake bali Roho Wake hukaa hapa kwa ajili ya mwingine, pia. Naam. Mtu fulani atalipokea Neno hilo. Mtu fulani atatiwa mafuta njia moja ama nyingine. Inategemea kile wewe, ni roho gani iliyo ndani ya punje hii. Huyo ndiye, utaliamini Hilo ama hutaliamini Hilo. Hiyo ni kusema, vema, wewe si . . .

78 Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, mhudumu. Ungeshangaa. Nami nilikuwa kwenye ofisi ya daktari wakati aliposema hilo. Nami nawaambia ukweli, nilipata madaktari wengi walioamini katika uponyaji wa Kiungu kuliko nilivyopata wahudumu. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Nimekuwa chini ya . . . Nilihojiwa, mwajua, kule, kwa sababu ya gazeti la *Look*, ama sio *Look*, bali . . . Ni lipi lile gazeti lililoandika ule "Mwujiza wa Donny . . . ?" *Reader's Digest*. Naam. Ndipo wakati waliponihoji pale kwenye Mayo Brothers, mnajua yale waliyosema? "Hatudai kuwa waponyaji, tunadai tu kuyasaidia maumbile. Kunaye Mponyaji mmoja tu, huyo ni Mungu." Loo, jamani! Haya basi. Ni mtu anayeweza kuwazia. Mtu fulani anayeweza kuangalia huko ng'ambo na kuangalia hicho kitu chote. Sisi ni wanadamu. Tunapasiwa mauti, makosa na kila kitu. Yeye ni Mungu, asiye na kikomo.

79 Hatuna budi kuliamini. Kama ningaliweza kulielezea, basi si imani tena. Siwezi kuelezea ni kwa nini ng'ombe mweusi anaweza kula nyasi za kijanikibichi na kutoa maziwa meupe, bali anayatoa. Hiyo ni kweli. Wala wewe huwezi kulielezea. La, bwana. Siwezi kuelezea jinsi Mungu anavyofanya mambo haya, bali Yeye alisema tu angeyafanya. Kamwe sitaweza kujua, hutaweza kujua, bali tunaamini. Kwa imani unaokolewa. Kwa imani unaponywa. Kila kitu kinachokuja, pia, kutoka kwa Mungu, hakina budi kuja kwa imani.

80 Wakati fulani uliopita, akisimama kwenye matangazo, jamaa fulani alikuwa akiudhihaki mkutano, hakujua nilikuwa ni nani. Akasema, "Siamini Hilo." Kasema, "Jambo hilo halingewezekana. Kamwe siwezi kuliamini Hilo namna hiyo." Akasema, "Sina budi . . . Halina budi kuthibitishwa kisayansi

kwangu.”

81 Nikasema, “Basi kamwe usingeweza kuwa Mkristo. Huwezi kamwe.”

Akasema, “Loo, mimi ni Mkristo.”

82 Nikasema, “Huwezi kuwa. Huwezi.” Nikasema, “Kisayansi nithibitishie mahali Kristo alipo.” Nikasema, “Je, wewe ni mwanamume uliyeoa?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Je, unampenda mke wako?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Kisayansi nithibitishie upendo ni kitu gani.” Yeye, akasema . . .

“Vema,” akasema, “Nisingeweza kufanya hilo.”

83 Nikasema, “Basi huna chochote ninachoita upendo. Mnaona? Sasa, unaninii tu . . . wewe, huko ni kujisingizia imani niani mwako. Unaona? Ikiwa huwezi kulithibitisha kisayansi. Niambie nini . . . Shuka hapa chini ukaninunulie upendo wa thamani ya robo moja. Uninunulie imani ya thamani ya peni moja. Huwezi kufanya hivyo.”

84 Nayo silaha yote ya Mungu ni imani, upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, upole, utu wema, saburi. Silaha yote ya mwaminio ni imani. Tunamwamini Mungu kwa imani, kwa sababu, Mungu alisema hivyo. Basi ni nini? Ibrahimu alihesabiwa haki, na Paulo, kwa imani; lakini, na Yakobo, kwa matendo. Ibrahimu alikuwa akizungumzia yale Mungu aliyoona, naye Yakobo alikuwa akizungumzia yale mwanadamu aliyoona. “Nionyeshe imani yako kwa matendo yako,” “pasipo matendo yako,” na kadhalika. Mnaona? Basi ikiwa huna matendo kwa imani yako, inaonyesha huna imani, unazungumza tu kutoka kinywani mwako. Lakini kama kweli unayo imani, unaliamini na kutenda jinsi hiyo. Hiyo ni kweli, iweke katika matendo!

85 Nuhu alifanya hivyo, aliitia katika matendo. Aliendelea moja kwa moja kuijenga safina. Haidhuru sayansi yoyote ilisema nini, “Sasa, angalia hapa, tutakuthibitishia kisayansi hakuna mvua huko juu.”

86 “Sijali mnaweza kunithibitishia kiasi gani, ni kiasi gani mnaweza kusema hayo kwa utafiti wa kisayansi, ama vyovyote mnavyotaka kuliita, Mungu aliniambia ‘Mvua inakuja,’ nami ninamwamini Mungu.” Jambo ndilo hilo. “Itanyesha.”

87 “Inatoka wapi? Bw. Nuhu, ningetaka kukuuliza, bwana, kasisi, mvua hiyo inatoka wapi? Iko wapi?”

88 “Vema, Mungu anaweza kuiweka kule juu kama Yeye aliniambia itakuwako.” Kweli!

89 Na leo hii wanasema hili haliwezi kufanywa. Wanaona upambanuzi mkutanoni. Wanasema, "Haina budi kuwa ni telepathia." Telepathia, ati telepathia? Kupambanua roho, kuhusu maono ya Bwana! Manabii walikuwa na telepathia ya jinsi gani? Yesu alikuwa na nini wakati Yeye aliposimama pale siku ile?

90 Naye huyu hapa Filipo akaja, naye akaokoka kisha akaenda kule na kumpata Nathanaeli, akamleta mbele za Yesu, naye Nathanaeli akasema, "Ah, sasa kusingekuwako na jambo jema kutoka—kutoka Nazareti."

91 Kwa hiyo wakati alipokuja mahali Yesu alipokuwa, Yesu alimwangalia na kusema, "Wewe ni—wewe ni Mwisraeli. Huna hila."

92 Naye akasema, "Rabi, ulinijua lini Wewe? Ulipataje kunitambua Wewe?"

93 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti nilikuona."

94 Sasa, kimwili, hiyo ilikuwa. . .Kama ulipata kuwa kule, ni maili kumi na tano kuuzunguka huo mlima. Mahali hapo pawili, safari ya siku nzima kuuzunguka huo mlima. Angewezaje kumwona? Ndipo nini? Akiwa ni mtu wa imani, akiwa ni mtu aliyetaka kuliona Neno la Mungu likithibitishwa, alitaka kujua kwamba Mungu alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea, Masihi atakapokuja atakuwa ni Nabii," kama tu yeye alivyokuwa. Naye akaona hilo, na akajua. Akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu." Hiyo ni kweli. Jina lake halipatikani na mauti.

95 Lakini pale walisimama wale makuhani mashuhuri baridi waliokuwa na DD., Ph.D., LL.D za kutosha nyuma yao, labda, waliopitia kwenye mstari wa wahudumu waliosimama pale, walidhani walilijua Neno. Walilijua, neno, bali kunayo mengi hawaninii. . .Sio kulijua Neno Lake, bali kumjua Yeye, kumjua Yeye aliye katika hilo Neno. Hiyo ni kweli. Kumjua Yeye, Uzima ulioko kwenye Neno. Sasa, walisimama pale na kusema, "Mtu huyu ni Beelizebuli. Yeye ni mpiga ramli. Yeye huyaona mambo hayo. Yeye ni—Yeye ni mpiga ramli. Hiyo ni. . . "

96 Yesu aligeuka akasema, akijua. Sasa ngojeni, kamwe hawakusema hilo kwa sauti kubwa, waliwazia hilo moyoni mwao. Naye alijua mawazo yao. Hivi Biblia inasema hivyo? Luka Mtakatifu. Naam, Yeye alijua mawazo yao. Mnaona, wao walidhani alikuwa akisoma akili yao. Alijua mawazo yao. Akasema, "Mkisema neno dhidi Yangu, nitawasamehe. Lakini," kwa maneno mengine, "siku moja Roho Mtakatifu atakuja kufanya jambo lili hili, nanyi mkisema neno moja dhidi yake, mkiongea dhidi ya huyo, hamtasamehewa katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao." Mnaona?

97 Mnaona, Roho Mtakatifu, wasingeweza kulielewa Hilo. Iliwabidi kulijibu kusanyiko lao, maana kusanyiko lao lilikuwa limesimama hapo. Nao wakasema, "Vema, Yeye—Yeye hapana shaka anasoma akili zao. Ana telepathia. Yeye ni Beelizebuli, mpiga ramli." Na mtu yeyote anajua ya kwamba mpiga ramli ni wa ibilisi. Nao wakaiita kazi ya Mungu "ibilisi," wakiziita kazi za Mungu.

98 Hivi hamjui ya kwamba chochote alicho nacho ibilisi ni kitu kilichopotoshwa kutoka kwa kilicho halisi? Uongo ni nini? Ni ukweli uliopotoshwa. Uzinzi ni nini? Ni tendo la haki lililopotoshwa. Dhambi yote ni—ni kweli na haki iliyopotoshwa. Mauti ni kitu gani? Uzima uliopotoshwa. Hakika, ndivyo ilivyo katika Neno Lake. Hivyo ndivyo ilivyo, nao watu wanajaribu tu kuliwekea uvuli, kulitia uvuli, kulifanya liseme mambo kwa sababu hawajui, hawajui. Hawana imani kulichukua Neno. Lakini Nathanaeli alikuwa nayo.

99 Vipi kuhusu Simoni wakati alipokuja kule juu? Alimsikia yule baba yake mzee Mfarisayo, akisema, "Simoni, mwanangu, kabla wakati wa mwisho kuja, labda kutakuwako... Nimemtazamia Yeye kuja katika siku zangu, bali hakuja. Huenda akaja katika wakati wako. Na kama akija, Simoni, haya hapa yatakayotukia: Kila kitu kitakuwa kikiendelea, mwanangu, na kutakuwako na kila namna ya mambo ya uongo yatakayoibuka kila mahali. Lakini wewe kumbuka hili, dumu na Neno. Unaona? Sasa, Masihi huyu akitokea, Yeye atakuwa ni Nabii. Naye Masihi huyu atakuwa ni Nabii kama tu Musa alivyokuwa, maana Neno letu la Mungu linasema Yeye atakuwa ni Nabii kama yeye. Sasa, wewe utajua Yeye atakuwa ni zaidi ya Nabii, Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii. Lakini matendo Yake na maneno yatakuwa ni Nabii, maana usingeweza kupanda juu zaidi ya hapo mpaka umfikie Mungu. Unaona?" Kwa hiyo yeye akasema "Yeye atakuwa, Yeye atakuwa Mungu-Nabii. Kazi zake hapa duniani zitaonyesha Nabii, kwa hiyo tunajua kwamba ni, itakuwa ni Mungu. Kumbuka hilo."

100 Nami nadhani wakati Andrea alipokuja akamwambia usiku huo, "Loo, tulimwona Masihi," ninawazia Simoni alisema, "Nenda zako, nenda. Toka. Ah, endelea, usinisumbue."

101 Lakini kesho yake wakati alipohudhuria mkutano, akaenda Mbele za Bwana Yesu, na Yeye akasema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Hilo liliondoa ukakamavu kutoka kwake. Alifanya nini? Yeye, Yesu... Yule mvua samaki asiye na maarifa ambaye hata asingeweza kuliandika jina lake mwenyewe, Biblia ilisema alikuwa asiye na elimu wala maarifa. Bali ilimpendeza Mungu, kwa imani hiyo, kumfanya Petro, jiwe dogo, kumpa funguo za Ufalme, "Juu ya Mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu." Kitu gani, juu ya mwamba kama Katoliki isemavyo? La. Juu ya nini, ni kitu gani? Juu ya ufunuo

wa kiroho. Mnaona, "Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia. Juu ya mwamba huu, juu ya Neno lililoandikwa la Mungu kufunuliwa kiroho, nitalijenga Kanisa Langu, wala malango ya kuzimu hayawezi kulishinda." Kwa nini? Ni zaidi ya mbegu ya haradali. Ni nguvu za Mungu zikifanya kazi miongoni mwa wanadamu juu ya Neno, Neno likifanywa hai.

102 Hilo ndilo lililokuwamo ndani ya Nuhu. Yeye alisema. . . Neno ni Uzima ndani yake. "Nami nitajiandaa kwa ajili yake."

103 "Vema, haikunyesha jana. Ulisema itanyesha. Itanyesha lini?"

"Sijui, bali itanyesha."

"Unajuaje itanyesha?"

"Mungu alisema hivyo."

104 Kama walivyomwambia Ibrahimu, mbona, umri wa miaka themanini, yeye; naye mke wake, umri wa miaka tisini. Maskini mke mkongwe pale, alikuwa akibeba baadhi ya pini na kadhalika kwa ajili ya vibuti vidogo kwa ajili ya mtoto mchanga, kwa miaka ishirini na mitano; huyu hapa mwenye umri wa miaka tisini, ameshika maskini fimbo ya kutembelea, namna *hii*, akienda huku na huku. Ibrahimu, mwenye kibyongo, na masharubu yakining'nia chini. "Vipi kuhusu hilo, Ibrahimu? Hei, ulitoka—ulitoka kwenye mji wa Uri muda mrefu uliopita. Ulisema utampata mtoto mchanga. Vipi kuhusu hilo sasa?"

"Utukufu kwa Mungu, tutampata haidhuru!"

"Kwa nini?"

"Mungu alisema hivyo!"

"Mbona, hiyo imekuwa ni miaka ishirini na mitano iliyopita."

105 "Mungu alisema hivyo! Haileti tofauti yoyote kama ni miaka mia moja na ishirini na mitano, Yeye atafanya hivyo haidhuru!" Mnaona? Kushikilia, kung'ang'ania, kufuata, kufuatilia. Umeishika!

Kama yule mvulana mdogo akiipeperusha tiara. Kasema, "Iko wapi?"

106 Akasema, "Sijui, bali iko huko nje mahali fulani, ninaweza kuihisi mwishoni mwa hii kamba."

107 Jambo ndilo hilo. Mwanamume ama mwanamke anayelichukua Neno la Mungu, umeshika kitu fulani. Nanga yako inashikilia ndani ya pazia. Dhoruba na tufani huenda zikasukuma na kutikisa kwa kila njia, bali wewe umetiwa nanga. Inakuja moja kwa moja mahali pale. Unang'ang'ania. Utaliamini.

108 Nuhu aliliamini Hilo, hakika, naye akalifanikisha kusudi la Mungu kwa ajili ya maisha yake. Hivi unataka kufanikisha kusudi la Mungu maishani mwako? Basi ng'ang'ania wakati ukininii. . . ng'ang'ania unapolipata Neno. Lishikilie Hilo, ahadi, ni yako.

109 Musa. Ni watu wangapi ningaliwaendea sasa! Ninasema hapa Musa, huko katika Kutoka, Musa, yeye alikuwa ni mwanachuoni, mwanadiplomasia, mwanajeshi. Sio tu mwanajeshi, yeye alikuwa ni jenerali. Yeye si jenerali tu, bali alikuwa halifa wa Farao. Amina. Ninajisikia kubarikiwa sasa hivi, kwa hiyo samahani. Naam, halifa wa Farao. Kama alitaka kuwakomboa watu wake, vema, alikuwa ameishika Misri mkononi mwake. Alikuwa halifa wa Farao, angefanya alichotaka atakapokuwa Farao. Bali Mungu alisema naye, uhu-huuh, siku moja huko katika kichaka kilichowaka moto.

110 Loo, alitoroka kama mwoga, pamoja na elimu yake yote. Theolojia yake yote, yeye alishindwa. Mambo yake yote makuu, yeye alishindwa. Lakini siku moja, katika kichaka kilichowaka moto, Mungu alikutana naye. Wakati Mungu alipomjia katika kichaka hiki kilichowaka moto, mwangalieni, akiwa na fimbo mkononi mwake, mke wake juu ya nyumbu, huku mtoto Gershomu ameketi pajani mwake, akiwa njiani kwenda Misri. Yeye alikuwa nini? Akishuka kwenda kuiteka. Alikuwa, alikuwa aking'ang'ania, alikuwa ameshikilia sana.

111 "Musa, unafikiri wewe, kwenye umri wa miaka themanini, ukiwa na fimbo iliyopinda mkononi mwako, kavu iwezavyo kuwa?" Hum! Fimbo iliyopinda, uvamizi wa mtu mmoja, akishuka kwenda Misri kama vile mtu mmoja kwenda Urusi kuiteka. Tunahitaji tu. . . Mungu anahitaji tu mtu mmoja. Huyo tu, Yeye anahitaji mtu mmoja tu aliye mkononi Mwake kabisa. Mtu mmoja, huyo tu ndiye anayemhitaji. Anaweza kuitikisa Urusi vipandevipande akiwa na mtu huyo mmoja.

112 Yeye alimchukua Nuhu, ama Musa, samahani. Alimchukua Musa wakati alipokuwa akitorokea *huku*, ametulia katika maisha mazuri, msichana mdogo wa kupendeza, amemwoa, alikuwa na mtoto mchanga, akiwa ni mrithi wa kondoo za baba mkwe wake, Yethro, kuhani wa Midiani. Kila kitu kilikuwa shwari kwake. Alikuwa na makazi mazuri, mahali, maisha ya raha huko nje, na kuwinda mara moja moja kwa uta wake, labda, na kumwua kulungu, na forsadi nyingi sana na kondoo wengi sana, na sufu na biashara, misafara iliyopitia humo. Mbona, alikuwa amewasili, hakuwa na chochote cha kuhofia. Lakini siku moja, siku moja mzigo wa hao watu, watu wake waliolemewa na mizigo ulikuwa tayari umeondoka niani mwake. Walikuwa huko chini Misri. Alikuwa ameshindwa, kwa hiyo Mungu anaweza kufanya jambo jingine kulihusu. Lakini siku moja wakati Mungu alipokutana naye katika kichaka

kilichowaka moto, nena kuhusu kung'ang'ania, huyu hapa anaenda!

"Kwani jeshi lako liko wapi?"

113 "Sihitaji jeshi lolote. Jeshi langu ni jeshi lisiloonekana." Kama ilivyokuwa huko Dothani asubuhi moja, wakati nabii . . . "Jeshi langu ni jeshi lisiloonekana." Huyu hapa anaenda, kitu pekee unachoweza kuona ni maskini fimbo iliyopindika, akimwongoza nyumbu huyu nyuma, nayo masharubu yakipeperuka. "Mungu asifiwe!" Macho yake yameelekezwa Mbinguni, akishuka kwenda kuiteka.

114 Wakati mwingine imani hukufanya kutenda kimzaha, kwa mwenye akili ya kimwili. Bali kama ni Neno la Mungu, halina budi kutimia. Ng'ang'ania, mwone Mungu akilitimiza.

115 Akashuka huko, alikuwa ameshikilia kwa dhati. Akaenda mbele za Farao, ilionekana kana kwamba atashindwa. Akasema, "Nitawaonyesha kama nimetumwa na Mungu ama la." Akaitupa ile fimbo chini sakafuni namna *hiyo*, kana kwamba kusema . . . nayo ikageuka kuwa nyoka; yeye na Aaroni. Naye akawaita tu wanajimu wawili, ama watu wawili waliopagawa na ibilisi kama tulio nao katika siku za mwisho, wakiwaiga walio Wateule, kama yamkini. Hiyo ni kweli. Wakashuka, wakatupa fimbo zao chini, zikawa kitu kile kile. Sasa, Musa alijua jambo hili moja, ya kwamba Mungu aliyemtuma aliweza kumshughulikia. Sasa, yeye hakujua atende nini tena.

116 Unafikia mahali hujui la kufanya, nao watu wanasema, "Kamwe hakuponywa. Mbona, kitu hicho kingali pale." Kama Mungu aliliweka hilo moyoni mwako, wewe simama imara. Endelea tu kushuhudia kwa utukufu wa Mungu. Endelea!

117 Musa alisema, "Ninajua Mungu alinituma." Ni jambo gani lililotukia? Yule nyoka akapulizia mara tatu ama nne, mkubwa, labda chatu ama kitu fulani, akainuka na kuwameza hao wengine. Hivi uliwahi kuwazia kilichozipata hizo fimbo zingine? Waliokota moja tu. Yeye aliwala hao wengine. Hawakuwako tena. Na hivyo ndivyo Mungu atakavyofanya moja ya siku hizi kwa nguvu Zake. Naam.

118 Musa alikuwa aking'ang'ania. Halafu, muda si muda mwajua, Yeye akamtuma huko nje, na kusema, "Fanya hivi, Farao." Ndipo akasema, "Usipofanya hivyo, tutafanya *hivi-na-vile*." Ndipo akamlilia Mungu, Naye akawatuma nzi, viroboto, kila kitu kingine juu ya nchi. Yeye alikuwa nini? Alidhamiria. Mungu alimwambia, "Walete hao watoto kwenye mlima huu, huku nyuma." Alijua alikuwa na mapenzi ya Mungu, alijua alikuwa na ono mbele zake. Alijua ya kwamba mbingu na nchi zingepita, bali ono hilo lisingeweza kushindwa. Kwa hiyo akashuka akaenda huko chini, mng'ang'anizi.

119 Sikilizeni, ndugu, kama unaweza kuja asubuhi ya leo pamoja na ono la mapenzi ya Mungu, kama unaweza kuja pamoja na Neno la Mungu, sijali kinachotukia, "Nitang'ang'ania. Nime . . . moyoni mwangu, tangu nimekuwa nikiketi hapa, ninalo ono la Mungu. Ninang'ang'ania. Nitakuwa—nitang'ang'ania. Ninashuka niende, ninaenda kuiteka. Kitu hiki hakina budi kuniacha." Kitakuacha, ndugu. Usijali, kitakuacha.

120 Daudi, akisimama pale juu mbele ya Goliathi, mbona, aling'ang'ania. Akasema, "Mnataka kuniambia kwamba mtasimama na kuiacha hiyo sayansi mamboleo, wanasayansi huko nje?" Sasa linasikika la kukufuru, bali natumaini mnajua ninalomaanisha. Mnataka kuniambia ya kwamba hao wanasayansi mamboleo wanaweza kusimama pale na kusema siku za miujiza zimepita, wakati Neno la Mungu aliye hai linalikanusha? Mnataka kuniambia ya kwamba mtaiacha sayansi ya kisasa iseme hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, nayo Biblia, asilimia sitini na kitu ya huduma ya Yesu ilikuwa ninii ya Kiungu . . . naam, asilimia themanini na sita, nafikiri, ilikuwa ni uponyaji wa Kiungu? Nayo ahadi, na zile ahadi za mwisho!

121 Mnataka kuniambia, ndugu zangu wahudumu, ya kwamba mtasimama na kuyaacha haya mashirika ya kisasa yanayojiita makundi ya kidhehebu yanayoelekea kwenye Shirikisho la Makanisa hapa, ama Baraza la Makanisa, na mnataka kuniambia mtasimama kwenye shirika hilo na kuwaacha waligubike Neno la Mungu ndani yenu, na kuwaambia siku za miujiza zimepita? Ninyi ni nani hata hivyo? Mmepata kuwa na ujuzi wowote? Mlipata kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu? Wewe, kama umefanya hivyo, ndugu, hakika utalichukua Neno la Mungu kwa ajili yake. Acha kila kitu kingine kiwe ni uongo. Bila shaka!

122 Angalieni, Daudi alikuwa na ujuzi. Alichukua kombeo dogo. Hakuwa na mengi sana. Lilikuwa ni kombeo, bali alijua ya kwamba Mungu wa Mbinguni alikuwa pamoja naye. Naye akatoka akaenda huko nje na kumwua dubu na simba, naye alijua kile hilo lingefanya. Ndipo akasema, "Mnataka kuniambia, kama Mungu anaweza kumweka huyo dubu na simba mikononi mwangu, ni zaidi sana vipi anavyoweza kumweka maskini Mfilisti huyo asiyetahiriwa, anayejivuna huko nje?"

123 Ulimwengu huu wa siku hizi unaojivuna, ukisema siku za miujiza zimepita, nayo Urusi ikiinuka hapa juu, ikiyakanyaga makanisa chini na kuyaaibisha. Hakuna kitu ndani yao cha kufanyia kazi. Ni kwa nini maskini Castro kule chini, maskini jamaa huyo aliyepagawa na pepo . . . Sasa, ni—ninamjua, nilimpa mikono na kukutana naye, na kadhalika, nilipokuwa kule. Naye alinizungumzia vizuri, na kila kitu namna hiyo; kasema aliamini

kulikuwa na Utawala wa Miaka Elfu unaokuja na Kristo, na kadhalika, bali yeye alijiuza kabisa kwa ibilisi. Lakini yeye alifanya nini? Alifanya mambo fulani mazuri. Kweli alifanya jambo moja, alighushi fedha zote kisha akaanzisha fedha zingine tena. Hilo ndilo litakalotukia hapa moja ya siku hizi, ambako hivi vikeneko vikubwa vichoyo vya wiski, na makampuni ya tumbaku ambayo yanaweza kuchukua kodi zao za mapato na kuziweka kwenye televisheni huku nje. Ninajua ninazungumza kwenye kanda. Lakini hebu niwaambie, hiyo ni kweli, hata hivyo. Hizo ni fedha zinazopaswa kwenda kwa serikali. Lakini wanaweza kukwepa. Lakini hebu wewe uanze, ukose kulipa yako wakati mmoja uone kitakachotukia. Watakuvua nguo kwa ajili yake.

124 Mnataka kuniambia ya kwamba kundi hilo la Wafilisti wasiotahiriwa linaweza kusimama hapa nje na kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai? Tunategemeza kitu kama hicho. Kile kanisa linachohitaji siku hizi ni kumrudia Mungu, kulirudia Neno Lake, kuzirudia zile Nguvu, kurudi kwenye pentekoste; sio kwenye dhehebu la Kipentekoste, kurudi kwenye ule ujuzi wa pentekoste. Hao jamaa wametatanishwa kabisa wanapozungumza juu ya dhehebu la Kipentekoste. Pentekoste ni tukio, linamjia Mmethodisti, Mbaptisti, Wapresbiteri, ama yeyote anayelitaka. Hiyo ni kweli. Mungu hashughuliki na taifa, na watu, na dhehebu, Yeye hushughulika na mtu binafsi. Sikuzote, pamoja na Mataifa, akiwachukua watu kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake. Mnaona? Hivyo ndivyo anavyowashughulikia. Sasa, upesi, sina budi kuharakisha.

125 Daudi alisema, "Mnataka kuniambia mtaacha hilo litukie?" Akasema, "Kombeo hili dogo!" Akamwandama yule simba. Ati nini? Akamwua. Kisha akamwandama yule dubu na kumwua. Akasema, "Ni zaidi sana vipi Mungu atanipa yule Mfilisti anayejivuna huko nje anayesema siku za miujiza zimepita?"

126 Akamcheka na kusema, "Nitakunyanyua kwa ncha ya sindano hii ya mfumaji, mkuki, nikuning'inizie juu, niwaache ndege waile nyama yako." Yeye angeweza kufanya hilo.

127 Sauli akamwambia, kasema, "Mtu huyo ni . . . mbona, vidole vyake vina urefu wa inchi kumi na nne." Akasema, "Mbona, mtu huyo ni shujaa tangu ujana wake, nawe si kitu ila maskini mvulana mdogo mwekundu."

128 "Loo, bali," akasema, "Ninalo jambo fulani la kukwambia. Nina kitu fulani usichokijua."

129 "Mbona, wewe si kitu," ndugu yake akasema, "rudi nyumbani. Wewe ni mtukutu. Nitamwuliza baba akupe kichapo utakaporudi."

130 Yeye alisema nini? Alisema, "Nilikuwa nikichunga. Mtumishi wako, baba yangu, nilikuwa nikiwachunga kondoo wake huko nje siku moja. Ninamtumaini Bwana Mungu. Naye

simba akaja na kumchukua mmoja wa hao wana-kondoo, nami nikamwandama." Kwa nini? Alipewa agizo, akiongozwa na baba yake. "Ndipo nikamwangusha chini. Na alipoinuka, nikamwua, maana niliachiwa agizo."

131 Loo, ndugu mhudumu, tumeachiwa agizo. Simba anaingia na kumchukua mmoja wa watumishi Wake na kumtoa nje, ninakuja na kombeo asubuhi ya leo. Kombeo la maombi ya imani yatamwokoa huyo mgonjwa, naye Mungu atamwinua. Kile Yeye alichosema! Tunakuja kumtafuta, kumrudisha mwana-kondoo huyo zizini. Tunawahitaji, kila Mkristo, tunamhitaji kila mmoja wenu. Tunawahitaji, hatuna budi kuwa pamoja nanyi. Baba ametupa agizo, hima twende tukamtafute. Hebu tulidumishe agizo.

132 Akasema, "Basi kama Yeye angaliweza kufanya hivyo kwa kondoo huyo, ni zaidi sana vipi kusimama hapa na kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai! Ninamwonea aibu ndugu yangu na hao wengine wote," akasema, ni kama kusema hivyo. "Ninawaonea aibu, udhaifu wenu."

133 Nami ninalionea aibu kundi langu la wahudumu siku moja ninapowasikia wakisimama na kupatana, kuchukua upande mmoja na wasioamini katika kusema, "Loo, hakuna kitu kama hicho. Hakuna. Hu—hu—hutarajii mambo hayo yatukie."

134 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa watoto wa watoto wenu, kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Ikiwa Yeye angali anaita, Yeye angali anammwaga Roho Mtakatifu. Kama Roho Mtakatifu angali anaishi ndani yako, Huyo hana budi kuishi maisha yale yale aliyoishi katika Kristo Yesu.

135 Ukiona tawi likichipuka, nalo linazaa tofaa, vema, linalofuata halitakuwa ni pea na hilo lingine zambarau. Kama ndivyo lilivyo, limepandikizwa. Hiyo ni kweli. Bali kama shina asili la huo mti likizaa tawi lingine, litakuwa ni tofaa. Kwa hiyo, siku hizi, tunayo mashirika mengi na madhehebu ambayo yamepandikizwa. Hiyo miti itaishi. Naam, bwana.

136 Niliona mti hivi majuzi wenye matunda tisa mbalimbali ya aina ya mchungwa juu yake, nao ulikuwa na komamanga, pia ulikuwa, ninaamini ilikuwa ni balungi, limau na yote juu yake, bali kweli ulikuwa ni mchungwa. Ndipo nikamwambia huyo mtu, Bw. Sharrit, rafiki yangu, nikasema, "Vema, vipi hivyo, nao ni mchungwa?"

137 Akasema, "Vema, unaupasua tu huu mti na kuchomelea hii iliyopandikizwa mle."

138 Nikasema, "Vema, litakapozaa tunda, litazaa chungwa?"

Akasema, "La, linazaa kwa jinsi yake."

139 Haya basi! Ndugu, ninapowaambia, wakati makanisa yamepandikizwa ndani ya Kristo, hivyo, ama kujaribu, inavyodhaniwa, yakapasuliwa tu mle ndani kwa jina, yakijiita makanisa ya Kristo, yanapofanya hivyo, yanaleta nini? Matunda ya kimadhehebu. Ila tawi hilo likiwahi kuzaa tawi lingine, litakuwa kama lile la kwanza lilivyokuwa. Lakini hebu nikwambie, ndugu, kama Roho Mtakatifu ni halisi Kanisani leo hii, namna ya Kanisa Huyo alililokuwa nalo lililoandika Kitabu cha Matendo nyuma Yake, iwapo Kanisa la Mungu aliye hai, Kanisa la Yesu Kristo likifanyika hai tena kwa Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste, Hilo litaandika Kitabu cha Matendo nyuma Yake. Kweli. Litashikilia kwa dhati, litang'ang'ania mpaka kitu hicho kitimie. Ee Mungu, uturehemu. Naam, bwana. Naam, bwana.

140 Samsoni, Samsoni, alikuwa mvumilivu sana mradi tu angeweza kuhisi vishungi saba vimemzunguka. Yeye alijua hiyo ilikuwa ni ahadi ambayo Mungu alimpa. Na kila mwanamume na mwanamke angeweza kushikilia kwa dhati tu kama Samsoni alivyofanya, mradi tu unaweza kuhisi nguvu hizo za ahadi zimekuzunguka, za Mungu. Hili hapa Neno, Neno lilisema hivyo. Nawe unaweza kuwa mng'ang'anizi mradi tu unajua ya kwamba unayo ahadi hiyo moyoni mwako, imani hiyo iliyokwambia, wakati ukiketi hapa sasa, imani hiyo inasema, "Nimeponywa. Nimeponywa." Unaona? Ukijisikia hivyo, endelea tu kusonga mbele. Ndugu, Mungu atawashughulikia hao Wafilisti, usiwe na hofu.

141 Uliwahi kuwazia jinsi Samsoni, akiwa na maskini mfupa huo wa taya la nyumbu . . . Unajua jinsi hizo helmeti zilivyokuwa nene? Baadhi yazo yapata inchi moja, ama inchi moja na nusu ya shaba tupu. Ungechukua upanga wenye mikono miwili na kumpiga nao kichwani, usingemdhuru. Naye Samsoni akaokota maskini mfupa uliooza wa taya, samahani, maskini mfupa huo mkavu wa taya la nyumbu, akauokota na kupiga na kuwaangusha elfu moja wao. Mbona, pigo la kwanza juu ya moja ya vichwa hivyo, mfupa huo wa taya ungalipasuka vipande milioni moja. Lakini, mnaona, huo mwujiza ulikuwa katika huo mfupa wa taya kadiri ulivyokuwa katika Samsoni. Yeye alijisikia, "Kama ninaweza kuihisi ahadi hiyo pale," akasema, "waache waje." Na, ndugu, akaanza kuwapiga Wafilisti kulia na kushoto. Kwa nini? Alikuwa ameshikilia kwa dhati mpaka Mfilisti wa mwisho akawa amelala chini. Amina! Yeye alikuwa na kitu gani? Sio vingi sana. Alikuwa na taya la nyumbu kupigana dhidi ya panga na mikuki na watu waliofunzwa. Ila alikuwa na nguvu za Mungu juu yake. Mnaona, nguvu za Mungu zilikuja juu yake, kwanza.

142 Loo, ndugu, piga vita mpaka kila dalili imekwisha. Haleluya! Piga vita mpaka kila—kila shaka limeondoka.

143 Wasema, "Vema, kisa changu ni tofauti." Chukua mfupa huo wa taya na kukiponda kitoke hapo.

144 Huyu alisema, "Lakini, unajua, mimi ni tofauti tu kidogo, ninazeeka kupita kiasi." Uponde utoke. Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja. Endelea.

145 "Vema, lakini kisa changu ni kibaya sana." Yona alikuwa katika tumbo la nyangumi, mikono imefungwa nyuma yake, amelala huko chini katika matapiko ya nyangumi. Kila mahali alipoangalia palikuwa ni tumbo la nyangumi. Alikuwa na dalili chungu nzima, bali aligeuka na kusema, "Mara nyingine tena nitaangalia kwenye hekalu Lako takatifu, Bwana." Huwezi kumficha Yeye. Jambo ndilo hilo, kushikilia kwa dhati! Kung'ang'ania, dumu moja kwa moja na Neno la Mungu. Kwa nini Yona akakaa namna hiyo? Kwa sababu alijua ya kwamba wakati Sulemani alipoliweka wakfu lile hekalu, yeye aliomba na kusema, "Bwana, kama watu Wako wakiwa katika shida mahali popote na waangalie mahali hapa patakatifu, basi sikia kutoka Mbinguni, yajibu maombi yao." Naye alijua jambo hili moja, ya kwamba Mungu angesikia maombi hayo.

146 Basi kama Yona, chini ya hali hizo, angeweza kuwa na imani kiasi hicho katika Mungu, na wewe je? Hakuna mmoja wenu hapa aliye vibaya hivyo chini ya hali za mambo. Sasa ni zaidi sana jinsi gani! Kuangalia kwenye hekalu ambapo mtu hatimaye alirudi nyuma, Sauli, aliyeomba hayo maombi, bali ilikuwa ni kuwekwa wakfu na Mungu wakati Roho Mtakatifu alipolishuhudia kwa Nguzo ya Moto iliyoingia na kushuka chini hapo nyuma? Nguzo ile ile ya Moto ambayo mnayo picha yake pamoja nanyi leo hii, ikitenda kazi miongoni mwetu, ikifanya ishara zile zile na maajabu. Kuna shida gani? Sikilizeni kwa utulivu. Sikilizeni. Sisi tungewezaje, wakati tukiangalia sio kwenye hekalu la duniani, ama shirika fulani ama dhehebu fulani, bali kwenye mkono wa kuume wa Mungu, ambapo Yesu ameketi akiwa na mavazi Yake Mwenyewe yaliyolowa damu, amina, Damu Yake Mwenyewe mbele ya Baba, kufanya maombezi juu ya maungamo yako! Amina. Waebrania 3, ilisema ya kwamba Yeye—Yeye ni Kuhani Mkuu, yu hai milele ili kufanya maombezi, loo, jamani, mbele za Baba asubuhi ya leo. Kuhani Mkuu! Kama Yona angeweza kuangalia nje, akatae kuona tumbo la nyangumi, ni zaidi sana vipi tunavyoweza kukosa kuona maumivu kidogo na uchungu kidogo, ama kitu chochote kidogo tulicho nacho! "Ninaangalia kwenye ahadi Yako takatifu, Bwana." Huwezi kumficha mtakatifu kutoka kwenye maombi yake, ni hayo tu. Hakika, loo, yeye alikuwa hivyo.

147 Sina budi kuharakisha, enyi marafiki, nitachelewa kupita kiasi tena. Hebu mengine machache, fungu dogo hapa.

148 Yohana, alikuwa na hakika sana, maana Mungu

alimwambia. Mwajua, sasa baba yake alikuwa ni kuhani, mwajua, lakini, ajabu, hakushuka kwenda kuwa kuhani, alienda nyikani. Hakutaka kuchanganyikana na nadharia ya mwanadamu. Alienda nyikani apate kujua, kwenye umri wa miaka tisa. Baba yake na mama wakiwa ni wakongwe, walijua kamwe hawatamwona mwana wao nabii akiingia mamlakani kwenye siku hizo.

149 Pia, kumbukeni, Roho yuyo huyo ameahidiwa kwetu katika siku hii ya mwisho, Eliya.

150 Kumbukeni, Yesu kamwe hakurejea kwenye hilo wakati aliposema . . . Yeye alinena habari za Yohana Mbatizaji. Kama mkiangalia, "Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu," Mathayo 3. Maana, huninii, mna kuhitilafiana katika Maandiko.

151 Yeye alisema, "Kabla siku hii haijaja, siku ile iliyo kuu na ya kuogofya ya Bwana itakapokuja kuiteketeza dunia kwa moto." Dunia haikuteketezwa kwa moto huko nyuma katika siku hizo. Ulimwengu utateketezwa kwa moto baada ya kuja *huku*. Yeye angemtuma Eliya kuyanyosha mambo na kuwarudisha watu kwenye upatanisho. Na yale Eliya huyu, wa kwanza aliyekuja, angerudisha, angeileta imani ya baba iwaelekee watoto wao, lakini huyu katika siku za mwisho angewarudisha kwenye Imani ya baba. Mnaona? Mnaona, kurejea kwenye wale baba wa pentekoste ya asili, Ujumbe wa kweli, hapo mwanzo. Eliya! "Mungu, mtume," ndilo ombi langu. "Mtume, Ee Bwana, mtume upesi." Tutamwombea, kwamba atajitokeza jukwaani. Naye Mungu sikuzote anaye mwakilishi Wake mahali fulani duniani. Kamwe hajawahi kuwa bila ya shahidi mahali fulani, sikuzote yuna shahidi akisimama mkweli. Nami ninaamini yeye ni . . . Ninaamini kwamba tumekaribia kule Kuja kwa Bwana sasa hivi. Wakati umewadia kwa nguvu za Mungu kuinuka tena katika mfano wa nabii Eliya, na kutumwa hapa chini na kuwanyosha watu, na kuwaleta, kundi hilo dogo. Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa, katika uchache tu, Kanisa litakuwa hivyo.

152 Vema, tunaona Yohana hakwenda kupata mafunzo yake ya kikanisa, bali alienda nyikani kupata ujuzi. Wakati aliporudi, alinena ya nyikani. "Uzao wa nyoka," nyoka aliowapata nyikani. "Shoka limewekwa penye shina la mti." Mahubiri yake yaliwekwa msingi juu ya vitu kama hivyo. Lakini, tazameni, walipokaribia, yeye alisema, "Kuna Mtu anayesimama miongoni mwenu sasa msiyemjua." Yeye alijua alichokuwa akinena habari zake.

"Wewe ndiye Masihi?"

Akasema, "La."

153 "Wewe ni Nabii yule, yule Masihi-Nabii aliyekuwa ainuke?"

“Mimi siye,” akasema, “bali Yeye amesimama miongoni mwenu sasa.”

154 Labda huenda ikawa Kayafa, kuhani mkuu, alikuwa pale. Ambaye, nadhani hakuwapo, alikuwa na cheo kikubwa kupita kiasi kushuka kwenda mahali kama hapo. Lakini yeye, mmoja wa hao makuhani huenda alisema, “Bwana, huyu hapa Ndugu Jones. Yeye ni jamaa mzuri. Ndugu *Fulani-wa-fulani* hapa, Ndugu John Doe, yeye, ni—ninaamini yeye, Bwana anamfanya Masihi.”

155 Yohana akasema, “Nitamjua. Kutakuwako na ishara itakayomfuata.” Alijua ni kitu gani. Heri walio wa kiroho wanaofahamu. Heri wale walio na macho na wanaweza kuona, masikio yanayoweza kusikia. Kasema, “Nitamjua. Mungu atamtambulisha, atamtambulisha Yeye.” Mungu huwatambulisha watumishi Wake. Naam, bwana. Na baada ya kitambo kidogo Yeye akaja, akaangalia pale juu na kuona, akasema, “Tazama Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu.” Yeye alishikilia kwa dhati kwamba hakuna Ph.D., LL., L maradufu, yeyote yule, atakayeingia, kuhani fulani, mtu fulani anayependwa sana wa majira hayo akiwa na namna fulani ya madoido. Alikuwa . . . Mtu huyo alishuka pale na kujua kwamba Yeye alikuwa ni Nani kwa kuwa kulikuwako na ishara iliyomfuata. Alijua Huyo alikuwa ni Nani.

156 “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Kanisa la Mungu likiinuliwa na kuwekwa mamlakani. Naam. Sasa, chini mpaka nimalize hili somo sasa. Yohana, akishikilia kwa dhati. Naye aling’ang’ania kwa kuwa alijua kwamba angemtambua Masihi huyo, kwa sababu huyo Masihi alikuwa awe na ishara. Nasi tunaona ishara leo hii, ishara za Masihi ajaye, zikisukumia ndani. Basi sikilizeni kwa utulivu sasa.

157 Wakati mwanamke huyu Myunani, aliposikia habari za Yesu, “Imani chanzo chake ni kusikia.” Sasa, yeye alikuwa ni Myunani, kafiri, kwa hiyo alisikia na akaja. Mwajua nini? Imani hupata chanzo ambacho wengine hawakioni. Imani hupata chanzo ambacho wengine hawawezi kukiona.

158 Unasema, “Loo, kuna nini huko juu? Kuna nini hapa chini? Kuna nini huko? Ni nini maskini ile . . . Loo, ni misheni ndogo. Ni *ninii*. Kama Mungu alikuwa akienda kufanya lolote, Yeye angekuja kwenye ukasisi wa Katoliki ya Kirumi, Yeye angemjia askofu mkuu wa kanisa la Kimethodisti, angewajia ma—ma—mapadre wa Kianglikana, ama baadhi yao. Angewajia . . .” Naam, hivyo ndivyo walivyowazia hapo mwanzo. Lakini Yeye alizaliwa wapi? Katika hori. Aliwapata wanafunzi Wake wapi? Kutoka mtoni, wavuvi, wenye hadhi ya chini, hawana elimu. Mnaona, Mungu hufanya atakalo, lakini mnamfahamu.

159 Ilikuwa tofauti namna gani hapa, ya Moabu huku juu, wakati Israeli walipokuwa wakipita? Moabu walitoa mafahali

saba, kile hasa Israeli walichokuwa nacho. Moabu walitoa dhabihu saba, kondoo dume, kama tu vile Israeli. Kimsingi, walikuwa ni sawa kabisa. Nao kwa kweli walikuwa ni ndugu, Moabu alitoka kwa binti ya Lutu. Naye hapa alikuwako Balaki huko juu akitoa dhabihu ile ile, akafanya kimsingi tu alivyoweza kuwa. Lakini ni kitu gani kilicholeta tofauti? Mmoja wao alikuwa na Mwamba uliopigwa, Nguzo ya Moto, sauti ya Mfalme kambini, kundi la wasiojali madhehebu. Hawakuwa na makazi, hapana mahali pa kuita makwao. Walikuwa wakielea, wasafiri na wageni, wahamaji, wakikiri kwamba walikuwa ni wasafiri na wageni. Walikuwa wakiutafuta mji.

160 Hivyo ndivyo ilivyo leo hii. Si uhusiano na dhehebu fulani kubwa. Ambalo ni sawa, lakini, hilo, sijali wewe ni mfuasi wa shirika kiasi gani, kuwa mfuasi popote utakapo. Lakini, jambo la kwanza, liweke jina lako kwenye Kitabu Kule, acha Mungu aliandike katika Damu ya Yesu Kristo, umpokee Roho Mtakatifu, pamoja na imani ya kuamini kila Neno Yeye aliloandika, kwamba Hilo ni kweli. Haya basi. Naam.

161 Sasa, mwanamke huyu alikuwa ni Myunani, kwanza kabisa, lakini imani hupata chanzo ambacho wengine hawajui chochote kukihusu.

162 Sasa, kumbukeni, Neno Lake—Lake ni Upanga. Biblia ilisema hivyo. Ni Upanga. Waebrania, wa 4, 4:12, mkitaka kuliandika. Waebrania 4:12, ilisema Yeye ni, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili." Hebu nisimame hapa kwa dakika moja tu. Sikilizeni. "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, huchoma hata kuugawanya mfupa, na kadhalika, yale mafuta, na ni Mtambuzi wa mawazo ya moyoni." Hiyo ni kweli? Hilo—hilo, hebu tusimame tu kwa dakika moja, wazieni sasa, "Mtambuzi wa mawazo ya moyoni." Hivi Maandiko husema uongo? Hayawezi. Kama yakijipinga Yenyewe, hayafai hata karatasi yaliyoandikiwa, ni madanganyifu. Kama ahadi za Mungu zikihitilafiana zenyewe, u—utaamini nini?

163 Ni kama yule mvulana wa Kihindi aliyekuja hivi majuzi kwa Daktari Morris Reidhead na hao wengine, rais wa Misheni ya Sudani, naye akasimama pale na kusema, "Kumbuka," kasema, "tunajua kwamba Yesu yu hai," akasema, Daktari Reidhead kasema—kasema, "maana Yeye anaishi moyoni mwangu. Hiyo ni kweli."

164 Akasema, "Naam, naye Mohammed anaishi moyoni mwangu, pia." Kasema, "Tunaweza kutoa saikolojia nyingi katika Uislamu kadiri Ukristo unavyoweza." Lakini kasema, "Vema, ninataka kuona alama hizo za ishara, ishara za Marko 16 zikitimizwa."

165 Akasema, "Loo, hizo," kasema, "wewe—wewe unaninii tu. . . " Kasema, "Unaona, bwana, kutoka mlango wa 9. . .

kifungu cha 9 cha mlango wa 16 wa Marko, havijavuviwa kama hivyo vingine. Hivyo vimewekwa tu humo ndani na Vatikani."

166 Akasema, "Basi labda hivyo vingine havijavuviwa. Kwa hiyo mnasoma Kitabu cha namna gani?" Kasema, "Kurani nzima imevuviwa." Ni aibu jinsi gani! Ni fedheha jinsi gani kwa kanisa la Kikristo! Hilo ama ni Neno la Mungu au si Neno la Mungu. Na kama ukiweka tu imani katika Hilo, hebu lione likitenda kazi. Liamini Hilo, likubali. Naam, bwana. Tunaliamini Hilo.

167 Ati nini? Mpambanuzi wa mawazo ya moyoni. Sasa angalieni, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu," Yohana Mtakatifu 1, "naye Neno akafanyika mwili, Kristo." Ndipo wakati Yeye alipokuja hapa, aliwaangalia hao watu. Maskini mwanamke mmoja aliligusa vazi Lake, Yeye akageuka, kasema, "Ni nani aliyenigusa?" Petro akamkemea. Akaangalia kote na kusema, "Ni nani aliyenigusa?"

Kasema, "Kila mtu anakugusa."

168 Akaangalia kote na kusema, "Lakini naona nimekuwa mnyonge." Akaangalia huko nje. "Kutokwa kwako na damu kumekoma." Ati nini? Neno la Mungu likiyatambua mawazo.

169 Hao Mafarisayo wanasema, moyoni mwao, walisema, "Yeye ni Beelizebuli. Mnaona, Yeye, hivyo ndivyo Yeye alivyo. Hiyo ni kweli hasa."

170 Akageuka na kusema, "Nitawasamehe hilo." Yesu akiliangalia kusanyiko na kutambua wazo lao. Ilikuwa ni kitu gani? Neno, Neno lililofanyika mwili, mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo. Hivyo ndivyo Neno la Mungu lilivyo sasa. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaona?

171 Huna budi kulitia Neno lililo hai ndani yako upate kuwa na Mungu aliye hai ndani yako, kwa sababu Neno hapa ni Mungu wakati Hilo limefanyika mwili ndani yako, limefanyika Roho, Uzima ndani yako. Wakati Hilo linapoingia ndani ya mwili wako na imani yako, na likawa Uzima, basi wewe ni mfano ulio hai. Wewe ni waraka wa Mungu, unaosomwa na watu wote. Hutakuwa na Yeye kama Kristo, sio katika utimilifu, kwa maana Huyo aligawanyika katika Siku ya Pentekoste.

172 Sasa, ninyi watu mnaoamini kwamba inawabidi kunena kwa lugha ili kuwa na Roho Mtakatifu, ninawatakeni msikilize hili kwa dakika moja tu. Wakati Roho Mtakatifu aliposhuka, kwenye Siku ya Pentekoste, Yeye alikuwa ni ndimi za moto. Hiyo ilikuwa ni ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, ilikuwa imejiwaganya na ilikuwa juu ya kila mmoja wao, Mungu katika Kanisa Lake. Naam, bwana, Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Hapo ndipo walipompokea Roho Mtakatifu, wakati waliponena kwa lugha. Haikuwa ni lugha isiyojulikana, walikuwa wakinena na watu huko nje waliowaelewa. Injili haina budi kuenezwa wakati huo. Walitoka wakaingia kwenye

kusanyiko, kisha wakaingia barazani na kuanza kunena kwa lugha, sio zisizojulikana. Ninyi hufanya kinyume cha mambo mnapowazia inawabidi kunena kwa lugha zisizojulikana. La, bwana, walinena kwa lugha nyingi. Hao watu walimwelewa kila mtu, "Tunasikiaje kila mtu katika lugha yetu tuliyozaliwa nayo?" Tendo la Mungu kumtuma Roho Mtakatifu. Hayo yatosha.

173 Neno hili la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, yaani Mpambanuzi wa mawazo ya moyo. Na kitu gani? Linaweza tu kutumiwa kwa mkono mmoja. Upanga una nguvu. Huo—huo hauna kitu ndani yake isipokuwa ushikwe kwa mkono. Basi wakati mkono wa imani unapoweza kuutwaa Upanga wa Mungu, utafanya jambo lile lile alilofanya Yesu. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya."

174 Labda unaweza kukata tu kidogo, labda una mkono dhaifu wa imani, unaweza kukata ya kutosha kusema, "Vema, ninaweza kuona nuru ya mchana ya kutosha kuona nimeokoka." Lakini vipi kuhusu ahadi hizo zingine? Endapo unao mkono wenye nguvu wa imani, lichukue Neno lote la Mungu na ukate kupitia kwenye kila giza, amina, mpaka Nuru ya Mungu imulike ndani, ndipo uangalie uso kwa uso na Mungu, ukisimama juu ya Neno Lake. Amina.

175 Alikuwa na vipingamizi vingi, maskini mwanamke huyu alikuwa navyo. Alikuwa na vipingamizi vingi, lakini imani yake haikuwa na chochote. La, la. Alikuwa amesikia. Imani ilikuwa imetia nanga. Yeye alisikia nayo imani yake ilikuwa imeshikilia. Sasa, huenda walimwambia hili, "Unajua wewe ni Myunani. Unajua kamwe hutapata chochote, kwa sababu kuna ubaguzi, unaona. Kamwe hutapata chochote hapa." Lakini yeye alisikiliza hayo? La, bwana. Alikuwa na imani, na hiyo imani ndiyo yote aliyohitaji, kwa sababu alijua ya kwamba hilo lilikuwa ni Neno la Mungu limesimama hapo. Alikuwa na imani. Baadhi yao huenda walimwambia namna hii, "Lakini ngoja kidogo!" Taifa lake mwenyewe, kanisa lake mwenyewe huenda lilisema, "Sasa ngoja kidogo, siku za miujiza zimepita. Usishuke kwenda huko chini. Siku za miujiza zimepita." Lakini kitu kingine kuhusu imani, inacho chanzo ambacho hakizingatii hayo, wala hakiyaoni kabisa. Alikuwa tayari amelichukua Neno hilo. Yeye ni Neno. Alikuwa na imani ya kulishika Hilo. Akasonga mbele. Huenda walimcheka, kasema, "Vema, kila mtu mwingine atakucheka, maana binti yako atakuwa mgonjwa tu mwaka ujao kadiri alivyo mwaka huu. Angali atakuwa na ibilisi huyo, atakuwa mgonjwa vivyo hivyo tu." Lakini hakusikiliza hayo. Imani ilikuwa imeshikilia, mnaona. "Utafukuzwa kutoka kanisa lako kama ukiwahi kwenda kule katika mmoja wa hiyo. Kumbuka tu, watakufukuza. Watakufukuza." Hilo halikumaanisha chochote kwake. Imani

ilipita juu ya hayo. Alidhamiria kwenda kwa Yesu. Jambo ndilo hilo.

176 Sasa, kuokoa wakati, wakati tungaliweza kuchukua somo la kila mmoja wa hao na kudumu nao, lakini sasa kuokoa wakati. Alipofika kwa Yesu, angali alivunjwa moyo, yeye mwenyewe, bali si imani yake. Wakati alipofika kwa Yesu, Yeye alisema, "Sijatumwa kwa jamii yenu." Ni kukataliwa kubaya jinsi gani! "Sijatumwa kwenu nyinyi watu." Wazia tu, Mtu ambaye yeye alidhani alimwamini sana, na Yeye akamkatalia. "Sijatumwa kwenu ninyi watu, nimetumwa tu kwa Israeli. Wewe ni Mmataifa, hata sijatumwa kwenu. Na, isitoshe, ninyi si kitu ila mbwa." Whiu! Hilo halikuisumbua imani hiyo, aliendelea tu kusonga mbele. Naam, kasema, "Nimetumwa tu kwa kondoo waliopotea wa Israeli."

177 Sasa, kama huyo angalikuwa ni mmoja wetu, loo, jamani, hilo lingetosha. "Dhebebu lenu, halina chochote."

"Looo, alizungumza juu ya dhehebu langu, kamwe sitamsikiliza Huyo tena!" Um-hu, haya basi. Endelea, unaona, kamwe hutapata chochote. Dumu tu na Neno hilo. Mahali hilo Neno lilipo, wewe ambatana moja kwa moja Nalo. Imani ilikuwa imetia nanga!

178 Huenda baadhi yao walisema, "Vema, sasa, nitakuambia nini, watakucheka. Watakutoa kanisani mwako."

"Acha wanitoe. Unaona, ni vema."

179 Yesu alisema, "Sijatumwa kwa jamii yenu, kamwe sikuja kwa ajili yenu enyi watu hata kidogo. Nanyi si kitu ila mbwa, si vema kwangu Mimi kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia ninyi mbwa." Whiu!

180 Vipi kama ingalikuwa ni mmoja wenu Wamethodisti, mmoja wenu Wabaptisti, Wapresbiteri, mmoja wenu Wapentekoste? Loo, jamani! Ungalisema, "Mbona, huyo tapeli! Nitamwambia Daktari *Fulani-wa-fulani* na *Fulani-wa-fulani* a—alisema kweli." Unaona, huna imani yoyote.

181 Yeye alijua palikuwapo na msaada. Alikuwa amesikia. Imani chanzo chake ni kusikia. Kusikia nini? Neno. Alijua kulikuwako na kitu halisi pale. Naam. Angali alishikilia. Haidhuru kama yeye. . . Akasema, "Sasa, kumbuka, sijatumwa kwenu. Baba kamwe hakunituma Mimi kwenu Wamataifa, enyi kundi la mbwa. Mnafikiri ningechukua chakula cha watoto na kukitupa kwenu nyinyi kundi la mbwa wasiostahili? Sijatumwa kwenu." Bali hata hivyo imani yake ilishikilia moja kwa moja.

182 Ndugu, yeye hakuwa ni mmea wa tuta, imbidi kuengwaengwa, kubembelezwa kote kama zao fulani la siku hizi, "Loo, jamani, vema, kamwe sitaenda tena, hayo tu ndiyo yaliyoko kwake." Loo, jamani. Si ajabu huwezi kuushika Upanga huo wa imani, si ajabu unapatana juu ya Neno. Unaenda

mahali fulani ambapo unaweza kusikia namna fulani ya kitu fulani cha kidondoadume kilichowekwa pamoja. Ewe maskini mmea wa tuta, wee. Mdudu wa kwanza atakayekuuma, anakuua, inakubidi kunyunyiziwa wakati wote. "Loo, usiamini upuuzi huo, siku za miujiza zimepita," ni kinyunyizio cha ibilisi. Mgeni katika mazingira magumu!

183 Hakuwa hivyo. Ndugu, yeye alikuwa jasiri. Kweli alikuwa na kitu fulani. Alishikilia. Alifanya nini? Alikubali Yeye alisema kweli. Yeye sikuzote. . .Nayo imani halisi ya kweli, sikilizeni, kama inalikatakata dhehebu lako ama la, itaukubali Ukweli. Naam, bwana, Ukweli, ile imani. Kama una imani, nayo ni Neno la Mungu na ahadi ya Mungu, haijalishi wengine wanasema nini, unaliamini Hilo, unalikubali. Alisema, "Hiyo ni Kweli, Bwana. Mimi ni Myunani, sistahili. Mi—mimi ni mbwa, mimi si. . .Si—sistahili chochote, bali ninafuatilia makombo tu."

184 Mimi ni mtafuta makombo, mwenyewe, nanyi je? Ninataka tu makombo, Bwana. Siwezi kuwa na kanisa kama walilokuwa nalo kwenye Siku ya Pentekoste. Kama siwezi, Bwana, jalia nipate tu makombo yanayoanguka. Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Hili ni Lile." Nami sikuzote nimesema, kama hili si Lile, nitaweka tu hili mpaka Lile litakapokuja, mnaona. Naam. Naam. Nitaliweka tu hili mpaka Lile litakapoonekana. Mnaona? Hili ni Neno. Wakati mtu fulani. . .Sininii. . .Hu—hu—huenda nisiwe na imani ya kutosha kwenda kama Henoko, na kufanya matembezi ya alasiri na kwenda nyumbani pamoja na Mungu, bali nitawaambia jambo moja, kamwe sitasimama njiani mwa mtu yeyote aliye na imani kubwa hivyo. Naam, bwana. Ikiwa anayo, Mungu asifiwe, ninashukuru sana kwa ajili yake. Hebu hilo Neno litie nanga humo ndani. Natumaini Hilo litatia nanga ndani yangu jinsi hiyo mauti yatakapokuja, nione barabara imefunguliwa huko ng'ambo, nitembee moja kwa moja niondoke. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Loo, kwa hiyo mimi ninayafuatilia tu makombo.

185 Lakini, ukijaribu kuwaambia baadhi ya hawa watu wa kisasa siku hizi, unachukua tu makombo. "Loo, la!" Kama hawawezi kuchukua nafasi ya kwanza, hawataki chochote hata kidogo. "Ama utashuka uje kwangu. . ." Kama vile Naamani alivyokuwa na ukoma wake, "Utashuka uje nawe utaupiga mkono wako juu yangu kisha uniambie mambo haya yote mbalimbali, na kadhalika, la sivyo sitaamini Hilo hata kidogo. Hiyo ndiyo njia. Mbona, kamwe sitarudi tena." Hiyo ndiyo sababu hupati chochote. Unaona?

186 Inakupasa kuwa tayari kuokota makombo. Mnasikia hilo? Okota makombo, ndugu yangu, okota makombo, dada yangu, haijalishi Yeye anakupa nini, lipokee tu Hilo. Useme, "Mungu," umshukuru, "ninayo imani ndogo tu, bali hakika nitaishikilia hiyo na kukushukuru Wewe kwa ajili Yake. Ninaamini ya

kwamba ninaweza kufanywa mzima. Naam, Bwana. Ninaamini Neno la Mungu ni kweli, nami nitalishikilia Hili moja kwa moja. Nami nitapata afya.” Wewe angalia kinachotukia. Chukua tu makombo, kombo lililo dogo kabisa. Hakika.

187 Kumbukeni, kamwe hakuwa ameona mwujiza. Alikuwa ni kafiri. Kamwe hakuwa amemwona akifanya miujiza yoyote. Kamwe hakuwa amejua kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Kamwe hakuwa amejua, ila tu kwa kusikia. Lakini alipofika pale, labda, na kuona kitu ambacho Yeye alikuwa amefanya, hilo lilikuwa ni tofauti. Mnaona, waliwasikia wakisema, “Vema, unajua ya kwamba katika Biblia yao inasema Bwana atainua Nabii, Naye atafanya miujiza na kujua siri za moyo, na kuwaambia watu mambo haya, na mambo makuu yatatukia.” “Hiyo ni kweli?” Kamwe hakuwa ameliona likitendwa, bali aliliamini kwa vyovote vile. Haya basi. Haya basi.

188 Ninawazia juu ya Rahabu kahaba, kamwe hakuwa amewaona Israeli, bali alisikia, naye akawaficha wale wapelelezi. Alilikataa kanisa lake—lake mwenyewe, watu wake na kila kitu kingine, na kuwaficha wale wapelelezi, kwa sababu alisikia. Kamwe yeye hakusema, “Ngojeni mpaka nitakapomsikia Yoshua akihubiri wakati mmoja. Acheni nipate wazo langu nikiisha kumsikia akihubiri. Hebu nimwone Mungu akiifungua Bahari ya Shamu mahali fulani, ama acheni nimwone Yeye akifanya jambo kama hilo. Ndipo labda ningaliwaficha ninyi nyote kama ningalikuwa nimeona jambo kama hilo.” Yeye hakungojea hilo. Alisema, “Ninaamini. Tumesikia. Tumesikia.”

189 Ee Mungu, nilisikia, ninajua ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninajua ya kwamba Yeye ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Ninajua ya kwamba Yeye anaishi leo hii katika Kanisa Lake. Ninajua ya kwamba Yeye yupo hapa sasa. Ninajua. Ninajua hiyo aliyokuwa amepiga si picha yangu, ninajua Hiyo ilikuwa ni Yake. Ninajua hiyo ni Nguzo ile ile ya Moto iliyo pamoja nasi leo hii, kwa kuwa inafanya kazi zile zile, ishara zile zile, maajabu yale yale, mambo yale yale Yeye aliyofanya. Ni Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza Israeli. Wakati, Yesu, mtu yeyote anayeijua Biblia yako anajua kwamba Yeye alikuwa ni Malaika wa Agano, Malaika aliyewatangulia huko nyikani. Hivi Kristo hakuninii . . . Musa alihesabu shutuma la Kristo kuwa ni hazina kuu kuliko zile za Misri? Akaifuata Nguzo ya Moto akaingia nyikani.

190 Yesu, wakati alipokuwa . . . Nguzo ile ya Moto ilipodhihirishwa, Yeye alisema, “Nimetoka kwa Mungu na ninarudi kwa Mungu.” Akarudi kwa Baba.

191 Ndipo baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, na kupaa juu, Paulo, Sauli ambaye wakati huo alikuwa ni wa Tarso, akiwa njiani kwenda Dameski, alipigwa akaangushwa na Nguzo iyo hiyo ya Moto, ambapo hakuna mtu mwingine aliyeiona Hiyo.

Wote waliosimama karibu, hawakuiona Hiyo, bali Sauli aliiona. Ndipo Sauti ikasema, "Sauli, Sauli, mbona wanitesa Mimi?"

Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu." Mnaona? "Nimetoka kwa Mungu, naenda kwa Mungu."

192 Sasa, kama niliwaambia ya kwamba uhai wa John Dillinger ulikuwa ndani yangu, mngenitarajia kuwa na bunduki kubwa huku nje kuwapiga risasi. Ningaliwaambia uhai wa mwanasanaa ulikuwa ndani yangu, mngenitarajia kuchora picha ya mwanasanaa. Sikilizeni, enyi kanisa! Siwakemei. Angalieni, iwapo Uhai wa Kristo umo ndani ya kanisa, utafanya ninii. . . Iwapo Roho Mtakatifu yuko ndani ya kanisa, ikiwa Nguzo hii ya Moto ambayo sayansi imeipiga picha yake, na kadhalika, tunayoiona hapa kanisani wakati wote, ikiwa huyo ni Roho wa Kristo, atafanya kazi za Kristo. Yesu alisema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo. Hizo ndizo zinazonishuhudia Mimi." Kama Roho Mtakatifu angali halisi, basi Roho Mtakatifu atajishuhudia Mwenyewe. Aminini kazi za Roho Mtakatifu.

193 Kumekuwako na imani nyingi za kujisingizia na maigizo. Mnatarajia hayo. Mungu alisema yangekuja. Lakini inajaribu kufanya nini? Kama kuna dola ya bandia, haina budi kufanyizwa kutoka kwa iliyo halisi. Mmewaona watu wakidai kuwa na Roho Mtakatifu, na kuishi katika uzinzi, na kunywa pombe, na kila kitu kingine, hawanaye Huyo. Wanajaribu kumwigiza. Bali kuna mtu halisi wa kweli aliye na Huyo, aliye na Roho Mtakatifu, naye Mungu huyathibitisha Maneno Yake kwa ishara zinazofuata. Kahaba alisikia, akaliamini Hilo.

194 Sasa, mwanamke huyu, mwanamke huyu Msirofoinike, yeye aliamini pia, Myunani huyu. Akasema, "Bwana." Kwanza alisema, "Ewe Mwana wa Daudi." Mmataifa hana uhusiano na Kristo kuwa Mwana wa Daudi; hiyo ilikuwa ni kupitia kwa Mfalme Daudi, ile jamii ya Wayahudi. Hakumjali kabisa. Lakini alipogeuka na kusema, "Bwana, unisaidie!" Amina, hilo lilimpata. Yeye alikuwa ni Bwana wake; sio Mwana wa Daudi, bali Yeye alikuwa ni Bwana wake. "Bwana, unisaidie!" Hilo lilimshika. Naye. . . Yeye akageuka. Kasema, "Ni kweli mbwa hula makombo kutoka mezani pa bwana. Hiyo ni kweli." Angalieni nini, mwanamke huyo alikuwa na maajilio mazuri kwa karama ya Mungu. Alisema nini? Yeye alisema alilijilia vizuri.

195 Yeye alimtahayarisha, Yeye akasema, "Ninyi ni. . . Sijatumwa kwenu. Ninyi ni mbwa katika kizazi chenu. Jamii zenu si kitu ila mbwa. Mimi sijatumwa kwenu."

196 Naye akasema, "Ni kweli, Bwana." Hilo hapo Neno. Amina. Dumuni na Neno. Imani daima italitambua Neno. "Lakini mbwa

hula makombo chini ya meza za bwana zao.” Hilo lilimshika. “Bwana, unisaidie!”

197 Yeye aligeuka akasema, “Kwa usemi huu, Ewe mwanamke, imani yako ni kubwa. Na, kwa usemi huu, ibilisi amemwacha binti yako.” Ati nini, yeye alipata nini? Aliiendea karama ya Mungu kwa njia ifaayo. Inakubidi kuiendea . . . Pia, kumbukeni, huyo alikuwa ndiye Mmataifa wa kwanza aliyepata kufanyiwa mwujiza juu yao na Mwana wa Daudi. Kumbukeni, huo ulikuwa ndio mwujiza wa kwanza uliofanyiwa Mmataifa, hiyo ni kweli, uponyaji huu wa mwanamke Msirofoinike. Hiyo ni kweli. Aliiendea karama ya Mungu kwa njia sahihi. Imani hukubali Neno ni kweli. Uchaji, unyenyekevu. Mnaona?

198 Huendi huku na huku ukisema, “Hum! Si—sitaamini upuuzi huo. Iwapo katekismo yetu haisemi hilo, um-hu, mimi silioni.” Haijalishi kile katekismo yako inasema, unaiweka katekismo ama chochote kile juu ya Neno la Mungu? Neno la Mungu ni la kweli. Kila kitu kingine ni cha uongo. Mnaona?

199 Naye akaja kwa uchaji, kwa amani, kwa uchaji, kwa unyenyekevu. Inakupasa kuwa mnyenyekevu. Njia ya kupanda ni kushuka, daima. “Yeye ajidhiliye atakwezwa, bali yeye ajikwezaye atadhiliwa.”

200 Mwangalieni Martha siku ile. Loo, najua ninawaweka kwa muda mrefu, bali ni—nitailipa siku moja kwenu na kufanya mfupi kabisa. Sikilizeni, ninayo mambo machache tu zaidi ya kusema sasa hivi, nitaondoka. Natumaini siimalizi saburi yenu. Martha, yeye alikuwa na ninii sana, aling’ang’ania sana Uweponi mwa Yesu. Angalieni, alikuja huko juu na kusema, “Bwana.” Sasa, kumbukeni, yeye aliagizia Yeye aje akamwombee ndugu yake, wala Yeye hakufanya hivyo.

201 Sasa, katika Yohana 5:18, Yesu alisema, Yohana 5:19, ninaamini ndipo, Yesu alisema, alipopitia kwenye birika la Bethesda pale, Naye akaona, Yeye alimjua mtu mmoja aliyekuwa hawezi kwa muda wa miaka thelathini na minane. Angalieni, yapata watu elfu mbili wamesimama pale, watoto wenye vichwa vilivyojawa maji, viwete, vipofu, vilema, waliopooza, waliopindika. Yesu akapitia kwenye hilo birika, akaangalia kote, amejawa upendo, amejawa huruma. Mnaona, hatujui maana ya upendo. Tunauchukulia upande wa kibinadamu. Amejaa huruma, hakika, mnazungumzia huruma za kibinadamu. Huruma halisi ni kufanya mapenzi ya Mungu. Mnaona? Hilo hapo.

202 “Loo, nisingesema lolote kwake, maana yeye ni mvulana mzuri. Hu—hu—hunywa pombe, hufanya *hivi*.” Anamhitaji Kristo. “Nisingelimwambia, kwa kuwa amekuwa mfuasi wa kanisa hilo muda mrefu. Nisingetaja uponyaji wa Kiungu kwake.” Loo, ndugu, hujui huruma ni nini.

203 Yesu alipitia pale, Yeye aliyajua mapenzi ya Mungu. Kumbukeni, Yeye ndio—Yeye ndio kwanza amfufue mtu aliyekufa. Basi kumbukeni kilichotukia pale. Yeye alipitia kwenye lile birika pale, akapitia kando ya birika hili, kulikuwako na akina mama wenye watoto wachanga. Walikuwa wakijaribu kumngojea Malaika wa Bwana ayatibue hayo maji. Akaenda pale, akamwendea mtu aliyekuwa hawezi, hebu tuseme ugonjwa wa kibofu. Alikuwa nao miaka thelathini na minane. Ulikuwa umedumaa. Usingemuua. Akasema, "Wataka kuwa mzima?" Vipi kuhusu huyu kipofu, kiwete, kipofu, aliyelemaa, aliyepooza? Kasema, "Ungetaka kuwa mzima?" Mnaona, Yeye alijua hasa mahali pa kwenda. Mungu, Neno, alimwongoza. Sasa, Yeye alisema, "Wataka kuwa mzima?"

204 Akasema, "Bwana, mimi sina mtu wa kunitia birikani." Angeweza kutembea. Kasema, "Ninaposhuka mimi, mtu mwingine hushuka mbele yangu."

205 Akasema, "Jitwike godoro lako uende nyumbani mwako." Yeye alisailiwa. Nao wakamleta Yesu mahakamani wapate kumsaili.

206 Na kama Yeye angefanya jambo lilo hilo leo hii, angeulizwa maswali. Kweli. "Aliwaacha elfu mbili, na hao je? Ninamjua maskini Ndugu *Nanii* huko chini. Dada *Nanii*, yeye ni mwanamke mzuri. Amekaa kule miaka ishirini. Iwapo kuna Mungu yeyote kumhusu Yeye, angalishuka kule na kufanya hivyo." Ibilisi yuyo huyo wa kale husema jambo lilo hilo leo hii. "Kama Wewe ndiwe. Kama hili ndilo. Kama lile ndilo." Ibilisi yule yule wa kale, mnaona, jambo lile lile la kale.

207 Kwa hiyo hawa Mafarisayo walikuwa wakimwuliza Yeye maswali huko juu kuhusu mambo haya. Mwangalie Yeye, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe ila lile analomwona Baba analitenda." Yeye—Yeye alikuwa na ono. Hilo ono likamwonyesha Yeye. "Ninalomwona Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile." Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaona, Mungu yule yule.

208 Sasa, Martha, katika Uwepo Wake, alikuwa amesimama pale. Akasema, "Bwana, kama Wewe ungalikuwapo hapa."

209 Sasa, kwa nini Yeye hakuja? Kwa sababu Baba alikuwa amemwonyesha ono ya kwamba Lazaro alikuwa anaenda kufa. Sasa, angalieni, wa—waliagizia, na Yeye akaenda kwenye mji mwingine. Kisha wakaagizia tena, Yeye akaenda kwenye mji mwingine. Ndipo hatimaye Yeye akasema, "Lazaro amelala usingizi." Loo, wao. . .Hayo ndiyo matamshi aliyokuwa nayo. Hakuna mauti kwa Mkristo. Tunajua hilo.

"Loo," wao walisema, "kama amelala, anafanya vema, anapumzika."

210 Kasema, "Lakini amekufa," akawaambia katika lugha yao. "Lakini naenda kumwamsha." Loo!

211 Akaenda mahali alipokuwa, loo, ninaweza kuona hili. Akaingia mjini, naweza kuwasikia Wayahudi wakisema, "Haa-ha, yule pale mponyaji wa Kiungu! Haa-ha. Nao waliliacha kanisa lao, kila kitu kingine, wapate kumfuata. Ndipo wakati kisa halisi kilipotokea, hata rafiki Yake, Yeye aliponyoka kutoka mjini. Wakaagizia aje, sasa Yeye amerudi." Yesu akazidi kuenda mbele.

212 Lakini maskini Martha, kitu fulani ndani ya moyo wake, kitu fulani. Siku zote alikuwa na namna fulani ya uzito wa kutenda, alitaka kuweka nyumba safi na kila kitu, naye Mariamu alilisikiliza Neno. Lakini hapa ndipo alipoonyesha jinsi alivyo hasa, aliponyoka moja kwa moja akashuka kule. Sasa, yeye, mnajua yale ninayoamini, alikuwa amesoma kuhusu yule mwanamke Mshunami, Mshunami, mwajua, katika Biblia. Sasa, angesema nini? Akatoka nje, akasema, "Bwana." Hivyo ndivyo Yeye alivyokuwa. Ilionekana kana kwamba alikuwa na haki ya kumkemea, aseme, "Kwa nini hukuja? Mbona, hatutaninii . . . Tunaamini sasa Wewe kweli ni mtakatifu anayejibingirisha." Mnaona, mwujiza huo usingalitendeka.

213 Na hiyo ndiyo sababu hauwezi kutendeka siku hizi. Loo, Yeye yupo hapa katika umbo la Roho, sio kwamba unamwona Yeye, bali nini: Yeye ni Roho pamoja na Neno Lake. Mnaona? Loo, hakika. Mnauombea uamsho, nao unatokea kanisani, jambo moja ama lingine linatukia, na mtu fulani akipaza sauti "utukufu kwa Mungu, haleluya," mngelifunga hilo kanisa. Hamjui uamsho ni kitu gani. Kristo anakuja kanisani, halafu hata hamumkaribishi. Anafanya mwujiza na kumponya mtu fulani, na kusema, "Vema, huenda ilikuwa ni telepathia." Si ajabu Yeye hawezi kufanya kazi miongoni mwenu. Si ajabu kanisa la Laodikia, Yuko nje, akibisha, akijaribu kurudi ndani ya kanisa Lake Mwenyewe. Huo ndio wakati tunaoishi sasa. Madhehebu haya yamemkataa hata Yeye yuko nje, akijaribu kurudi ndani. Hiyo ni kweli, ametupwa nje!

214 Sasa, tunaona ya kwamba Martha alimwendea Yeye, akasema, "Bwana, kama Wewe ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa Wewe."

215 Mwangalieni, Yeye alimjaribu. Akasema, "Ndugu yako atafufuka tena."

216 Kasema, "Naam, Bwana. Yeye alikuwa ni mvulana mzuri, atafufuka katika ufufuo wa kiama. Atafufuka katika siku ya mwisho."

217 Akasema, "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima." Hapo likawekwa jaribio. Mtu amesimama pale akisema . . . Yeye alikuwa ndiye Mtu pekee aliyepata kuishi, Mtu pekee atakayepata kuishi

ambaye angeweza kusema hivyo, Mwana wa Mungu, alisema, "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima."

218 Biblia ilisema, "Hana uzuri hata tumwangalie Yeye." Labda mabega Yake madogo yaliinama chini, akiingia mvi, wakati akiwa na umri wa miaka thelathini na Yeye akaonekana alikuwa na hamsini.

219 Kasema, "Wewe unao umri wa miaka hamsini tu, nawe wasema umemwona Ibrahimu. Sasa tunajua Wewe una kichaa." Mnaona? Kazi Yake labda ilimdhoofisha.

220 Akasema, "Kabla Ibrahimu hajakuwako, Mimi niko." Amina. Hawakujua hilo. Huyo hapo ametiwa utaji katika mwili wa binadamu.

221 Kasema, "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Unayasadiki haya?"

222 Akasema, "Naam, Bwana. Nimesadiki ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu yule ajaye ulimwenguni."

"Mmemzika wapi?"

223 Ninalo jambo dogo hapa ambalo nimelisema sikuzote, mwajua, natumaini kama nikiudhi hisia za mtu yeyote silitendi makusudi. Mwanamke wa Sayansi ya Kikristo aliniambia wakati mmoja, kasema, "Ndugu Branham, unamjivunia Yesu kupita kiasi."

224 Nikasema, "Loo, la, la." Nikasema, "Sijivunii nusu vya kutosha. Laiti ningalikuwa na lugha zaidi ningaliweza kumjivunia kwayo." Mnaona?

Naye akasema, "Vema, unamfanya Yeye Mungu."

Nikasema, "Yeye alikuwa ni Mungu! Angali ni Mungu. Daima atakuwa ni Mungu."

Akasema, "Yeye alikuwa mwanadamu. Alikuwa ni mtu."

Nikasema, "Alikuwa ni Mwanadamu na Mungu pia."

225 Akasema, "Nitakuthibitishia Yeye alikuwa ni mwanadamu tu, kwa Biblia yako mwenyewe."

Nikasema, "Hebu nikusikie ukifanya hivyo."

226 Akasema, "Yohana Mtakatifu, mlango wa 11, Yesu alienda kwenye kaburi la Lazaro Naye akalia."

Nikasema, "Hilo ndilo Andiko lako?"

Akasema, "Ndiyo."

227 Nikasema, "Dada!" Simaanishi kukufuru. Hapa si mahali pa utani, bali nililisema tu kwa ajili yake. Nikasema, "Hiyo ni nyembamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa." Nikasema, "Mbona, unajua vema na vizuri

kwamba lisingekuwa ni jambo kama hilo.” Nikasema, “Hebu nikwambie jambo fulani.”

228 Huyu hapa anaenda, mabega yameinama, akilia, Yeye hulia pamoja nawe unapolia. Anayahisi maumivu yako. Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wako. Akilia, akishuka kwenda kaburini, akijua yale Baba alikuwa amemwambia. Kwa kuwa Yeye alisema hakutenda lolote mpaka Baba alipomwonyesha. Huyo hapo, mnaona, akienda. Yeye alikuwa akienda kumfufua, bali angeweza kulia kibinadamu pamoja na wanadamu. Anaenda kaburini, akilia. Lakini wakati Yeye aliposimama pale, loo, jamani, kasema, “Liondoeni hili jiwe.”

229 Kasema, “Ananuka!” Pua yake ilikuwa imebonyea tayari. Saa sabini na mbili, mnaona, ama siku nne mchana na usiku. Mnaona, uso wake umebonyea, ameharibika, ameoza.

230 Kasema, “Liondoeni jiwe.” Akasimama huko nyuma na kusema, “Baba, nakushukuru Wewe kwamba sikuzote umenisikia Mimi, bali ni—nimesema tu hili.” Mnaona, Yeye tayari alikuwa amemwambia. Akasema, “Nasema hili tu kwa ajili ya hawa waliosimama hapa.” “Lazaro, njoo huku!” Amina. Naye mtu aliyekuwa amekufa siku nne, akasimama kwa miguu yake akaishi tena. Huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Hakika alikuwa.

231 Huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu aliyeshuka kutoka mlimani usiku mmoja, yuna njaa, akitafuta chakula. Yeye alikuwa ni Mwanadamu, alikuwa na njaa ya chakula. Lakini wakati Yeye alipochukua samaki watano, ama biskuti tano na samaki wawili, na kuwalisha elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Hiyo ni kweli. Ni kweli. Naam, bwana.

232 Alikuwa ni Mwanadamu hapo alipokuwa amelala nyuma ya mashua hiyo usiku huo, amechoka sana, nguvu zimemtoka, akihubiri na kuponya, ndipo pepo akaja, na labda pepo elfu kumi wa baharini, kasema, “Tutamzamisha sasa, Yeye amelala.” Kama walivyomfanyia Paulo huko nje kwenye dhoruba. “Tumempata sasa, tumemtega. Yeye amelala, tutaizamisha meli hiyo.” Ibilisi akipulizia upepo wake kule, nayo ikirukaruka juu chini namna hiyo. Hayo mawimbi hata hayakumwamsha. Yeye alikuwa ni Mwanadamu amelala huko nyuma, mchovu, amelala usingizi.

233 Lakini mara alipoamka, loo, jamani! “Loo, nendeni mkamwamshe Yesu!” Akauweka mguu Wake. . .Loo, enyi kanisa, hivyo ndivyo inavyowapasa kufanya. Laiti ningalikuwa na wakati ningalihubiri sasa, mnaona, juu ya hilo. Mnaona? Akaweka mguu Wake juu ya demani ya huo mtumbwi, akaangalia juu, kasema, “Amani, tulia.” Mnaona? Nayo mawimbi na pepo zikamtii. Huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, ilihitaji Mungu kufanya hivyo.

234 Naam, Yeye alilia msalabani, apate rehema. Hiyo ni kweli. Akaona kiu msalabani. Alikufa kama mwanadamu. Lakini kwenye asubuhi ya Pasaka, wakati Malaika alipoliondoa lile jiwe, ndipo Mtu aliyekuwa amekufa, akayashinda mauti, kuzimu na kaburi pia, akatokea, ameshinda mauti, kuzimu na kaburi. Kasema, "Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa, nami ni hai milele." Huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Mtu huyo. Naam, bwana.

235 Imani kamwe haiikani Kweli Yake. Loo, kama kusema, "Nguzo ya Moto, hiyo haikuwa ni kweli. Nayo miujiza ya Musa haikuwa ya kweli," sikuzote wangesema. Haijalishi ni la dhihaka jinsi gani, linadumu moja kwa moja hasa pamoja na Neno. Kweli kabisa. Loo, unaweza kuwa—unaweza kuwa mng'ang'anizi. Unaweza kushikilia kwa dhati wakati wowote unapolishika Neno la Mungu, unapolishikilia Hilo.

236 Kama vile Mikaya alivyokuwa, Mikaya papo hapo, wakati manabii mia nne walipokuwa wamesimama pale, wakisema, "Kwea, Ahabu, kwea." Mikaya alijua ya kwamba ono lake lilikuwa ni kulingana na Neno la Mungu. Yeye alinena Neno kwa vyovyote vile. Wao walisema, "Tutakutupa korokoroni, na kukupa maji ya huzuni na mkate wa huzuni."

237 Akasema, "Nitupeni ndani mkitaka." Yeye alikuwa ni nini? Aling'ang'ania. Alilifahamu Neno la Mungu. Alijua mapenzi ya Mungu. Alikuwa ameona ono. Alijua lilikuwa ni kitu gani. Hilo ono lilitoka kwa Mungu, kwa sababu hayo maono yalilingana na Neno la Mungu. Siku hizi, kila mwaminio hana budi kupiga vita, nawe huna budi kupiga vita, pia.

238 Mtu mmoja hapa muda fulani uliopita alikuwa akiniambia, kasema alienda kwenye. . . kasema, "Unajua, ma—maskini pepo mdogo sana *hivi* alisimama mbele yangu wakati mmoja katika ndoto." Akasema, "Ibilisi huyo alisema, 'buu'; nami nikafanya 'umhu.' Kisha," kasema, "kila wakati ningeruka nyuma, yeye angekuwa mkubwa zaidi nami nikawa mdogo zaidi." Kasema, "Muda si muda wajua, 'buu,' nami ningeruka nyuma. Naye. . . kila wakati akisema, 'buu, buu,'" anamrukia. Kasema angerudi nyuma, arudi nyuma, arudi nyuma. Kasema, "Yeye akawa mkubwa kuliko nilivyokuwa." Ndipo kasema, "Nilijua ilinibidi kupigana naye. Kwa hiyo si—sikupata chochote, kwa hiyo nilichukua tu Biblia, nami. . . akafanya 'buu'; nikafanya 'buu,' pia." Kasema, "Yeye akaanza kuwa mdogo." Hiyo ni kweli.

239 Hivyo ndivyo inavyokubidi kufanya, lichukue Neno la Mungu. Haikubidi kusema "buu," bali sema, "BWANA ASEMA HIVI!" Shikilia, simama kwenye Neno! Ni Kweli. Tunaliamini Neno siku hizi. Tunaliamini Hilo kama Mikaya alivyoliamini. Tuliliamini kama hao wengine wanavyoliamini. Haijalishi ni wangapi wanaosema Hilo si kweli, lingali ni kweli. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. "Yeye aniaminiye

Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Mtu yeyote angeweza kukuponya? La, bwana. Tayari, umeponywa tayari. Mtu yeyote anaweza kukuokoa? Limefanyika tayari. Ni wangapi wanaoamini hilo? "Yeye *ali*jeruhiwa kwa makosa yetu. *Ali*chubuliwa kwa maovu yetu." Hiyo ni kweli? Kweli. "Na kwa mapigo Yake sisi tu*li*ponywa," wakati uliopita. Kila kitu Yeye anachoweza kukufanyia kimefanywa tayari.

240 Sasa Yeye aliweka kanisani, kuliweka kanisa sambamba na Neno, kitu gani? Mitume, manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti, ofisi za kanisa. Waliotumwa na Mungu, sio walioitwa na mwanadamu. Watu waliotumwa na Mungu, waliovuviwa kuliweka kanisa sawa. Sasa, ni kitu gani? Karama za Roho kanisani. Sio kundi la ushupavu, bali kweli ni karama za Roho kanisani. Hiyo ni kweli, kuliweka kanisa. Kama kanisa halisi lilikusudiwa na Mungu, limejazwa kweli na Roho Mtakatifu, kama dhambi ingeonekana kanisani, ingekuwa kama Anania na Safira wengine. Wakati kanisa halisi...Ningetaka kuingia katika moja, niwaone wanawake wote na wanaume chini ya Nguvu za Roho Mtakatifu. Kama mtu fulani alikuwa amefanya kosa fulani, Roho Mtakatifu anasimama papo hapo na kulifunua. Ingewabidi kujitakasa. Hizo ni karama za Roho kanisani. Ee Mungu, tutumie kanisa kama hilo, tutumie moja kama hilo. Unaamini jambo hilo? Kristo, Yeye amekufa? Yu hai.

Yeye alikuwa vipi? Alimwambia mwanamke pale...

241 Yeye alisema, wakati Mfarisayo alipomwuliza kuhusu ishara, Yeye alisema, "Enyi kizazi cha zinaa mnatafuta ishara." Hiyo ni kweli? Kizazi kiovu na cha zinaa! Akasema, "Wataipata. Wataipata hiyo ishara, kizazi hicho kiovu na cha zinaa." Ni lini kulipata kuwa na kizazi kiovu na cha zinaa kuliko tulicho nacho sasa? Ni lini kulikuwako na dhambi zaidi? Tunao watu wengi zaidi juu ya nchi sasa hivi, wanatwambia, kadiri ya watu wengi duniani sasa hivi waliopata kuwa duniani tangu Adamu, wako duniani sasa hivi. Hiki ndicho kizazi kile kiovu na cha zinaa. Walawiti, upotovu, kila kitu, kinaongezeka kwa maelfu na maelfu. Makanisa yakianguka, "Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wasiowapenda walio wema, wenye mfano wa utauwa," kama alivyosema Roho, "huku wakikana Nguvu zake. Hao nao ujiepushe nao!" Unaona? Biblia ilisema, "Ujiepushe nao!" Tunaishi katika siku hiyo.

242 Sasa, kumbukeni, kunao watu wanaozunguka, wakisema, "Ninazo nguzu za kuwaponya." Jamaa huyo anawaambia uongo. Yeye hana nguvu za kukuponya. Kristo tayari amefanya hivyo! Loo, kwa kukiri dhambi, na kadhalika, na kasisi fulani ama mhudumu akikusamehe dhambi zako? La, bwana, dhambi zako zimesamehewa tayari. Wakati Kristo alipokufa msalabani, Yeye alisema, "Imekwisha." Ati nini? Mpango mkamilifu, kila kitu.

Kristo alifanya hivyo pale msalabani. Umeokolewa tayari. Kila mwenye dhambi ameokolewa, bali hautakufaa kitu mpaka uukubali. Ukishuka pale madhabahuni na kupiga makelele, ulie mpaka uingie mvi na nywele zako zianguke, haitafaa kitu mpaka uamini, uamini kwamba Kristo alikufa badala yako, nawe. . . Alikufa kama upatanisho wa dhambi zako, unapomkubali kama Mwokozi wako. Ndipo wokovu unakujia. Jambo lile lile kwa uponyaji. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tumepona."

243 Kunalo jambo moja tu ambalo Kristo angeweza kufanya leo hii kuonyesha ya kwamba Yeye yuko. Jambo la kwanza, ni, huna budi kuamini juu ya msingi wa Neno Lake. Hiyo ni kweli kabisa, ukweli wa Neno. Lakini Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi!" Sasa, Yeye kamwe hakusema, "Mimi humponya" mtu yeyote. Kama Yesu alisema, "Si Mimi nizitendaye kazi, ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu," sasa kama Yesu hangeweza kuchukua jina la "mponyaji wa Kiungu," vipi kuhusu maskini baradhuli kama mimi, ama mtu mwingine, ama mtu mwingine yeyote, na kujaribu kuwa mponyaji wa Kiungu? Unawezaje kuwa mponyaji wa Kiungu wakati tayari, kila mtu angaliweza kuponywa ameponywa tayari? Inakubidi kuukubali, kuuamini. Sasa, hiyo ni kweli? Hilo ndilo tunalotaka kujua. Hiyo ni kweli?

244 Sasa, kama usingalilichukua neno langu, ingekubidi tu kwenda, ama ninii yako. . .nisingelichukua neno lako, ingebidi liende. Bali Mungu sivyo alivyo, Yeye hutuma karama kanisani, mitume. Mtume ni nini? Mmishenari. Mmishenari, neno *mmishenari* linamaanisha "mtu aliyetumwa." *Mtume* linamaanisha "mtu aliyetumwa." *Nabii*, huyo ni "mwonaji." Mchungaji, mwalimu, mwinjilisti, mambo hayo yote, yanaligawanya Neno la Mungu kwa halali, kulishusha Hilo chini, kisha zi—zile karama za Roho kutenda kazi kanisani, kulihakikisha Neno, kuonyesha kwamba Yesu Kristo anaishi kanisani.

245 Sasa, sote tunafahamiana, hili ni kundi letu tu la kanisa. Sijui kama kuna yeyote. . .Mimi sipo hapa mara nyingi mno kujua kama ni wageni ama kama si wageni, na kadhalika. Lakini, enyi marafiki, leo hii, ninyi watu mlio wagonjwa sasa, kama kulikuwapo na jambo lolote la kufanya kuwasaidia, ningelifanya. Kama nilijua kwamba mtu fulani hapa ni mgonjwa, hasa sana dada huyu hapa ninayemwona kwenye kitanda cha wagonjwa, kama nilijua kulikuwako na jambo fulani ambalo ningalifanya, kama vile kuchukua, kuisukuma sarafu kwa pua yangu kulizunguka jengo zima la mji, kote, ningefanya hivyo. Ningetoka moja kwa moja huko na kusema, "Msinifunike kwa mwavuli, kama kulikuwa kukinyesha, acheni tu niisukume. Ninataka kumwonyesha Mungu kwamba mimi ni mwaninifu." Sasa, hilo halingefaa kitu. Nimekuwa Afrika, nami ninajua ambako wanalalia misumari huko India, na kila namna

ya mambo, kuwatolea miungu dhabihu, na kuwapa mamba watoto wao, na kila kitu kingine. Hilo silo; huo ni uaminifu, bali mtu anaweza kunywa asidi kaboliki kwa uaminifu akidhani ni dawa. Mnaona? Mnaona, hu—huna budi . . . Jambo lililo kweli ndilo tunalotaka kujua, naye Mungu huushuhudia Ukweli Wake. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nilizofanya Mimi yeye naye atazifanya." Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule!"

246 Yeye angekuwa nini kama ulimtafuta leo hii? Kama nikiwaambia Kristo yuko ndani yangu, Kristo yuko ndani yako, tunaweza kutarajia nini? Ungemtarajia mtu mwenye ukosi uliopinduliwa, na kitu fulani? La, la, Yeye hakutenda jinsi hiyo, Yeye alivalia kama watu hao wengine. Kama alikuwa na makovu mkononi mwake? Mtu yeyote anaweza kufanya makovu mkononi mwake, alama za miiba. Wana madazani yao kote nchini sasa, waigaji, na damu na moto na moshi, kila kitu. Hilo silo—hilo si Neno! "Kazi nizifanyazo Mimi!" Yesu alisema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nifanyazo. Zitanishuhudia Mimi. Hizo ndizo zinazosema kwamba Mimi ni Nani."

247 Sasa hebu tuombe kwa muda kidogo. Iweni na haja zenu moyoni mwenu. Baba wa Mbinguni, najua hili limekuwa ni fidhuli na gumu. Nakuomba uturehemu. Simaanishi . . . Unaujua moyo wangu, Bwana, bali ninaomba tu ya kwamba Wewe utanisaidia sasa. Ninaomba ya kwamba utayaruhusu maneno haya, ingawa yamevunjikavunjika na kukatikakatika, na—na si kama vile mhudumu anavyopaswa kufanya, Bwana. Nami hapa, bila elimu, sijui jinsi ya kuzungumza na watu, lakini yote nijuayo ni kwamba Wewe uliahidi kama ningekifungua kinywa changu Wewe ungekijaza. Hiyo imekuwa ni miaka thelathini na moja nimekutumainia Wewe katika jambo hilo. Kwa hiyo, Baba, mahali fulani, labda baadhi ya watu wamekusanya Maneno machache, wale walio wagonjwa, ama wale wanaomhitaji Kristo. Wako—wako huko nje mahali fulani. Wa—wanakuhitaji Wewe, Bwana, nami ninatumaini ya kwamba jambo fulani limesemwa ambalo litainua imani yao katika ahadi Zako. Ninaomba ya kwamba Wewe utatujalia baraka hiyo.

248 Sasa wakati vichwa vyetu vimeinamishwa, kuna wale hapa ambao hawamjui Kristo kama Mwokozi, wangesema, "Ndugu Branham, ni—nisingetaka kufa namna hii. Si—sistahili kufa. Kama nikifa, ningepotea. Sijazaliwa mara a pili. Ha—hakika ninataka sana maombi yako sasa hivi. Niombee, mimi ni mwenye dhambi"? Inua tu mkono wako, sivyo, useme, "Nikumbuke tu . . . " Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe. Mungu awabariki. Kweli maanisha hilo kutoka moyoni mwako. Mungu awabariki. Dazani moja ama mbili ya mikono kwenye kundi hili dogo la watu hapa. Kundi hili dogo la watu hapa, yapata mia moja ama mia mbili, kitu kama hicho, nayo hii hapa mikono dazani moja. Papo hapo ulipo. Madhabahu yamejaa watoto walioketi. Hakuna

njia kwangu kuwaleta hapa madhabahuni, lakini, papo hapo mlipo, ombeni pamoja nami.

249 Baba wa Mbinguni, ninakuletea watu hawa walioinua mikono yao. Ninaamini walifanya hivyo kwa uaminifu mkubwa. Jalia wajue kwamba walivunja kila kanuni ya sayansi papo hapo. Sayansi inathibitisha kwamba mikono yetu haina budi kuning'inia chini, kwa sababu nguvu za uvutano za dunia huiweka chini. Lakini inaonyesha kwamba kulikuwako na Roho ndani yao ambaye ana mamlaka, nguvu za mkono huo, kwamba waliuinua kuelekea kwa Muumba aliyeufanya. Hiyo ilionyesha papo hapo. Isingeweza kuthibitishwa kisayansi, kwa sababu Roho anajulikana tu…Ni imani. Tunaamini Hiyo. Na hapa Roho fulani amewajia na kuwaambia wainue mikono yao, kwamba walitaka kuokoka.

250 Sasa, Baba Mungu, ninatambu-…Ninazinukuu ahadi Zako. Bwana Yesu Kristo alisema, wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba, watakuja Kwangu. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele. Yeye aulaye Mwili Wangu na kunywa Damu Yangu, yuna Uzima wa Milele, nami nitamfufua katika siku za mwisho." Hizi ni ahadi. Sasa, watu hawa wasingeweza kuinua mikono yao isipokuwa kulikuwako na Roho fulani pale aliyewaambia walikuwa wamekosea. Wasingeweza kufanya jambo hili isipokuwa Wewe ulikuwa umewakusudia tangu zamani. "Wote ambao Baba tayari," *tayari*, wakati uliopita, "amenipa Mimi, watakuja." Tumekusudiwa Uzima wa Milele. Wale aliotangulia kuwajua, Yeye amewaita; wale ambao amewaita, Yeye amewahesabia haki; wale aliowahesabia haki, Yeye amewatukuza tayari mbele za Mungu. Ni ono tu kuu la Mungu likiendelea, likitimizwa. Watu hawa, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Wewe Ambaye huna kikomo uliujua huu mkutano asubuhi ya leo, na ukajua wangeinua mikono yao, na sasa wameinua mkono wao.

251 Hilo tu ndilo ninalojua kufuatilia, Bwana, ni Neno Lako. Basi, katika Jina la Yesu Kristo, ninakukabidhi Wewe hawa walioinua mikono yao, kama kumbukumbu za Neno Lako. Waweke, Ee Bwana Mungu, hakuna anayeweza kuwanyakua kutoka mkononi Mwako. Wape Uzima wa Milele. Jalia wapate kanisa, ama wakae papa hapa asubuhi ya leo na wabatizwe kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao, ama kukiri imani yao. Wajalie wao, watakapotoka ndani ya maji, kama vile Roho Mtakatifu hapo mwanzo alivyotembea juu ya maji, jalia Roho Mtakatifu awe hapo kuijaza mioyo na nafsi zao. Tujalie, Bwana. Jalia waishi kwa utauwa siku zote za maisha yao, na wawasilishwe kama kumbukumbu na vito katika taji Yako kwenye siku ile. Kupitia Yesu Kristo Bwana wetu, tunaomba. Amina.

252 Bwana awabariki. Sasa, kweli ninapaswa kuwa nimeondoka saa moja iliyopita. Lakini sasa tutaitisha mstari wa maombi. Ngojeni, kunazo kadi zozote za maombi zilizosambazwa? Kuna mtu yeyote aliye na kadi za maombi? Billy yuko wapi, Billy yuko karibu? Moja hadi hamsini? Alisema alisambaza kadi hamsini za maombi. Vema, sasa, hatuwezi, kunao wengi sana waliosimama. Sasa, nyote mwaweza kutupa muda wa dakika chache tu sasa? Kama ninyi. . . Sasa, yote niliyosema. . . Sasa, hebu—hebu kidogo tu, ninajua chakula cha kutwa hakitaungua. Ngojeni kidogo, *Hili* ni zaidi, *Hili* ni bora kuliko chakula cha kutwa (linapaswa kuwa): Neno la Mungu.

253 Sikilizeni enyi marafiki, ninataka kuwaulizeni swali hili kabla sijasema jambo hili. Kwa nini tunaenda kanisani? Yote hayo yanahusu nini? Kama hakuna ufufuo wa wafu, kama hakuna ufufuo, basi hebu tule, tunywe, na tushangilie, kwa kuwa sisi si kitu ila magogo, mbwa, na kadhalika, kwa vyovyote vile. Hatuamini hilo. Tunajua ya kwamba kuna Mungu aliye hai. Bila shaka. Vema, kama Yeye ni Mungu aliye hai, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Basi Maneno haya niliyosema, huenda mkakubaliana nami, huenda msikubaliane nami. Lakini ikiwa mnakubaliana nami, basi hata hivyo m—mngali mnaweza kulitilia hilo swali mpaka mlione likidhihirishwa. Hiyo ni kweli. Kama ni Neno la Mungu, Mungu hana budi kulitimiza Neno Lake. Asipolitimiza Hilo, vema, basi si Mungu, basi ni—nimekuwa wa uongo, nimekuwa ninii. . . nilifanya dhihirisho la uongo, ni—nimekuwa nabii wa uongo. Lakini kama Mungu alisema hivyo, Mungu hulitimiza Neno Lake. Basi kama Mungu hulitimiza Neno Lake, Neno moja, unaweza kung'ang'ania basi. Unaweza kuishikilia ahadi yako na kuidumisha. Hiyo ni kweli?

254 Sasa, angalieni, hivi niliwaambia ningeweza kuwaponya? La, bwana. Nisingeweza kuwaambia ningeweza kuwaokoa si zaidi ya mlivyookolewa basi. Ninaamini mmeokolewa. Usingeweza kuinua mkono wako pasipo Mungu kukwambia uuinue. Sasa kuna maji hapa, ambapo mnaweza kubatizwa wakati wowote mtakao. Ukitaka kubatizwa na nanii lako. . . katika kanisa lako mwenyewe, endelea, chochote kile. Hatuna uanachama hapa hata kidogo, mnaona, tunaninii tu—sisi ni kanisa dogo tu hapa. Mchungaji wetu mzuri hapa, Ndugu Neville, alikuwa ni Mmethodisti, naye yupo hapa tu. . . Sisi ni wa baina ya madhehebu. Sisi. . . mtu yeyote amekaribishwa. Tunalo tu kusanyiko linaloingia. Tunahubiri, tunawaombea wagonjwa. Tunaamini katika kuwafanya wanafunzi wa Kristo, sio kuunda chochote. Mnaona? Hatuamini hilo. La, bwana. Sasa, ukitaka kuu-. . . ukitaka dhehebu lako, endelea moja kwa moja. Hilo ni—hilo ni sawa kabisa, bali usilitegemee. Usilitumainie. La, bwana. Nenda kule kwa ajili ya ushirika, lakini wewe mtumainie tu Mungu.

255 Sasa, sasa, hili hapa jambo moja. Ikiwa Kristo angali hai. . .

Sasa, hebu tuchukue Andiko moja dogo tena sasa. Tunataka kuwa na hakika sasa kwamba yote ni shwari kabisa. Jambo dogo nililotaka kusema muda mfupi uliopita, Yeye alisema, “Kizazi kiovu na cha zinaa kinge—kingepata ishara.” Hiyo ilikuwa ni ishara ya Yona, ya ufufuo. Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaoamini kwamba hiyo ni Kweli? Sasa ninataka tu kuona. Hicho kiovu... Mnaamini hiki ni kizazi kiovu, cha zinaa? Vema, ishara ya Yona ingekuwa ni ipi? Ingekuwa ni kufufuka kwa Kristo. Hiyo ni kweli? Kufufuka kwa Kristo, kungekithibitishia kizazi hiki kiovu ya kwamba Kristo angali hai, ambalo, Yeye amekuwa hai sasa kwa miaka elfu mbili, kwa hiyo ingekuwa ni thibitisho la ufufuo.

256 Vema, kunao wengi wetu Waprotestanti kote nchini wasioamini katika ufufuo wa mwili. Mamia ya makanisa hayaamini hilo, kurudi kwa mwili, wala chochote kile. Mnaona? Ninaamini katika kuzaliwa kwa kawaida, kufa, kuzikwa, kufufuka, Kuja kwa Pili, yote Kristo Yesu. Naam, bwana. Ninaamini kwamba Yeye ni Kristo kikamilifu. Yesu yeye yule aliyetwaliwa juu, ndiye Yesu yule yule atakayerudi. Nami ninaamini katika Utu wa Roho Mtakatifu, Yeye yuko hapa sasa, Roho Wake, Uzima Wake ukitenda kazi Kanisani.

257 Sasa, kama hili ni la Kristo... Sasa nitalibinafsisha hili. Ninatumaini ha—hamtalichukulia namna hiyo. Nitalibinafsisha hili sasa, kwa karama iliyotolewa. Ambayo, Hii, huko Washington Nuru hii inaning’inia, hii Nguzo ya Moto ambayo imethibitishwa kwa miaka kadhaa kote ulimwenguni, na kadhalika. Sasa, ikiwa Roho huyo yuko hapa ndani, basi Huyo ataninii... Kama Huyo ni Roho wa Kristo, Yeye atafanya kazi za Kristo. Sasa, hayo ni Maandiko. Na ni kweli. Kama hilo Neno limekuja, basi Neno hili ambalo nimewaambia asubuhi ya leo ni Kweli. Kwa sababu Kristo asingekuja ndani yangu kama...

258 Si—sifanyi—siwadhihaki ninyi Wakatoliki, lakini ninyi mkisema kwamba roho wa Petro ndiye aliyekuwa kanisani mwenu huko nyuma. Mnafikiri Myahudi angeweka sanamu? Mnafikiri Myahudi angemkana Roho Mtakatifu na kufanya kipande kidogo cha mkate kilichowekwa madhabahuni, ambapo vipanya na panya wangeviokota, nanyi mnaendelea mkisema ati huyo ni Mungu? Kuna shida gani? Mnajua huyo si Mungu. Roho Mtakatifu ni Mungu akishuka kutoka Mbinguni, Roho. Unasujudu mbele ya sanamu, ukijaribu kuutazamisha u—uhai uingie katika hiyo. Wewe ndiye sanamu, Mungu humwingiza Roho Wake ndani yako nawe ni mwakilishi Wake aliye hai. Unaona, Mungu yuko ndani yako, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

259 Sasa tutaitisha mstari wa maombi. Ulisema ulisambaza zipi, kutoka moja mpaka hamsini? Hebu tuanze, hebu tuanzie moja. Kwa hiyo unasema nini? Vema, itatubidi tu kuwaita

wachache kwa wakati mmoja, maana ninii zao. . . Hebu tuone, hebu tuwaite kama wanane ama kumi kwa wakati mmoja. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Sasa msininii. . . Ninii tu, simama tu wakati namba yako imeitwa, maana huu si uwanja wa michezo sasa, hili ni kanisa. Vema. Wasemaje? A—A, namba moja. Ni nani aliye nayo? Waweza kuja huku, mama, ama papa hapa mahali fulani? Papa hapa tu, simama papa hapa mbele ya madhabahu. A, namba mbili, ni nani aliye na namba mbili? Kadi ya maombi namba mbili. Sasa, inua mkono wako upesi tupate—tutaninii. . . Vema, nenda papo hapo nyuma ya huyo mama, tafadhali. Namba tatu, namba tatu. Vema, dada, huwezi kusimama, kwa hiyo kaa tu hapo, nami nitakuja nikuombee papo hapo. Namba nne, A, namba nne, inua mkono wako. A, namba nne, namba nne. Huko nyuma kabisa, huko, nyuma kabisa. Vema, mnaona, wanakuja tu chini hapa, na yeyote anayezitaka, wanazichanganya kadi hizi na kuwapa watu namna hii, ambapo mnazihitaji. Hatujui. Vema, namba nne, njoo hapa, mama. Namba tano, ni nani aliye na namba tano? Kadi ya maombi namba tano, naomba uinue mkono wako upesi. Sasa hatuwezi kuchukua muda mwingi sasa, utakosa nafasi yako. Namba tano, namba sita, vema, namba saba.

260 Sasa, hebu tuone, hebu—hebu—hebu—hebu—hebu hao wengine waje. Tunaweza kupata hizi kwa njia hii. Namba nane, kadi ya maombi namba nane, ni nani aliye na namba nane? Wewe ni kadi ya maombi namba nane, mama, unayo nane? Vema. Inua mkono wako ili niweze kukuona, unaona, wakati. Namba tisa, ni nani aliye na namba tisa? Vema, hilo ni jema, mama. Namba kumi, kadi ya maombi namba kumi, ni nani aliye na namba kumi? Waweza kuinua mkono wako, yeyote yule. . . Vema. Samahani. Vema, mtu huyu hapa. Vema, bwana, njoo huku. Namba kumi na moja, namba kumi na moja. Naomba uinue mkono wako, namba kumi na moja.

261 Usipokee kadi isipokuwa utaitumia, enyi marafiki, maana kama wewe—wewe—wewe—wewe—wewe. . . Unaona, ukiamka na kutoka nje, na usitumie kadi yako ya maombi, basi wewe—basi wewe—wewe ni. . . hupaswi kufanya hivyo. Namba kumi na moja, namba kumi na mbili. Vema. Papa hapa, dada, nenda moja kwa moja ukazungukie huko nyuma. Namba kumi na tatu, kuzunguka papo hapo. Namba kumi na nne, namba kumi na tano. Hilo ni jema, hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Namba kumi na sita. Sasa mnalifanya. Namba kumi na saba. Chukueni tu nafasi zenu huko nyuma. Kumi na saba. Hebu tuone tunao wangapi zaidi sasa. Wasemaje? Zunguka upande huo tafadhali, ndugu, kwa kuwa tunachanganyikana hapa. Namba kumi na saba, namba kumi na nane, kumi na tisa, ishirini, ishirini. Vema. Nafikiri hao wametosha papo hapo, ki—kidogo. Hebu tuone jinsi tunavyofika hapa chini mstarini, tutaona. Ishirini, ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na

tano. Sasa hebu tuwashughulikie, tuone ni wangapi huko ndani sasa. Namba ishirini na tano. Nami ninaamini tutasongamana hapa, sivyo? Ishirini na tano, nafikiri, ishirini na tano. Vema, sasa tunao wengine ishirini na watano wanaokuja mara baada ya hili—kundi hili likimalizika. Tunao wengine ishirini na watano wanaokuja. Vema, ishirini na watano.

262 Vema, sasa hebu tuone ni wangapi hapa ndani walio na kadi za maombi. Ni wangapi hapa ndani wasio na kadi za maombi nanyi mngali mnataka Mungu awaponye, inueni mikono yenu. Aminini. Mlio na . . . Hamna kadi za maombi bali unataka Mungu akuponye, inua mkono wako.

263 Sasa, wakati wakiwafanyiza hao mstari, nisikilizeni kwa makini sasa, maana kama ukilikosa hili sasa hu—hutajua la kufanya. Sasa, tutachukua wakati wetu, tuchukue tu wakati wetu. Sasa, msiwe na haraka. Sina budi kutulia, mimi mwenyewe, kwa sababu Roho Mtakatifu katika mambo ya namna hii asingetia mafuta katika njia hiyo.

264 Sasa, ni wangapi katika chumba hiki, ama mstari huu wa maombi waliosimama hapa, wanaojua ya kwamba—ya kwamba . . . Ninawajua baadhi ya hawa watu. Ninaamini ninawajua. Ninajua ninamfahamu mama huyu papa hapa, mama huyu hapa. Yeye huja hapa kanisani, siwezi kulikumbuka jina lake. [Dada huyo anasema, "Baker."—Mh.] Baker, a-ha, ninamfahamu. Sina hakika, sininii . . . Ninaamini jamaa huyu mkubwa mrefu anayesimama papa hapa, ninaamini ninamjua. Sijui jina lake, bali nimemwona hapa.

265 Vema, kwa vyovyote vile, kila mmoja wenu mstarini, na kila mmoja wenu huko kwenye wasikilizaji aliye mgonjwa, anayejua ya kwamba sijui lolote kukuhusu, inua mkono wako, anayejua kwamba simjui. Naam. Mnaona? La. Sijui lolote kukuhusu. Hatufahamiani. Sasa hebu tuuone mstari wa maombi tena, inua mkono wako, unayejua sijui lolote kuhusu shida yako sasa. Vema, vema, vema, karibu tu asilimia mia moja, nafikiri. Vema, na kwenye kusanyiko sasa, sasa inueni mikono yenu, wewe uliye mgonjwa na umeinua mkono wako nawe ungali utasema kwamba mimi . . . "Hanijui mimi wala lolote kunihusu." Mnaona, kunao watu wengi hapa. Mimi huingia na kutoka, nao watu wengine nawajua na wengine siwajui. Mnaona? Na mimi—mimi sijui. Lakini hao ninaowafahamu, nisingejua shida zao.

266 Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani. Sasa endapo . . . Sasa, angalieni, palikuwapo na maskini mwanamke mmoja. Ninyi watu ambao hamtakuwa katika mstari wa maombi, mnaona, ninyi watu ambao hamtakuwa kwenye mstari wa maombi. Sasa, kuna maskini mwanamke mmoja, wakati mmoja, wala hakuwa awe kwenye mstari wa maombi, naye alikuwa akitokwa na damu. Lakini yeye aliamini ya kwamba huyo alikuwa ni Mtu mtauwa. Sasa, sikilizeni kwa makini sasa, msilikose. Yeye

aliamini ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo, naye akasema "Kama nikiweza tu kugusa upindo wa vazi Lake." Sasa, yeye hakuwa na Maandiko yoyote kwa ajili ya hilo, mnaona, si zaidi ya labda kama Eliya alivyochukua. . .ama alivyoichukua fimbo yake na kuiweka juu ya mtoto, ama kitu fulani, mnaona, ama kugusa mifupa ya Eliya akiisha kufa. Lakini aliamini kama alimgusa Yeye angepata kile alichoomba. Akapenya kwenye huo umati na kuunyosha mkono. Sasa, kama mtu yeyote aliwahi kuwa huko Palestina, wanalo vazi la ndani na vazi la juu, nalo linapwaya. Hiyo ndiyo sababu wanatawadha miguu na kadhalika, mavumbi huingia kwenye miguu yao. Ndipo akagusa upindo wa vazi Lake. Sasa, kama aliligusa koti langu, namna *hiyo*, nisingehisi, nalo linaning'inia karibu sana nami. Lakini yeye aligusa chini upindoni, nchani, ambao labda ulikuwa umbali *huo* kutoka miguuni Mwake, ama, mwilini Mwake. Yeye aliugusa upindo wa vazi Lake, kisha akaenda akaketi chini, ama lolote alilofanya. Yesu akasimama.

267 Basi, kumbukeni, umati wote ulikuwa umeweka mikono yao. . . "Aloo, Rabi!" "Nafurahi kukuona!" "Wewe ni Nabii?" "Tu—tuna furaha kukuona." "Loo, Ewe mnafiki!" "Wewe ni Mtu mzuri!" Loo, matamshi mbalimbali tu.

268 Sasa sikilizeni kwa makini. Halafu maskini mwanamke huyu, aliligusa vazi Lake, naye akarudi nyuma kwa sababu aliridhika alikuwa amemgusa Mungu. Yesu akasimama, kasema, "Ni nani aliyenigusa?"

269 Petro akamkemea, kasema, "Wote wanakugusa. Mbona Wewe unasema jambo kama hilo?"

270 Akasema, "Lakini ninaona kwamba nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka." Akaangalia kote juu ya hilo kusanyiko mpaka akampata maskini mwanamke huyo, ndipo Yeye akamwambia kuhusu kutokwa kwake na damu, nako kulikuwa kumekoma. Hiyo ni kweli? Sasa, sasa, sasa shikilieni hilo. Sasa, semeni "amina" kwa hilo, hilo linamaanisha "na iwe hivyo." Sasa, angalieni sasa, hivi Biblia inasema, kwenu Wakristo wasomaji, kwamba Yesu Kristo sasa ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Wangapi wanajua Biblia ilisema hivyo? Vema, kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hivi Yeye si angetenda vile vile alivyotenda basi? Vema, basi, kama ninyi mnaoketi huko nje mngemgusa Yeye huko juu, na kama mimi ni mwakilishi Wake, Sauti Yake hapa sasa, hivi si Yeye angesema jambo lile lile alilosema wakati huo? Hilo si linasikika ni la Kimaandiko? Hiyo si ni kweli? Mnaona? Utajuaje ulimgusa iwapo Yeye hakutenda jinsi ile ile? Mnaona? "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya."

271 Vema, sasa ninyi msio na kadi za maombi, ombeni tu na kusema, "Bwana Yesu, sikufika hapa kwa wakati mzuri kupata kadi ya maombi, bali ni—ninakuomba Wewe, nami

ninaamini yale mtu huyu aliyosema ni Kweli. Kwa hiyo nitaninii . . . Utaniruhusu niliguse vazi Lako, Bwana Yesu? Wewe ndiwe Kuhani wangu Mkuu. Simwangalii maskini mtu huyu mdogo mwenye upara anayesimama hapa juu ya jukwaa. Ninakuangalia Wewe, nami ninakugusa Wewe, nami ninaamini ya kwamba Wewe utanipa afya. Kwa hiyo, ninakugusa Wewe, Wewe nena na Ndugu Branham na ufanye jambo lile lile hapa kama ulilomfanyia mwanamke yule. Nami nitakuamini Wewe kwa moyo wangu wote." Mtafanya hivyo? Ni wangapi watakaofanya hivyo, inua mkono wako, useme, "Ni—nitafanya hivyo." Vema, ninyi ombeni tu. Sasa hapa ndipo mahali pa kuiweka imani yako kazini. Liamini, usilishuku. Wewe amini hilo kwa moyo wako wote. Amina.

272 Halafu ninyi mlio kwenye mstari wa maombi, sasa ni . . . Mtu wa kwanza ni nani? Njoo papa hapa tu kwa dakika moja. Sasa, simama tu papo hapo. Hilo—hilo ni zuri vya kutosha, mnaona, simama papo hapo. Ninaamini, muda mfupi uliopita, uliinua mkono wako, sikukujua. Hiyo ni kweli. Hatufahamiani. Vema.

273 Sasa ninataka kuliuliza kusanyiko hili jambo fulani. Hii hapa mikono yangu imeinuliwa mbele za Mungu, naye aliinua mkono wake kwamba hatufahamiani. Sasa, hii si ni picha ya Biblia ya Yohana Mtakatifu 4, wakati Yesu alipokutana na mwanamke kisimani? Mwanamume na mwanamke walikutana kwa mara ya kwanza. Naye Yesu alifanya nini? Akaanza kuzungumza naye. Alikuwa akifanya nini? Sasa, Yeye alisema, "Baba . . . "

274 Alihitaji kwenda mpaka Yerusalemu, au mpaka Samaria. Sasa, mnaona, Wa—Wayahudi walikuwa wameiona ile ishara, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Nabii na Yeye alionyesha ishara ya nabii. Na kuna—kuna jamii tatu tu za watu, hizo ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Sasa, Wayahudi walikuwa wameiona ishara yao, maana walikuwa wakimtazamia Masihi. Wakaiona. Sasa Wasamaria hawana budi kuiona, kwa sababu walikuwa wakimtazamia Masihi.

275 Sio Wamataifa, si hata wakati mmoja aliowahi kufanya hilo juu ya Mmataifa, bali Yeye alitabiri, "Katika siku za mwisho," kama Yeye alivyofanya, "kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu na katika siku za Lutu," wakati Malaika huyo alipokuja akazungumza na Lutu, akamwambia Sara aliyofanya hemani nyuma Yake. Yesu alisema hilo lingejirudia tena katika siku za mwisho. Ni wangapi wasomaji wa Biblia wanaojua hilo? Mnaona, kweli. Mnaona? Sasa tuko katika siku za mwisho, ni wakati wa Mataifa. Kama Yeye . . . Mnaona, nilisema hapo mwanzoni mwa somo langu, kama Mungu akifanya lolote, akijitambulisha wakati mmoja, Yeye hana budi kudumu hivyo.

276 Kwa hiyo Nathanaeli alijuaje—alijuaje Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu? Kwa sababu Yeye alimwambia mahali

alipokuwa, jambo fulani kumhusu.

277 Mwanamke huyu alijuaje? Angalieni, hebu tuchukue mazungumzo yake, tuone ni mengi—mengi zaidi vipi aliyojua kulihusu kuliko hao wahubiri wote huko chini. Yeye alitoka akaenda huko. Huenda alikuwa ni mwanamke mrembo. Alikuwa akienda kuchota ndoo ya maji. Akaivuta ile ndoo ya maji. Yeye alikuwa ni Myahudi, mwanamke huyu alikuwa ni—ni Msamaria. Na kwa hiyo, akaivuta ile ndoo ya maji, na huko kwenye maskini hayo mandhari mahali kilipo kile kisima. Kingali kule Sikari. Kwa hiyo basi Yeye alikuwa ameketi pale namna hiyo, Yeye akasema, "Mwanamke, nipe maji ninywe." Akageuka. Sasa, yeye alikuwa ni mwanamke mwenye sifa mbaya, mwajua, alikuwa ameolewa mara nyingi kupita kiasi. Akasema, "Nipe maji ninywe." Yeye . . .

278 Akasema, "Si kawaida kwenu Wayahudi kumwomba mwanamke Msamaria kitu kama hicho."

279 Hayo mazungumzo, mnaona. Baba alikuwa amemtuma huko juu. Sasa kumbukeni, Yeye hakufanya lolote hata Baba alipomwonyesha. Mnaona? Kwa hiyo sasa akaketi pale, kwa hiyo Yeye alikuwa akifanya nini? Alikuwa akijaribu kuona shida yake ilikuwa ni ipi, ili aweze kuupeleka ujumbe kwa watu hao. Kasema . . . Alitaka kupata tatizo lake, mwajua. Kasema, "Nipe maji ninywe."

Akasema, "Si kawaida."

280 Akasema, "Lakini kama ulijua ni Nani uliyekuwa ukisema naye, ungeniomba Mimi maji unywe."

281 Akasema, "Vema, kisima ni kirefu, Wewe huna kitu cha kuchotea. Ungewezaje kupata maji kutoka hapa?"

282 Naye akaendelea kuzungumza, mazungumzo yakatokea, kuhusu kuabudia Yerusalemu. Alikuwa akifanya nini? Alikuwa akijaribu kuipata roho yake, aone tatizo lilikuwa ni lipi. Akalipata. Mnajua ilikuwa ni nini? Alikuwa na waume watano. Na Yeye akasema, "Nenda kamwite mume wako mje naye hapa."

Mwanamke akasema, "Sina mume yeyote."

283 Kasema, "Umesema vizuri, umesema vizuri, kwa kuwa umekuwa na watano naye unayeishi naye sasa siye mume wako."

284 Sasa angalia. Sasa, hakusema, "Yeye ni mpiga ramli," kama hao wahubiri walivyofanya. Hakusema, "Yeye ni Beelizebuli." Alisema, "Bwana," sikilizeni, "naona kwamba Wewe ni Nabii. Tunajua Masihi ajapo Yeye atatwambia mambo haya." Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi.

Yesu alisema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye."

285 Akakimbia mjini, na kusema, "Njoni mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu ndiye Masihi?"

286 Vema, kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi kwa Wayahudi, kwa Wasamaria, hivi si ingekuwa ni ishara ya Masihi kwa Wamataifa? Hivi Masihi basi, kama Yeye amefufuka katika wafu na yuaishi Kanisani Mwake, akijidhihirisha Mwenyewe, hivi Yeye si angefanya kazi zile zile wakati Yeye aliahidi angezifanya?

287 Sasa mimi nikisimama hapa nikikuzungumzia, sikujui, kamwe sijawahi kukuona maishani mwangu. Unaona? Lakini kama Bwana Mungu ataniambia jambo fulani ambalo limekuleta hapa, unajua kama ni kweli ama si kweli. Unaona, aniambie jambo fulani ambalo umefanya, jambo ambalo hukupaswa kufanya. Iwapo Yeye anaweza kukwambia yale umefanya wakati uliopita, hakika angejua ya usoni yalikuwa nini. Hiyo ni kweli, kama Yeye angeweza kukwambia hilo? Hakika. Na kama ataniambia sababu ya wewe kuwa hapa, ungemwamini kuwa ni Mwana wa Mungu, uliamini? Ni wangapi kwenye kusanyiko wataamini hilo? Nami pamoja na mwanamke huyu hapa huku mikono yetu ikiwa juu, ha—hatuninii. . .sisi, mnaona, hatufahamiani. Sina fununu, unajua sina. Umesimama hapo, mgeni tu kwangu. Lakini kama Bwana Mungu. . . Ninakuzungumzia nipate kumfanya Roho aanze kuwatia watu mafuta, unaona, kisha ataingia tu moja kwa moja. Nami ni—ninakuangalia tu nione kile Yeye atakachoniambia, maana sijui lolote kulihusu. Lakini kama Yeye atakwambia jambo fulani, basi wewe utajua kama ni kweli ama si kweli, sivyo? Kila mtu ataamini, kama Yeye atafanya hivyo?

288 Baba yetu wa Mbinguni, siwezi kufanya la zaidi sasa. Ni kufikia wakati huu, itakuhitaji Wewe tangu sasa na kuendelea, Bwana. Nimewaleta watu kwenye Neno Lako. Hayo ndiyo yote nijuayo. Umeahidi mambo haya. Nayo ingechukua majuma na majuma, tungali tungekuwa kwenye hiyo, tukizisimulia ahadi Zako za mambo haya kwa ajili ya siku za mwisho. Kama vile tumekuwa nyakati hizi zote kote ulimwenguni, Wewe kamwe hujatupungukia, Bwana. Sasa hapa linasimama kusanyiko la watu. Ninajua ya kwamba moja ya maono haya litatudhoofisha. Ninatambua hilo. Nguvu zilikutoka Wewe, Mwana wa Mungu, Mwana wa Mungu asiyeghoshiwa. Ni zaidi sana vipi itakavyokuwa kwangu, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yako?

289 Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utaliruhusu litukie sasa, kwamba Ujumbe huu asubuhi ya leo usiende pasipo kuzaa matunda, lakini hawa waongofu wachanga, labda ishirini ama thelathini wao ambao ndio kwanza wakuinulie Wewe mikono yao, kwamba wataridhika, Bwana, kwamba Mungu wao amefufuka katika wafu na Yeye yu hai milele, akijitambulisha Mwenyewe, Mungu yeye yule anayezijua siri za moyo, na aliahidi katika siku za mwisho lingetukia tena. Sisi hapa, mwisho wa wakati. Nao Wamataifa wamekuwa na miaka elfu mbili, kama

tu vile Wayahudi walivyokuwa nayo, kujifunza kutoka kwa Mungu, na sasa wanapata ishara ile ile na kuikataa Hiyo kama tu Wayahudi walivyofanya. Wayahudi walimkataa Masihi wao, maana waliyaundia yote madhehebu. Ndivyo nao wamefanya leo hii, Bwana, wamefanya jambo lile lile. Lakini hatuwezi kudhamini hilo. Tunapaswa tu kushuhudia, Bwana. Ni kama tu kondoo, yeye hatengenezi chochote, huzaa sufu kwa kuwa yeye ni kondoo. Na, Bwana Mungu, jalia tumzae Roho wa Mungu, kwa kuwa sisi ni Wakristo. Tunakuamini Wewe. Tunamwamini Mwana wa Mungu. Sasa, Bwana, mimi sistahili, bali chukua . . . Ni nani anayestahili? Ni nani anayestahili, Bwana? Hakuna mmoja wetu. Sote tumezaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja ulimwenguni tukisema uongo. Tusamehe uovu we—wetu, Bwana. Na sasa tutumie katika siku hizi za mwisho ambapo unaishughulikia jamii ya binadamu. Katika Jina la Yesu. Amina.

290 Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho chini hapa, hapa ndani, chini ya mamlaka yangu. Mnaona? Sasa iweni na kicho. Pasipo kukujua wewe, bila kujua lolote kukuhusu. Ni karama. Jinsi tu unavyojivuta mwenyewe, mbele za Mungu, unajifanya tupu. Hebu Yeye ashughulike na kuangalia. Sijui, bali ninajua Yeye yupo hapa. Ninajua Yeye amesimama hapa. Naam, mama, hili hapa tatizo lako. Unataka maombi kwa ajili ya kansa. Kansa hiyo iko usoni mwako; haionekani, kitu kama hicho, bali iko juu karibu na jicho lako. Hiyo ni kweli, inua mkono wako.

291 Nililihisi hilo likija moja kwa moja kutoka huko kwenye kusanyiko, ulisema, "Yeye alibahatisha hayo ama aliiangalia kwenye uso." Sikufanya hivyo. Simama kimya. Hebu mimi . . . Shetani, umekosea. Simama kimya, dada. Ukimwachilia aanze, kama akianza, basi atavuruga kila kitu. Tunamkemea ibilisi huyo, katika Jina la Yesu Kristo, na kumwaibisha.

292 Una matatizo zaidi ya hilo. Una ugonjwa wa moyo, pia. Magonjwa ya ziada, magonjwa yote tu ya wasiwasi, umekuwa hivyo kwa miaka kadhaa. Hiyo ni kweli kabisa, uchovu, hisia za huzuni, na kila kitu. Hiyo ni . . . Iwapo hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa umeponywa. Imani yako imekuokoa. Unaweza kwenda nyumbani sasa ukapate afya. Yote yamekwisha. Nenda tu, ukiamini, yote yakupasayo kufanya. Mshukuru Mungu.

293 Unaamini? Simama tu papo hapo, mama, angalia huku. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo? [Dada anasema, "Naam, Yeye anaweza."—Mh.] Vema, Yeye ameuponya wako, basi, kama utaamini. Nenda, amini.

294 Unaamini Yeye aliponya kansa? Basi rudi kitini mwako, useme, "Asante, Bwana Yesu."

295 Vipi kama sikusema neno moja kwako bali kuninii tu . . . Ungeamini kama nilisema uliponywa wakati ulipokuja pale

mstarini? Ungeliamini neno langu kwa ajili yake? Umeponywa, na hakuna haja ya kukwambia hili, tayari umeponywa. Sijamgusa mtu.

296 Hutaninii, haitakubidi kufanyiwa upasuaji ikiwa utamwamini Mungu. Unaamini kwa moyo wako wote? Hicho kivimbe kimekwisha. Nenda nyumbani nawe utapata afya.

297 Angalia huku, dada. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Hebu kidogo. Sasa, kunaye mtu anayeendelea kujitokeza mbele yangu hapa, anacho kitu kile kile alicho nacho mwanamke huyu, mahali fulani katika kusanyiko. Pia angalia ile Nuru kwenye picha, Ambayo inasimama papa hapa. Hivi hamwezi kuiona hiyo? Ni mtu huyu anayeketi papa hapa. Una kadi ya maombi, bwana? Jamaa mdogo, ninaamini wewe ni Ndugu Hupp, sivyo? Ndiyo kwanza nikutambue. Si—sijui shida yako ni nini, Ndugu Hupp. Unajua sijui. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Unayo shida. Ulikuwa umeketi pale, ukiamini. Unapaswa kuamini kwa ajili ya binti yako hapa hivi majuzi. Unaamini, sivyo? Mwanamke huyu ana baridi yabisi; unayo, pia. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Aminini kwa moyo wenu wote nanyi nyote wawili mnaweza kuponywa. Mungu awabariki. Shetani alidhani angeponyoka na mtu huyo, akalikosa. Kuwa na imani sasa. Usitie shaka. Sasa, mtu huyu hapa, nanii. . .Ndugu Hupp, huna kadi ya maombi, sivyo, Ndugu Hupp? Naam, umeketi tu hapo, ukiamini. Angalia kitakachokupata. Amini tu sasa kwa moyo wako wote.

298 Kila mmoja katika maombi. Mnaamini sasa? Sasa, mnatambua mambo haya hunifanya tu dhaifu sana hata ninaninii tu. . .

299 Unaamini kwa moyo wako? Kama ningekwambia utakuwa mzima, unge—ungeliamini neno langu kwa ajili yake na kuliamini? Basi nenda na Yesu Kristo akupe afya. Amini kwa moyo wako wote.

300 Unafikiri kwamba Mungu anaweza kuuponya wasiwasi na kukufanya mzima? Nenda, amini hilo. Ninaamini mimi. . . sina hakika, nilidhani nilimfahamu mwanamke huyo. Sikuwa na hakika. Ono lilitokea juu yake lakini ni—nikalisimamisha, niliangalia tu upande mwingine; maana ninaamini ni—nilimfahamu huyo mwanamke, bali si—sikuwa na hakika.

301 Sasa iweni na kicho, kila mtu. Mnaamini? Mnaona, ninao mstari mkubwa mrefu wa maombi hapa, sitaki. . .Simameni tu. Na, sasa hivi, nimewahubiria kwa yapata saa mbili ama tatu, lakini sasa hivi mimi ni dhaifu maradufu kadiri nilivyokuwa na hayo mahubiri yote. Mnaona, linaunyonya tu uhai wangu. Lakini, hawa, tungeweza kuendelea kuwazungumzia watu, hilo lingekuwa ni sawa, hilo halileti tofauti yoyote. Unaweza kusimama, uwazungumzie watu muda mrefu utakao, mengine mengi yanaendelea kutukia, lakini nilisimama nipate kuziokoa

nguvu zangu kidogo kwa ajili ya hao wengine wanaokuja mstarini. Mnaona ninalomaanisha? Ni wangapi wameliona ambapo mara nyingi ninasimama na kuzungumza na watu, Hilo huwaambia yote kuwahusu, na kwamba wao ni nani na mahali wanakotoka? Jamani, mmekuwa mikutanoni na kuliona, mwajua.

302 Huyu—huyu afuataye, wewe ndiye unayefuata? Vema, bwana, unaamini kwa moyo wako wote? Vema, sawa. Sisi ni waaminio, tunaamini kwa moyo wetu wote. Na bila kukujua, Bwana Yesu angeniambia jambo fulani lililo shida yako, ungejua kama lilikuwa ni kweli ama la, sivyo, bwana? Naam, bwana. Hii ikiwa ni ninii yetu. . . Nadhani hatufahamiani. Siukumbuki uso wako. Sisi ni wahudumu pamoja, nasi ni. . . lakini hatufahamiani kibinafsi tu kama marafiki. Vema, bwana. Basi angalia huku, bwana, nawe uniamini kuwa ni mtumishi wa Kristo kwa moyo wako wote. Vema, bwana. Mtu huyu anaugua ugonjwa wa utumbo mpana. Uko katika utumbo wake mpana. Pia ni ugonjwa wa moyo ulio nao. Wewe ni mhudumu, hiyo ni kweli, wewe ni wa Kanisa la Muungano wa Ndugu. Umetoka Ramsey, Indiana. Jina lako ni Bw. Beanblossom. Kasisi Beanblossom, hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Basi nenda nyumbani na uwe mzima, bwana. Yesu Kristo anakuponya. Amini kwa moyo wako wote.

303 Baridi yabisi si kazi kwa Mungu. Unaamini Yeye anaweza kukuponya? Unaamini Yeye atakuponya? Nenda ukamwamini Yeye kwa moyo wako wote nawe unaweza kuipata kwa ninii yote. . . amini tu kwa ninii yote. . .

304 Ndugu, ninakujua, ninajua ugonjwa wako. Utaamini sasa hivi, wakati nikiwa chini ya upako wa Roho Mtakatifu, kwamba Mungu atakuponya na kukupa afya? Nenda ukaliamini, Ndugu Collins, na upate afya. Vema.

305 Mimi—mimi. . . ilionekana kama nilikuona, bali sina hakika. Lakini kama Mungu ataniambia shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama mtumishi Wa—Wake? Unaamini hilo? Vema. Unaugua ugonjwa wa wasiwasi. Huo ndio unaotaka uombewe. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Nenda nyumbani, upate afya. Amini. Endesha juu yake sasa. Iweni na ile imani ndogo ambayo kweli huuponya.

306 Unaamini Kristo atakuponya sasa hivi wakati umesimama hapo? Liamini, kisha uende nyumbani na kusema, "Yesu Kristo ananipa afya sasa hivi." Amini kwa moyo wako wote. Huna budi kuamini, upate kuishi. Unajua hilo, sivyo, dada? Kama huamini, huna budi kufa. Unajua hilo. Lakini Yeye huponya kila namna ya magonjwa, kansa, chochote kingine, na kukupa afya. Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Basi nenda zako na uamini kwa moyo wako wote, na upate afya, katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

307 Vema, ndugu, unajua ninakujua, na kwa hiyo ninajaribu tu kushika, hata hivyo. Lakini unaamini kwamba Yesu Kristo atakuponya sasa hivi wakati ukiwa chini ya upako wa Kiungu wa Roho Mtakatifu? Nenda ukaamini kwa moyo wako wote.

308 Sasa ni nini? Vema. Hebu kidogo tu sasa. Nilisimamia wapi, nilisimamia wapi muda mfupi uliopita? Ishirini na tano, ishirini na sita, ishirini na saba, ishirini na nane, ishirini na tisa, thelathini, pandeni moja kwa moja mwingie mstarini. Thelathini, thelathini na moja, thelathini na mbili, thelathini na tatu, thelathini na nne, thelathini na tano, thelathini na sita, thelathini na saba, kuendelea hadi hamsini, pangeni mstari hapo sasa, wale mlio na kadi zenu za maombi, ili mzikabidhi kwa bawabu ama ndugu wanapopita.

309 Sasa hebu tuchukue muda mfupi wa kupumzika, kidogo tu. Je, mnaamini? Mambo yote yawezekana, amini tu.

310 Ndugu na Dada Spencer, niliwajua tangu nilipokuwa mtoto mdogo. Ninajua tatizo lenu ni nini, nami ninajua ni kwa nini mnasimama hapo. Mnaamini Yesu Kristo atawaponya, mkisimama hapo? Ee Mungu wa Mbinguni, zijalie baraka Zako juu ya hawa mume na mke wakongwe, ukiwajalia wapate kuwa wazima, Baba. Mbali sana katika miaka hapa, bali wangali wanakutumikia Wewe. Ninawabariki katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina. Rudini kwenye ninii yenu. . .Mungu akubariki, dada. Yeye atachukua themanini na mitatu, unayo miaka zaidi ijayo, amini kwa moyo wako wote na Mungu awe pamoja nawe. Nawe, pia, Ndugu Jess. Mungu akubariki hapa.

311 Unaamini sasa kwa moyo wako wote? Ngoja, ninaamini nimemkosa maskini dada huyu hapa chini. Vema. Tunayo machela mawili, inatupasa kuwafikia katika dakika moja tu. Hujali kungojea kwa dakika moja tu, dada hapo, ama yeyote yule aliye mtu huyo mwingine?

312 Sasa iweni na kicho kabisa na msimame kimya, kila mtu awe na kicho. Mnaona, hamna budi kuwa na kicho sana, sana. Sasa hebu tupumzike kwa muda kidogo tu, mnaona, kutokana na maono, sekunde moja tu. Na mwe na kicho kabisa. Sasa kila mtu aangalie huku, na hebu tuimbe kwa utulivu, *Amini Tu,* sasa. Sote pamoja sasa. (Hebu mimi.)

Amini tu, amini tu,
Yote yawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Yote yawezekana, amini tu.

313 Sasa, yeye aliniomba niende nikawaombee sasa, lakini kwa namna fulani nimetulia kidogo tu sasa. Hebu nianzishe mstari tena, katika dakika moja nitasimama. Sasa, wako wapi watu watakaoombewa, mama yule pale kitini? Vema, hebu kidogo, nita—nitafika. . .nitakuja alipo, mnaona, kwa dakika moja. Vema, hebu kidogo. Sasa, kila mtu awe na kicho kabisa. Nina

hakika kabisa mna—mnatambua yale niliyo chini yake hapa. Mnaona? Sio hapa tu, bali, katika nchi za kigeni, wakati mwingine maelfu mara maelfu.

314 Nilisikia kidogo, nilihisi chuki kidogo muda mfupi uliopita, juu ya kuitwa kwa jina la mtu fulani. Hivi hamtambui ya kwamba Yesu analijua jina lako? Hamjaona hilo? Hapana budi pana wageni hapa ndani, hawajaliona. Mbona, jamani, wakati mwingine ni hapa jukwaani Yeye huwaambia watu dhambi zao zote, na kuzichimbua zote. Mnajua hivyo. Kila...Hivi Yesu hakumwambia Petro, "Jina lako ni Simoni. Jina la baba yako lilikuwa ni Yona. Mwana wa Yona"? Mnaona? Kuonyesha tu kwamba Yeye yupo hapa. Sasa, mtu yeyote anajua, kila mtu hapa hana budi kusema ya kwamba kuna namna fulani ya Roho anayefanya hivyo. Sasa, unaweza kusema, "Ni Beelizebuli," ama unaweza kusema, "Kristo." Mungu atahukumu chochote kilicho. Mnaona? Ninawaambia ya kwamba hiyo ni ahadi ya Biblia, Biblia Takatifu ya Mungu hapa huipa ahadi.

315 Sasa, sasa iweni na kicho kabisa. Sasa, hebu kidogo. Huyu ndiye mtu anayefuata? Vema, tokea upande huu, bwana. Simjui mtu huyu. Mungu anamjua. Lakini, bwana, kama Mungu ataniambia kile kilichokuleta hapa, vema, lingekufanya uamini. Sivyo? Hakika lingekufanya. Ni wengine wangapi huko nje lingewafanya kuamini? Hawa hapa watu wawili wakikutana, huyu mtu ana umri mdogo kuliko nilivyo mimi. Mungu amemlisha maisha yake yote. Amesimama hapo huku ameyafunga macho yake. Lakini kama Mungu atanifunulia kile kilichomleta mtu huyu hapa, ama jambo fulani kulihusu, linapaswa kumfanya kila mmoja wenu kuamini kwa moyo wenu wote. Sivyo?

316 Hapa, hebu kidogo, papa hapa nyuma, akiketi kwenye hii safu moja kwa moja nyuma hapa, pana mtu, anaomba. Ana kitu cha kipekee sana. Ninaona kimulimuli. Naam, amepigwa na radi. Naam. Kuwa na imani, ndugu yangu. Mimi ni mgeni kwako, bwana. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, hatufahamiani. Mungu anakujua. Kuwa na imani sasa.

317 Sasa unasema, "Unafanya nini, Ndugu Branham?" Ninaiangalia ile Nuru. Inasonga.

318 Matatizo ya kibofu, unayeketi hapo ukiombea...ukiwa na ugonjwa wa kibofu, mtu anayeniangalia. Hatufahamiani, sivyo? Niambieni kile mtu huyo aligusa. Ugonjwa wako wa kibofu umekwisha, bwana. Aligusa nini? Yuko futi thelathini kutoka kwangu. Alimgusa Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na hisia.

319 Mtu huyo anayeketi karibu nawe, yeye anaomba, pia. Hivi ndivyo anavyoomba, "Bwana, jalia niwe wa pili." Amesema hivyo sasa hivi. Hiyo ni kweli. Nilijuaje kile unachoombea? Yeye ayajibuye maombi. Hiyo ngiri unayoombea, hiyo ndiyo uliyo

nayo, ngiri. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema, kama ukiamini kwa moyo wako wote, kitu hicho kitapona.

320 Ninaipa changamoto imani yenu. Katika Jina la Yesu Kristo, amininі! Loo, jamani, ni hisia ya jinsi gani! Yeye yupo hapa. Naam. Sasa hebu litukie. Sasa mtaona Bosi ni Nani. Yeye ndiye Bosi. Hebu kafiri aseme jambo fulani sasa, asiyeamini. Bwana Yesu Kristo, kuwathibitishia kwamba wakati wa mwisho upo hapa, huyo ni Roho Wake juu yangu. Huyo ni Yeye. Si mimi, mimi siwajui. Ni Yeye. Aminini tu kwa moyo wenu wote.

321 Mtu huyu, ninaamini ambaye alikuwa ndiye anayefuata, mtu huyu hapa. Bwana, mimi ni—inanibidi tu kuangalia jinsi Hiyo inavyoenda. Sikujui. Kama Mungu atanifunulia kile kilichokuleta hapa, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, mtumishi Wake? Wewe ni shujaa. Umesimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine, hiyo ni kweli, anahudhuria kanisa pamoja nawe, vidonda. Hiyo ni kweli. Wewe hutoki hapa. Hapa si nyumbani kwenu. Umetoka mbali sana. Unaamini Yeye anaweza kuniambia unakotoka? Missouri. Hiyo ni kweli kabisa. Bw. Friels, sasa kama unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kwenda nyumbani ukapate afya, na mambo yako mengine yote unayoombea. Nenda ukamwamini Bwana Yesu Kristo.

322 Unaamini? Inaonekana kana kwamba ninapaswa kukujua. Nimekutazama mahali fulani. Loo, ninakujua, ninajua mahali ulipokuwa. Wewe ni . . . Sasa, ngoja kidogo. Sijarukwa na akili, bali huu ni upako. Wewe ni . . . Sasa, ngoja kidogo. Uliponywa huko Louisville, Kentucky, ama dada yako aliponywa. Wewe ni . . . Hupp, msichana wa Dada Hupp. Hiyo ni kweli. Unaamini kwa moyo wako wote, kuponywa kama dada yako alivyoponywa? Nenda nyumbani, uupokee, Yesu Kristo anakupa afya.

323 Ndugu, amini wasiwasi huo umeondoka kabisa, na uende tu nyumbani, useme, "Asante, Bwana Yesu, ninaenda nyumbani, nikaponywe." Na Yeye atalifanya.

324 Je, unaamini kwa moyo wako wote, bwana? Vipi kama ningeshuka chini na kukuwekea mikono, pamoja na upako huu? Unaamini lingekuwa, lingetukia kwako? Nitashuka nije nifanye hivyo, katika Jina la Yesu Kristo. Utakufa umelala hapo, wewe ni mahututi sana, sana, hakuna kitu kinachoweza kufanywa. Una maji mapafuni mwako. Hiyo ni kweli. Utakufa umelala hapo, hakika kabisa. Sasa, kwa nini usimwamini tu Yeye kwa moyo wako wote? Simama, katika Jina la Yesu . . .? . . .

[Ndugu Branham anawaombea watu kadha, mengi ya maneno yake hayatambulikani—Mh.] Mungu, tujalie hayo. Yeye aliyasikia maombi yangu katika Jina la Yesu. Mungu, tujalie hayo.

Usinipite, Ee mnyenyekevu . . .

325 Ombeni, kila mtu, sasa, wote pamoja, tutaweka mikono. Upako wa Roho Mtakatifu upo hapa, nitawawekea watu mikono. Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Vema.

[Ndugu Branham anaendelea kuwaombea watu, mengi ya maneno yake hayatambulikani—Mh.] . . .?. . . Toka ndani yake, Shetani, katika Jina la Yesu Kristo. . .?. . . Katika Jina la Bwana Yesu. . .?. . . Katika Jina la Bwana Yesu. . .?. . . Baba wa Mbinguni. . .?. . .

326 Hebu tuombe sasa kwa ajili ya vitambaa hivi hapa. Baba yetu wa Mbinguni, walichukua kutoka kwa mwili wa Mtakatifu Paulo, leso, ama nguo, na Hilo lilisema kwamba "Pepo wachafu wakawatoka." Tunatambua kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, bali tunajua ya kwamba Wewe ungali Yesu yeye yule, kwa kuwa Wewe ni hai leo hii kadiri ulivyokuwa katika siku za Mtakatifu Paulo. Ninaziombea haja hizi, Bwana, ambazo leso hizi zinawakilisha. Vitambaa vidogo na leso, na vijibuti vidogo kwa ajili ya watoto wachanga. Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe utalijalia.

327 Tunafundishwa ya kwamba Israeli waikuwa wakitembea taratibu kwenda kwenye nchi ya ahadi, Nguzo kuu ya Moto iliwatangulia, nabii aliwawakilisha, alimwakilisha Mungu, kwa ajili yao duniani. Nao. . . nabii huyu akawaongoza hata kwenye Bahari ya Chumvi, nayo ikafunga barabara. Kulikuwa na kizuizi fulani njiani wakati wakitembea kwenye jukumu lao. Mungu aliangalia chini kutoka Mbinguni kupitia kwa Nguzo hiyo ya Moto, nayo bahari ikaogopa, na ikarudi nyuma na kuifungua barabara kupitia baharini, Israeli wapate kuendelea kwenye wajibu wao, nao wakaenda kwenye nchi ya ahadi.

328 Mungu, wakati leso hizi zitakapowekwa juu ya wagonjwa na wanaoteseka. . . Shetani amevuka mpaka wao, anawazuia kuingia kwenye wajibu wao. Jalia Nguvu zilizomfufua Bwana wetu, Yule aliyepo sasa, aje juu ya leso hizi. Na, popote zitakapowagusa wagonjwa, jalia ibilisi aogope, wakati Yeye akiangalia chini kupitia kwa Damu ya Yesu Kristo, na jalia kila mmoja wao aponywe na aendelee kwenye wajibu wake. Tujalie, Bwana. Tunakushukuru Wewe. Uwepo Wako upo hapa. Loo, upako huu adhimu wa Roho Wako unaotutikisa sisi wanadamu, Bwana. Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya wema Wako! Wabariki hawa sasa, katika Jina la Yesu.

329 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kila mtu humu ndani. Sio tu kuviinamisha vichwa vyenu, sasa nitawaomba mwinamishe mioyo yenu pamoja navyo. Mungu angeweza kufanya nini zaidi kuwafanya mwone ya kwamba Yeye yupo hapa? Sasa aminini nisemayo. Upako huu ni mwingi sana sasa hivi mpaka karibu ninasinzia hapa. Mimi si shupavu wa dini. Mnajua sivyo nilivyo. Sifanyi mazingaombwe. Ninawaambia tu yaliyo kweli. Ni ya Kimaandiko. Hiyo Nuru kwa kweli

imesambaa kote, inaonekana kana kwamba Hiyo iko tu kila mahali huku. Hitaji kuu jinsi hii! Niaminini.

330 Biblia ilisema, katika Marko 16, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Ni waaminio wangapi waliopo hapa, semeni "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kusudi mjue sio mimi, ninyi mko ndani yake kadiri nilivyo mimi. Hii ni karama tu kutoka kwa Mungu, kumdhihirisha Yeye, inataja mambo. Nami ninamshuhudia yeyote, kote katika miaka, hivi Hiyo imepata kusema lolote ila lile lililotimia vivyo hivyo hasa? Kweli kabisa, kila wakati. Ha—haina budi kuwa, kwa sababu ni Mungu. Sasa, kidogo usitazame kule nusu, kutazama kitu fulani huko ng'ambo mbali sana. Tazama, Yeye yupo hapa sasa, sasa hivi!

331 Sasa, ikiwa wewe ni mwaminio, weka mkono wako juu ya mtu aliye karibu nawe, nao wataweka mkono wao juu yako. Usijiombee mwenyewe, wewe waombee kwa sababu watakuwa wakikuombea. Sasa kusudi mpate kujua, na—na kama mtafanya jambo hili, nitawahakikishia. Vema, hakuna machela yoyote ama vitanda vya wagonjwa vilivyosalia, vyote vimetoweka. Lakini mmekuwa hapa wakati machela na vitanda vya wagonjwa vilikuwa vimewekwa hapa, walemavu, viwete, waliopooza, vipofu, hapana wakati mmoja ila kila kimoja cha hivyo. Sasa, jinsi mnavyoomba kanisani, ikiwa wewe ni Mmethodisti, omba kama Wamethodisti wafanyavyo. Kama wewe ni Mbaptisti, omba kama Wabaptisti wafanyavyo. Kama wewe ni Mpentekoste, omba kama wao wafanyavyo. Chochote ulicho, omba. Lakini wewe mwombee mtu uliyemwekea mikono. Kisha uamini.

332 Sasa, kumbukeni, Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa ninyi ombeaneni, kama watu binafsi. Nitawaombea, kwa jumla, kutoka jukwaani. Sasa, kila mmoja katika njia yako mwenyewe.

333 Baba yetu wa Mbinguni, tunazikaribia rehema Zako. Tusingekuja katika jina letu wenyewe, hatujapewa ahadi kwa hilo. Lakini tumepewa ahadi na Mwana Wako Mwenyewe mpendwa, kwamba, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Hiyo ilikuwa ndiyo ahadi Yako. Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utajidhihirisha Mwenyewe pamoja na waaminio hawa. Wameweka mikono yao juu ya wagonjwa, mmoja kwa mwingine, nasi tunakuja sasa kwenye kiti cha enzi cha Mungu, tukiwaleta. Katika Biblia, katika Marko, mlango wa 11, kifungu cha 23, inasema, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako. Mkikaa ndani Yangu nayo Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtajaliwa."

334 Sasa, Baba, katika kila kanuni ya Neno Lako, nimelikubali Hilo haidhuru wengine wanasema nini. Nimeliamini Hilo jinsi tu lilivyoandikwa. Kwa kuwa Hilo si la kufasiriwa apendavyo mtu yeyote, tunaambiwa, lakini jinsi tu Hilo lilivyoandikwa. Kama Wewe utatuhukumu kwa Kitabu hiki, bila shaka ulihakikisha kwamba Hicho kimetujia katika hali nzuri, kwa sababu tunapaswa kuhukumiwa kwa Kitabu. Na sasa, Baba, ninaamini kwa moyo wangu wote, na hata zaidi ya karama ya Roho wa unabii ambayo Wewe unaijulisha. Na hiyo ndiyo sababu ninajua kwamba Hiyo ni Wewe, kwa maana sikuzote Hiyo inalingana kabisa na Maandiko. Sasa tunakuja, Bwana, na kukushukuru Wewe kwa ajili Yake. Basi tutie mafuta sasa. Tunakaribia maeneo ya adui.

335 Ee Shetani, wewe ni kiumbe kilichoshindwa. Huna nguvu. Mwana wa Mungu amezichukua nguvu zako, akakunyang'anya kila kitu ulichokuwa nacho, pale Kalvari; akathibitisha kwamba Yeye alikuwa pamoja nasi, kwa ule ufufuo. Na kama wale waliokuwa wakitoka Emau, Yeye ametutokea asubuhi ya leo na kufanya jambo fulani jinsi Yeye alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, kwa hiyo tunajua ya kwamba Yeye amefufuka kutoka kwa wafu. Na, Shetani, tunakuja katika Jina Lake, Jina la Yesu, pamoja na Nguvu za Kristo. Nawe umeshindwa, nawe ni laghai tu. Na kama tutaukubali ulaghai wako, ungetuua kabla ya wakati wetu. Lakini huwezi kufanya hivyo. Tunakuja, tukitolea hilo changamoto kwa Neno la Mungu, kwa mateso ya uwakilisho wa Yesu. Tunaushinda ulaghai wako. Tunakupa changamoto, ewe Shetani. Nasi tunamfuatilia kondoo huyo, kama vile yule simba katika siku za Daudi. Tunakuja kumrudisha kondoo huyo kwenye afya njema na nguvu. Waachilie, katika Jina la Yesu Kristo! Toka mahali hapa! Toka ndani ya watu hawa, Shetani! Tunakukemea, katika Jina la Yesu Kristo. Waachilie, kwa kuwa kwa Jina la Kristo, tunawarudisha kwenye Kiti cha Enzi cha Baba asubuhi ya leo, pamoja na afya na nguvu, kupitia Jina la Yesu Kristo.

336 Ninyi watu wote sasa mnaoamini ya kwamba maombi ya imani yameombwa, ya kwamba umeweka mikono yako juu ya mtu fulani, ya kwamba umeamini, na kuamini ya kwamba Kristo amewaponya, nawe unaamini ya kwamba umeponywa kwa sababu mtu huyo alikuombea, nawe unakubali sasa hivi ya kwamba umeponywa, sijali jinsi ulivyo kiwete, jinsi ulivyo kipofu, jinsi ulivyo kiziwi, vyovyote ulivyo, jinsi ulivyo dhaifu, jinsi ulivyo mgonjwa, simama kwa miguu yako, katika Jina la Yesu Kristo, na ulikubali. Amina. Simameni, kila mahali, haijalishi kuna shida gani. Simameni kwa miguu yenu, inueni mikono yenu na kumsifu Mungu kwa ajili ya wema Wake. Amina.

62-0218 Kung'ang'ania
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org